# MATUMIZI YA MBINU YA MAIGIZO KATIKA UFUNDISHAJI WA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI, KAUNTI YA NAIROBI, KENYA

**KIKECHI KOMBO BATHOLOMEW**

**E55/CE/22908/2010`**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA MAWASILIANO YA ELIMU NA TEKNOLOJIA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA ELIMU YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**JUNI, 2022**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na wala haijawasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine.

**Sahihi**__________________**Tarehe** 23/06/2022

**Kikechi Kombo Batholomew**

E55/CE/22908/2010

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi waliochaguliwa na Chuo Kikuu

**Sahihi**__________________**Tarehe** 24/6/22

**Dkt Hamisi Babusa Omar**

Idara ya Mawasiliano ya Elimu na Teknolojia

Chuo Kikuu cha Kenyatta

**Sahihi**__________________**Tarehe** 24/06/2022

**Dkt Florence Abuyeka Miima**

Idara ya Mawasiliano ya Elimu na Teknolojia

Chuo Kikuu cha Kenyatta



ii

## YALIYOMO

**UNGAMO** ........ **ii**
**YALIYOMO** ........ **iii**
**ORODHA YA MAJEDWALI** ........ **viii**
**ORODHA YA MICHORO** ........ **ix**
**VIFUPISHO VYA MANENO** ........ **x**
**TABARUKU** ........ **xi**
**SHUKRANI** ........ **xii**
**ABSTRACT** ........ **xiii**
**IKISIRI** ........ **xiv**
**SURA YA KWANZA** ........ **1**
**UTANGULIZI** ........ **1**
1.1 Usuli wa Utafiti ........ 1
1.2 Suala la Utafiti ........ 10
1.3 Lengo la Utafiti ........ 11
1.4 Madhumuni ya Utafiti ........ 11
1.5 Maswali ya Utafiti ........ 12
1.6 Umuhimu wa Utafiti ........ 13
1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti ........ 14
1.8 Misingi ya Nadharia ........ 14
1.9 Kielelezo Dhanifu ........ 18
1.10 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu ........ 20
**SURA YA PILI** ........ **21**
**MAPITIO YA MAANDISHI** ........ **21**
2.1 Utangulizi ........ 21
2.2 Mbinu Zinazotumiwa Kufundisha Kipengele cha Wahusika Katika Riwaya ya Kiswahili ........ 22
2.3 Kiwango cha Matumizi ya Mbinu ya Maigizo katika Kufundisha Kipengele cha Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili ........ 29

2.4 Athari ya Mbinu ya Maigizo kwa Uelewa wa Wanafunzi katika Ufundishaji wa Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili............................................ 32
2.5 Mtazamo wa Walimu na Wanafunzi katika Utumizi wa Mbinu ya Maigizo katika Ufundishaji wa Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili............... 35
2.6 Changamoto katika Matumizi ya Mbinu ya Maigizo katika Ufundishaji wa Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili .................................................. 38
2.7 Pengo la Utafiti.......................................................................................... 43
**SURA YA TATU........................................................................................ 46**
**MUUNDO NA MBINU ZA UTAFITI ...................................................... 46**
3.1 Utangulizi ................................................................................................. 46
3.2 Muundo wa Utafiti ................................................................................... 46
3.2.1 Vigeu vya Utafiti ..................................................................................... 47
3.3 Eneo la Utafiti .......................................................................................... 47
3.4 Idadi Iliolengwa ........................................................................................ 47
3.5 Sampuli Mahususi..................................................................................... 48
3.6 Vifaa vya Kukusanya Data........................................................................ 49
3.6.1 Mitihani kuhusu Wahusika katika Riwaya............................................... 49
3.6.2 Mahojiano kwa Makundi lengwa ya Mijadala ya Wanafunzi ................. 50
3.6.3 Hojaji ya Walimu...................................................................................... 50
3.6.4 Mwongozo wa Mahojiano ya Walimu...................................................... 51
3.6.5 Uchunzaji Darasani .................................................................................. 51
3.7 Majaribio ya Vifaa vya Utafiti .................................................................. 52
3.8 Uthabiti na Uaminifu wa Vifaa vya Utafiti............................................... 53
3.8.1 Uthabiti wa Vifaa vya Utafiti................................................................... 53
3.8.2 Uaminifu wa Vifaa vya Utafiti ................................................................ 53
3.9 Utaratibu wa Ukusanyaji Data .................................................................. 54
3.10 Uchanganuzi wa Data.............................................................................. 55
3.10.1 Mbinu Zilizotumiwa katika Ukusanyaji, Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data..................................................................................................... 56
Mbinu hizi zilifafanuliwa kwa kurejelea madhumuni yafuatayo ya utafiti...... 56

3.11 Suala la Maadili ........................................................................ 58
**SURA YA NNE ........................................................................ 59**
**UWASILISHO, UCHANGANUZI NA MAJADILIANO YA MATOKEO YA UTAFITI ........................................................................ 59**
4.1 Utangulizi ........................................................................ 59
4.2 Demografia ya Wahojiwa ........................................................................ 60
4.2.1 Usambazaji wa Hojaji ........................................................................ 60
4.2.2 Jinsia ya Walimu Wanaofundisha Fasihi ........................................................................ 61
4.2.3 Umri wa Walimu Wa Fasihi ........................................................................ 61
4.2.4 Kiwango cha Elimu ........................................................................ 63
4.2.5 Tajiriba Katika Ufundishaji wa Kiswahili ........................................................................ 64
4.2.6 Vipindi vya Riwaya ........................................................................ 65
4.2.7 Jinsia ya Wanafunzi ........................................................................ 65
4.2.8 Umri wa Wanafunzi Walioshiriki katika UtafitiSehemu hii ilibaini miaka ya wanafunzi walioshiriki katika utafiti huu. Mchoro 4.6 uliwakilisha umri wao. ........................................................................ 67
4.3 Mbinu za Ufundishaji wa Kipengele cha Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili ........................................................................ 68
4.3.1 Mbinu za Kufundisha Wahusika katika Riwaya ilivyoripotiwa na Wanafunzi ........................................................................ 69
4.4 Kiwango cha Matumizi ya Mbinu ya Maigizo kwa Kufundisha Kipengele cha Wahusika ........................................................................ 73
4.4.1 Kiwango cha Matumizi ya Mbinu ya Maigizo katika Ufundishaji wa Wahusika ........................................................................ 73
4.4.2 Wanafunzi Walivyopatiwa Mazoezi Kupitia Nyenzo ya Ufanani .......... 74
4.5 Athari ya Matumizi ya Mbinu ya Maigizo katika Matokeo ya Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili ........................................................................ 76
4.5.1 Jinsi Mbinu ya Maigizo Ilivyowavutia Wanafunzi Nyakati za Mafunzo ya Wahusika ........................................................................ 76

4.5.2 Matokeo Kutokana na Uchunzaji ............................................................. 77
4.5.3 Mjarabu wa Fasihi (Riwaya ya Chozi la Heri) ......................................... 77
4.5.4 Uchanganuzi wa Mjarabu wa Kwanza ..................................................... 78
Kundi dhabiti ................................................................................................ 79
4.5.5 Uchanganuzi wa Mjarabu wa Mwisho ..................................................... 79
4.6 Mitazamo ya Walimu na Wanafunzi kuhusu Mbinu ya Maigizo katika Ufundishaji wa Riwaya ........................................................................ 83
4.6.1 Mitazamo ya Wanafunzi kuhusu Matumizi ya Mbinu ya Maigizo katika Ufundishaji wa Riwaya ........................................................................ 83
4.6.2 Maoni ya Wanafunzi Kuhusu Hisia Zao Kutokana na Matumizi ya Mbinu ya Maigizo ................................................................................................ 85
4.6.3 Mitazamo ya Walimu Kuhusu Matumizi ya Maigizo katika Ufundishaji wa Riwaya ................................................................................................ 86
4.6.4 Maoni ya Walimu kuhusu Umuhimu wa Matumizi ya Maigizo katika Vipindi vya Riwaya ........................................................................ 87
4.7 Changamoto katika Ufundishaji wa Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili ................................................................................................ 88
4.7.1 Changamoto za Ufundishaji Wahusika katika Riwaya Darasani ............. 89
4.7.2 Changamoto Zilizobainishwa na Wanafunzi ............................................ 90
4.7.3 Changamoto Zilizobainika Kupitia Mbinu ya Uchunzaji ....................... 90
**SURA YA TANO ........................................................................................ 92**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ................................ 92**
5.1 Utangulizi ................................................................................................ 92
5.2 Muhtasari ................................................................................................ 92
5.2.1 Mbinu za Ufundishaji Kipengele cha Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili ................................................................................................ 92
5.2.2 Kiwango cha Matumizi ya Mbinu ya Maigizo kwa Kufundisha Kipengele cha Wahusika ................................................................................ 93
5.2.3 Athari ya Matumizi ya Mbinu ya Maigizo katika Matokeo ya Wahusika katika Riwaya ................................................................................ 93

5.2.4 Mitazamo ya Wanafunzi na Walimu kuhusu Ufundishaji wa Wahusika katika Riwaya kwa kutumia Mbinu ya Maigizo ........................................ 94
5.2.5 Changamoto Zinazokumba Ufundishaji wa Wahusika Katika Riwaya ya Kiswahili ........................................................................................................ 94
5.3 Hitimisho ........................................................................................ 95
5.4 Mapendekezo ya Utafiti ................................................................ 97
5.4.1 Mapendekezo kwa Utafiti Zaidi .................................................. 99
**MAREJELEO** ........................................................................................ **101**
**VIAMBATANISHO** ................................................................................ **111**
**KIAMBATISHO A: HOJAJI YA MWALIMU** ........................................ **111**
**KIAMBATISHO B: HOJAJI YA WANAFUNZI** ...................................... **115**
**KIAMBATISHO C: MWONGOZO WA MAHOJIANO YA WANAFUNZI** ................................................................................ **117**
**KIAMBATISHO D: MWONGOZO WA MAHOJIANO YA WALIMU** ...................................................................................... **118**
**KIAMBATISHO E: MWONGOZO WA UCHUNZAJI DARASANI** ... **119**
**KIAMBATISHO F: MJARABU KCSE KISWAHILI FASIHI 102/3** .. **120**
**KIAMBATISHO G: MTIHANI WA KCSE MASWALI YA FASIHI 2015 – 2019** ........................................................................................ **126**
**KIAMBATISHO H: IDHINISHO** ............................................................ **130**
**KIAMBATISHO I: IDHINISHO** .............................................................. **131**
**KIAMBATISHO J: KIBALI CHA UTAFITI** .......................................... **132**
**KIAMBATISHO K: RAMANI YA NAIROBI (ENEO LA UTAFITI)** .. **133**

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali 1.1: Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili, KCSE Mwaka 2015-2019 ..... 8

Jedwali 1.2: Matokeo ya Mtihani wa Fasihi, 102/3 Kati ya Mwaka 2015-2019 8

Jedwali 1.3: Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili, Kaunti ya Kiambu, Nairobi na Machakos (2017-2019) ........................................................................ 9

Jedwali 1.4: Maswali ya Mitihani ya KCSE Fasihi Kuhusu Wahusika ............ 9

Jedwali la 3.1: Sampuli ya Utafiti .................................................................... 49

Jedwali la 3.2: Sampuli ya Kiwango cha Shule .............................................. 49

Jedwali 4.1: Vipindi vya Riwaya vilivyoripotiwa kufunzwa na Walimu ........ 65

Jedwali 4.2: Mikakati Iliyotumiwa na Walimu Kufundisha Wahusika katika Riwaya.......................................................................................... 68

Jedwali 4.3: Mbinu zilizotumiwa Kufundisha Wahusika zilivyoripotiwa na Wanafunzi ........................................................................................ 70

Jedwali 4.4: Uchunzaji kuhusu Mbinu zilizotumiwa na Walimu wa Riwaya ya Kiswahili Darasani ............................................................................. 71

Jedwali 4.5: Uzoefu wa Kutumia Mbinu ya Maigizo katika Ufundishaji wa Wahusika........................................................................................ 74

Jedwali 4.6: Athari ya Mbinu ya Maigizo katika Somo la Wahusika............. 76

Jedwali 4.7: Utuzaji wa Alama (Mjarabu wa Kwanza)................................... 78

Jedwali 4.8: Takwimu za Uchanganuzi wa Mjarabu wa Kwanza kati ya Kundi Jaribio na Kundi Dhabiti ..................................................................... 79

Jedwali 4.9: Utuzaji wa Alama (Mjarabu wa Mwisho).................................... 80

Jedwali 4.10: Takwimu za Mjarabu wa Kundi Dhabiti na Kundi Jaribio........ 81

## ORODHA YA MICHORO

Mchoro 1.1 Uhusiano kati ya Matumizi ya Mbinu ya Maigizo katika Ufundishaji wa Wahusika na Matokeo katika Riwaya ya Kiswahili. ..................................................... 19
Mchoro 4.1 Jinsia ya Walimu Wanaofundisha Fasihi ................................................... 61
Mchoro 4.2 Umri wa Walimu wa Fasihi ........................................................................ 62
Mchoro 4.3 Walimu wa Fasihi Kulingana na Kiwango cha Elimu ................................ 63
Mchoro 4.4 Tajiriba katika ufundishaji wa Kiswahili .................................................... 64
Mchoro 4.5: Uwasilishaji wa Wanafunzi wanaofundishwa riwaya Kijinsia ................. 66
Mchoro 4.6 Umri wa Wanafunzi ................................................................................... 67
Mchoro 4.7 Zoezi la kusoma kwa matumizi ya mbinu ya ufanani ................................ 75
Mchoro 4.8 Changamoto za Ufundishaji Wahusika katika Riwaya ............................... 89

## VIFUPISHO VYA MANENO

**BBC** : British Broadcasting Corporation

**CBC** : Comptence Based Curriculum

**GoK** : Goverment of Kenya

**KCSE** : : Kenya Certificate of Secondary Educatiion

**KICD** : Kenya Institute of Curriculum Development

**KNEC** : Kenya National Examinaton Council

**NACOSTI** : National Commission for Science, Technology and Innovation

**QASO** : Quality Assurance and Standards Officer

**TAC** : Teachers Advisory Centre

**T-Test** : Statistical Measure for Comparing Mean Scores for Two Groups

**SPSS** : Statistical Package for Social Sciences

**UNESCO** : United Nations, Educational, Scientific and Cultural Organisation.

## TABARUKU

Kwa kazi hii ninatabaruku na mke wangu, azizi Joyce Moi na wanangu; Kimberly Kombo na Vivian Kombo. Maombi na himizo lenu lisilokoma yalikuwa muhimu katika mchakato mzima wa kusomea shahada hii ya uzamili.

## SHUKRANI

Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa neema, nguvu na uwezo wa kuanza na kuhitimisha shughuli nzima ya kusomea shahada hii. Kwa unyenyekevu mwingi sana, ninawashukuru kwa dhati wasimamizi wangu; Dkt Hamisi Babusa Omar na Dkt Florence Abuyeka Miima, kwa kujitolea na kujikalifu kunielekeza kwa uangalifu mkubwa, pamoja na maelezo muhimu waliyonipa nilipokuwa ninaandika kazi hii ya utafiti. Mungu awajaalie mema katika siku zenu za halafu. Nina wingi wa matumaini kuwa, tasnifu hii ambayo ni tokeo la uelekezi wenu muruwa, itatoa mchango mkubwa katika tasnia ya elimu.

Vile vile ningependa kuwashukuru wahadhiri wangu wote katika Idara ya Mawasiliano ya Elimu na Teknolojia katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kunitia moyo nilipokuwa ninalemewa na kuemewa. Tajriba zao zilinifaa sana nilipokuwa ninaiboresha kazi hii. Nitakuwa mchache wa fadhila nisipokumbuka kuwashukuru walimu wakuu na walimu wote wa shule za upili kaunti ya Nairobi kwa kukubali kushirikishwa kwenye utafiti huu na kunipa maelezo na taarifa muhimu nilizohitaji kuhusu mada niliyokuwa naitafitia. Waama, pasipo mchango wao nisingeweza kuikamilisha kazi hii.

Mwisho, ninatoa shukrani nyingi sana kwa wazazi wangu James Kikechi na Albina Khakasa Kikechi waliojitolea sabili kunielimisha. Nitakuwa mtovu wa nidhamu nikosapo kumtaja Jeff aliyepiga chapa kazi ya tasnifu hii na kunisaidia pakubwa katika uhariri wake. Moyo wangu umejaa shukrani za dhati kwa mke wangu, mpendwa Joy Moi na binti zangu Kimberly na Vivian, kwa kunipa ari na kunitumainisha wakati moyo ulikuwa ukishuka na nguvu za kuendelea na utafiti kutishia kunitindika.

## ABSTRACT

This study aimed at investigating the use of drama in teaching characters in Kiswahili novels in public secondary schools in Nairobi County, Kenya. This study had the following objectives: to Investigate the methods used to teach characters in a Kiswahili novel;to investigate the extent which dramatization approach is being used to teach characters in Kiswahili novel;to establish the effect of dramatization on students' understanding in teaching characters in Kiswahili novel; to establish a) teachers b) learners perception on the use of dramatization in teaching characters in Kiswahili novel and to explore the challenges if any,facing the use of dramatization in teaching of characters in Kiswahili novel in public secondary schools in Nairobi County, Kenya. This study was guided by constructivism theory developed by Piaget. Quasi experimental design was employed for the purpose of this study. This study targeted a total of one hundred and one (101) secondary schools in Nairobi County which consist of two hundred and two (202) Kiswahili teachers and three thousand four hundred and fifty (3,450) form three students. This data was obtained at the head quarter of Nairobi county educaton office. Stratified sampling was used to select four (4) public schools: National, Extra County, County and Sub county public schools. Purposive sampling was used to select 2 teachers teaching Kiswahili from each of the four (4) sampled schools while simple random sampling was used to select two groups of thirty (30) form three students from each school translating to a total of 248 respondents (240 students and 8 teachers). Data was collected using standardized tests for students, interview, and questionnaire and observation schedule. The pilot study was carried out in one public school in Nairobi County which were not included in the final study. Piloting was done to enhance reliability and validity of the research tools. Questionnaires, document analysis (test-scores), interview schedules and observation schedules were used to collect data. Data collected was analyzed using Statistical Package for Social Sciences (SPSS version 21.0). Both quantitative and qualitative methods were used. Data collected was analyzed using descriptive statistics such as frequency and percentages. T-test was used to test for significance and mean difference between control and experimental groups at a significance level of 5 % ($p \leq .05$), level Confidence Interval of (95%). The analyzed data was presented using tables, pie charts and graphs. Findings revealed that reading aloud was the most preferred by many Kiswahili teachers in secondary schools in Nairobi County. Majority of students agreed that the use of lecture method was common in teaching characters in Kiswahili novel. Drama was rarely used in teaching characters in Kiswahili novels despite its significance in creating interest among students. Most teachers reported that majority of students enjoyed learning when drama was used in teaching and learning of characters. Experimental group performed better than the control group after examining the second test. This study concluded that there was a statistically significant differences between the experimental group and the control group in the post-test of the understanding scale of characters in Kiswahili novels in favour of experimental group. The research recommends that; teachers should be encouraged to use dramatization method in teaching characters in Kiswahili novels. The Ministry of Education needs to revise the Kiswahili curriculum by increasing number of lessons for Kiswahili Literature to provide time for the use of drama in teaching characterization in Kiswahili novels.

# IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundisha wahusika katika riwaya za Kiswahili katika shule za upili za umma, kaunti ya Nairobi, Kenya. Madhumini ya utafiti yalikuwa kuchunguza mbinu zinazotumiwa kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili; kuchunguza ni kwa kiwango kipi mbinu ya maigizo inatumiwa kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili; kubaini athari ya mbinu ya maigizo kwa uelewa wa wanafunzi katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili; kubaini mitazamo ya a) walimu b) wanafunzi katika utumizi wa mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili; na kutambua ikiwa kuna changamoto katika matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Ubunaji iliyoasisiwa na Piaget. Muundo Majaribio ulitumiwa kufanya utafiti huu. Utafiti huu ulilenga shule mia moja na moja (101), jumla ya walimu wa Kiswahili mia mbili na mbili (202) na wanafunzi elfu tatu mia nne hamsini (3,450) wa kidato cha tatu. Utafiti huu ulitumia mbinu ya utabakishaji kuchagua shule nne (4) kuwakilisha shule zote katika kaunti ya Nairobi. Walimu wawili Kiswahili waliteuliwa kwa njia ya kimakusudi kutoka kwa kila shule. Mbinu ya sampuli nasibu ilitumika kuchagua wanafunzi thelathini (30) kutoka katika kila shule. Kwa ujumla utafiti huu ulikuwa na sampuli ya watafitiwa mia mbili arobaini na wanane (248).Vifaa vya utafiti vilivyotumiwa kukusanya data ni mitihani, hojaji, mahojiano na uchunzaji darasani. Uaminifu na uthabiti wa vifaa vya ukusanyaji data ulifanywa katika shule moja ambayo haikuhusishwa katika utafiti kamili. Data ilichanganuliwa kwa kutumia Uchakataji wa data (SPSS Toleo la 21.0). Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa ujumla kwa kutumia idadi marudio na asilimia. T-test ilitumika kutathimini ubora wa matokeo baina ya kundi jaribio na kundi dhabiti kwa kiwango cha Uaminifu cha 95% (kiwango cha $P \leq 0.05$). Data iliyochanganuliwa iliwasilishwa kwa njia ya maelezo, grafu, pai chati na majedwali. Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa asilimia kubwa ya walimu walitaja usomaji kwa sauti ni mojawapo ya mbinu kuu iliyotumiwa kufunza fasihi katika shule za upili. Wanafunzi wengi walikiri mbinu ya mhadhara ndiyo ilitumiwa mara nyingi darasani kufundishia riwaya ya Kiswahili.Walimu waliohojiwa walikubali kwamba mbinu ya maigizo ilitumika katika ufundishaji wa wahusika mara moja tu kwa mwezi. Wanafunzi wengi walibaini matumizi ya mbinu ya maigizo haikutumiwa kamwe katika ufundishaji wa vipindi vya fasihi. Idadi kubwa ya wanafunzi walieleza kufundishwa kwa njia ya kuigiza kwa kuiga iliwasaidia kuelewa na kukumbuka wahusika kwa haraka. Matokeo ya mtihani wa mwisho wa kundi jaribio yalikuwa bora kuliko ya kundi dhabiti. Utafiti unahitimisha kwa kuonyesha kulikuwa na tofauti kubwa kati ya matokeo ya kundi jaribio na kundi dhabiti katika mtihani wa pili.Walimu wanapaswa kufundishwa namna ya kufundisha fasihi kwa kutumia mbinu ya maigizo katika madarasa yao. Walimu wanapaswa kufahamishwa kuhusu umuhimu wa matumizi ya mchezo wa kuigiza na majukumu yake katika kukuza fahamu za wanafunzi. Wizara ya elimu inahitajika kufanya marekebisho katika silabasi ya kiswahili kwa kuongeza vipindi vya fasihi ya Kiswahili. Hili litatoa muda wa kutosha kwa matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Utafiti

Kila taifa duniani lina fasihi yake kwa sababu penye matumizi ya lugha kwa njia ya ubunifu na penye jamii hapakosi kuwa na fasihi (Njogu, 1997). Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kwa njia ya ubunifu kuelezea historia ya binadamu na panapojiri suala la kihistoria, fasihi hulivalia njuga kulinasa na kulihifadhi kisanaa. Msokile (1992) anasema kuwa, kipengele cha riwaya kilianza kuimarika wakati wa chimbuko la viwanda huko Ulaya. Senkoro (1976) anasimulia riwaya ya Kiswahili ilichipuka wakati mswada *Uhuru wa Watumwa* ulipoandikwa na James Mbotela (1959). Inafahamika ndiyo ilikuwa riwaya ya mwanzo ya Kiswahili, masimulizi yake yalilenga mazingira ya Afrika Mashariki, wahusika na maudhui yake yalihusu Waswahili kwa hivyo ikawa rahisi kueleweka iliposomwa na wasomi na hata kuigizwa na wasanii wenye vipawa katika janibu za Afrika Mashariki.

Fasihi ina historia ndefu duniani, iliyowaletea waandishi sifa kwa karne nyingi hata kabla ya kufa kwa wengine wao (Chimerah, 2011). Riwaya ni kisa ambacho urefu wake unakiruhusu kitambe na kutambaa mahali pengi namna apendavyo mwandishi wake. Riwaya, basi ni hadithi ndefu ya kubuni yenye visa vingi, wahusika zaidi ya mmoja na yenye mazungumzo na maelezo yanayozingatia kwa undani na upana wa maisha ya jamii. Riwaya inatoa picha yote ya ujumla wa maisha ya mtu kutoka nyumbani hadi katika

kiwango cha taifa na hata dunia nzima. Riwaya ya Kiswahili ni utanzu mchanga ukilinganishwa na tanzu zingine za fasihi andishi ya Kiswahili (Mutembei, 2012).

Aina nyingi ya maigizo na michezo ya lugha hujenga ujuzi wa kuzungumza na kuandika (Zyoud, 2010). Uigizaji ni muhimu katika kuwezesha kujifunza kwa stadi ya kuzungumzia (Stephanie, 2011). Mbinu ya uigizaji ni matendo yanayojumuisha maonyesho ya michezo ya kuiga ama kuigiza, michezo ya lugha, majadiliano ya vikundi, mijadala na shughuli zingine za ufundishaji ambazo zinaweza kufafanuliwa chini ya mbinu za maigizo (Gomez, 2010). Matumizi ya maigizo kama zana ya kufundisha lugha na wahusika wa fasihi sio mapya (Moore, 2004). Kwa kurejelea historia, michezo ya kuigiza na maigizo kwa muda mrefu yamekuwa yakitambulika kama njia bora ya elimu na ujasusi (Beena, Nyagah, Kibui na Odundo, 2015). Njia zinazotumiwa leo, hata hivyo ni za kisasa na ni tofauti kwa kiwango fulani na zile zilizotumika awali. Utafiti unaonyesha kuwa kutumia mbinu za kuigiza darasani wakati wa kufundisha hutoa hisia za kuvutia kwa wanafunzi na kutaka kujifunza zaidi. Njia za kuvutia ambazo zina uwezo wa kutoa msisimko, udadisi na matamanio ya kuelezea jambo linaloweza kushughulikiwa zinaweza kufanikiwa sana katika kuteka mawazo na umakini wa vijana (Ozbek, 2014). Ni muhimu kuruhusu vijana kukubali jukumu la ujifunzaji wao wenyewe kwa wenyewe.

Maigizo hukusudia kuleta hali halisi darasani kwa sababu mwanafunzi huwekwa katika mazingira halisi na huhamasishwa kwa kuwa anahusika moja kwa moja. Inakuwa kifaa chenye nguvu cha kufundishia na kujifunzia na athari chanya juu ya utambuzi wa wanafunzi, kijamii, kimhemko na kiimani. Mchezo wa kuigiza darasani ni mbinu

inayofanikisha uwezo wa viwango vya wanafunzi wote kutangamana vizuri wanapofundishwa (Prochazka, 2004). Kuingizwa kwa uchangamano katika kufundisha na ujifunzaji wa wahusika huwapa wanafunzi nafasi ya kuelewa majukumu ya wahusika katika maisha halisi na kuboresha uelewaji wao darasani (Suter, 2013).

Uvumbuzi wa mbinu ya maigizo unaweza kufafanuliwa kama mkusanyiko wa mbinu za kufundishia zenye msingi wa kuigiza na kujifunza ili kuwashirikisha wanafunzi katika uzoefu mzuri wa kusoma. Shughuli za kuigiza zinaweza kutoa utimilifu bainifu kati ya mwingiliano wa kijamii katika viungo viwili vya ulimwengu ajabu na ulimwengu halisi wa mchezo wa kuigiza (Ranzau, 2016). Michezo ya lugha inaweza kutumika kufundisha wahusika kwa sababu wanafunzi wanapenda kushiriki michezo ya kufurahisha (Tan, 2008). Wanafunzi hupenda kufanya mazoezi ya mwili wanapokuwa wanajifunza kwa sababu hali hii huchangia kufikiria na kukuza ubunifu wao. Kwa hivyo, walimu hawapaswi kuona michezo kama vifaa tu bali waijumuishe katika ujifunzaji wa lugha kwa kuiweka katika muktadha wenye maana katika ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili.

Kulingana na Mwihaki (2011), utumiaji bora wa Kiswahili unategemea aina ya shule, njia za kufundishia na mtazamo wa wanafunzi kuhusu lugha ya Kiswahili. Kunaweza kuwa na sababu zingine nyingi zinazochangia kuathiri matumizi ya Kiswahili fasaha nchini Kenya kama inavyoonekana dhahiri katika matokeo ya mtihani. Kirui (2015) alifanya utafiti juu ya utumiaji wa mbinu za kuigiza katika kufundisha na kujifunza lugha ya Kiswahili katika shule za upili. Hata hivyo, utafiti huo ulirejelea tu matumizi ya

maigizo katika kufundisha lugha ya Kiswahili wala hakushughulikia mbinu hiyo katika kufundisha fasihi ya Kiswahili.

Utafiti uliofanywa na Munther (2013) ulithibitisha kuwa ufanani miongoni mwa wanafunzi unaimarisha mawasiliano yao na hivyo kuboresha matokeo ya wanafunzi. Hali hii inasaidia wanafunzi kuondoa hofu ya kimhemko, makosa ya sarufi na vikwazo vya kijamii. Maigizo kama mkakati wa kufundisha umetumika kukuza na kuimarisha jukumu la lugha ya Kiswahili katika kufaulu kwa wanafunzi. Kwa mfano, Zyoud (2010) alielezea kwamba michezo ya kuigiza, ufanani, sanaa tuli na michezo ya lugha huchochea uimarishaji wa ujuzi wa mwanafunzi. Stephanie (2011) anasema maigizo yanapotumika katika kufundisha na kujifunza lugha kwa mfano utoaji wa hotuba, mwanafunzi hujenga stadi imara ya kuongea ambayo huchangia ari ya kufaulu kwake. Walimu wanapokosa kuhusisha mbinu ya maigizo katika ufundishaji, stadi ya mazungumzo kwa kiasi kikubwa hukosa kuimarika miongoni mwa wanafunzi. Prasad (2011) ameongeza kuwa wanafunzi huongea lugha sanifu mbinu ya maigizo inapotumika na hivyo huendeleza stadi ya kuongea zaidi. Kulingana na Heather (2011) ujifunzaji lugha ya Kiswahili huchangiwa zaidi na uhusishajiwa mhusika katika maswala yanayohusu lugha hiyo.

Utafiti uliofanywa na Awad (2013) kuhusu michezo ya kuigiza katika ufundishaji wa lugha huko Gaza. Alithibitisha kwamba walimu wanapaswa kutumia mbinu ya maigizo katika kufundisha lugha ili kukuza maendeleo ya lugha miongoni mwa wanafunzi. Vilevile, alibaini kuwa ufanani huimarisha lugha ya wanafunzi wenye ufinyu wa msamiati. Kulingana na Munther (2013) matumizi ya sanaa tuli yalihusisha kufundisha

kupitia mawasiliano yasiyokuwa ya maneno ya moja kwa moja bali vitendo vilihusisha matumizi mengi ya hisia na ishara.

Kulingana na Kemboi na Osman (2015), maigizo ya majukumu ni zana yenye nguvu katika kufundisha na kujifunza kwani, inatoa mafunzo kamili katika safari ya nyanja nyingi za ufumbuzi, kujieleza na kushiriki pamoja hali ambayo huwakuza wanafunzi wote na walimu kupiga hatua kwa pamoja. Imebainika kuwa mbinu ya majukumu huongeza mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji katika viwango tofauti vya elimu kwa kuongeza motisha, kutunza na ushirikiano katika kazi (Hong, 2010). Utafiti huu pia utajaribu kuhakikisha ikiwa mbinu ya majukumu itatumika kufundisha wahusika katika riwaya kama moja wapo ya sehemu ya maigizo. Licha ya ukweli kwamba umuhimu wa riwaya umesisitizwa katika tafiti nyingi, hakuna utafiti mtafiti alipata unaoonyesha matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundishia wahusika katika riwaya za Kiswahili katika shule za upili. Kwa hivyo, huu uchunguzi utabaini mchango wa matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundisha wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi.

Mbali na Kiswahili kuwa somo la lazima na kutahiniwa katika shule za msingi na upili, mtalaa wa 8-4-4 ulipozinduliwa mwaka 1985, Shule za msingi zilipata fursa ya kufundishwa kipengele cha fasihi ya Kiswahili. Ripoti ya Koech (1999) ilihimiza Kiswahili kubakia somo la lazima katika shule za msingi na za upili na kutahiniwa kitaifa katika darasa la nane na kidato cha nne. Katika mabadiliko ya mtalaa yaliyofanywa mwaka wa 2002 na Taasisi ya Elimu Nchini Kenya (KICD). Somo la Kiswahili

liliongezewa vipengele vingine kama vile Fasihi Simulizi, Isimu-jamii na hadithi fupi (KICD, 2016). Katika mtalaa mpya wa C.B.C, mfumo wa 2-6-3-3-3 Kiswahili kimepewa nafasi kubwa katika shule za msingi. Kwa sasa somo hili linafunzwa na kutahiniwa katika gredi zote.

Baadhi ya utafiti ambao umewahi kufanywa kuhusu usomaji na ufundishaji wa fasihi umeonyesha walimu wengi wamekuwa wakiangazia kufundisha wanafunzi mbinu za kupita mtihani wa kitaifa. Mbae (2004) anakiri kwamba wanafunzi wanapofundishwa, walimu hurejelea sana vitabu vinavyotahiniwa. (KICD, 2002), mwanafunzi anapoelekezwa kusoma fasihi ya shule za upili, anapaswa kuelewa anachokisoma, ajue namna ya kusoma na apanue msamiati wake ili aweze kafurahia kutumia stadi zingine za lugha. Anatarajiwa kusoma na kupanua sarufi ambayo ataitumia anaposoma na kuwasilisha madhumuni ya vitabu vya fasihi vinavyochambuliwa darasani.

Lengo la kuendeleza lugha ya wasomaji ni kuongeza uwezo wao kwa mawasiliano ambayo ni muhimu katika hali halisi ya maisha (Wamitila, 2003). Anaendelea kusema ufundishaji wa riwaya unapaswa kuendelezwa kwa kutumia nyenzo ifaayo ili kuleta athari chanya ya kuzaa matokeo bora ya lugha. (Ellis, 2011). Hata hivyo mwalimu anapaswa kuwapa wanafunzi maarifa ya kutosha katika sarufi kabla ya kuanza kuchambua maudhui yoyote katika riwaya (Gathumbi, Kimaliro, Mugambi, Bwanya na Kiio, 2005). Mbinu za kufundishia na kujifunza zina ushawishi mkubwa katika kuboresha mafanikio ya mwanafunzi katika masomo mbalimbali (Henson, 2004). Pana uwezekano mkubwa kuwa mbinu ambazo walimu wanawajibikia kufundishia fasihi na

kutowahusisha wanafunzi ndio huenda imewafanya wanafunzi kukuza mwelekeo hasi katika uchambuzi mwafaka wa riwaya.

Utafiti uliofanywa na Wanjala na Kavoi (2013) wanapendekeza wanafunzi wasome riwaya na wawasilishe mtiririko mbele ya wenzao. Japo mbinu yenyewe ni ya kuchokesha, wanafunzi wazembe hutumia mbinu za udanganyifu kama kunakili kazi za wenzao ama kunukuu kwenye tahakiki mbalimbali.

Utafiti ulilenga matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi. Utafiti ulifanywa katika kaunti hii kwa sababu ya kurekodiwa kwa matokeo duni katika somo la Kiswahili kwenye mtihani wa (KCSE) kuanzia mwaka wa 2015 hadi 2019 (KNEC, 2019). Matokeo yameonyesha kuwa ya kiwango cha chini ya asilimia hamsini katika kategoria ya alama ya wastani. Inafahamika ya kuwa kaunti hii ina uwezo zaidi wa kutoa picha ya hali halisi ilivyo nchini Kenya kuhusu mbinu za ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Nairobi ndilo jiji kuu la Kenya kwa hivyo lina shule nyingi baadhi yazo zikitoa matokeo ya juu zaidi katika mtihani wa taifa.

**Jedwali 1.1: Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili, KCSE Mwaka 2015-2019**

| Mwaka | Karatasi | Watahiniwa | Upeo | Alama Wastani | Alama Tenganisho |
|---|---|---|---|---|---|
| **2015** | 1 | 521159 | 40 | 20.86 | 5.19 |
| | 2 | | 80 | 36.12 | 13.50 |
| | 3 | | 80 | 38.80 | 15.38 |
| | Jumla | | 200 | 95.76 | 31.02 |
| **2016** | 1 | 571,176 | 40 | 18.23 | 5.53 |
| | 2 | | 80 | 34.11 | 13.83 |
| | 3 | | 80 | 25.67 | 12.87 |
| | Jumla | | 200 | 77.97 | 29.07 |
| **2017** | 1 | 610,392 | 40 | 18.84 | 5.23 |
| | 2 | | 80 | 25.45 | 11.79 |
| | 3 | | 80 | 25.15 | 13.42 |
| | Jumla | | 200 | 69.43 | 27.49 |
| **2018** | 1 | 659,465 | 40 | 16.98 | 4.82 |
| | 2 | | 80 | 27.22 | 10.88 |
| | 3 | | 80 | 22.20 | 11.95 |
| | Jumla | | 200 | 66.40 | 24.76 |
| **2019** | 1 | 694,982 | 40 | 19.88 | 5.43 |
| | 2 | | 80 | 36.50 | 12.64 |
| | 3 | | 80 | 21.08 | 12.64 |
| | Jumla | | 200 | 77.46 | 28.03 |

**Asilia**: (KNEC. Matokeo ya Mtihani wa Kitaifa wa Kiswahili Mwaka 2015-2019)

**Jedwali 1.2: Matokeo ya Mtihani wa Fasihi, 102/3 Kati ya Mwaka 2015-2019**

| Mwaka | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Alama wastani** | 38.80 | 25.67 | 25.15 | 22.20 | 21.08 |
| **Alama ya tenganisho** | 15.38 | 12.87 | 13.42 | 11.95 | 12.64 |

**Asilia (KNEC. Matokeo ya Mtihani wa Fasihi, 102/3 Kati ya Mwaka 2015-2019)**

**Jedwali 1.3: Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili, Kaunti ya Kiambu, Nairobi na Machakos (2017-2019)**

| MWAKA/ KAUNTI | 2017 | 2018 | 2019 |
|---|---|---|---|
| **Kiambu** | 3.93 | 4.10 | 4.64 |
| **Nairobi** | 4.38 | 4.43 | 4.61 |
| **Machakos** | 3.31 | 3.71 | 4.21 |

**Asilia**: (KNEC Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili, Kaunti ya Kiambu, Nairobi na Machakos mwaka 2017-2019)

Maswali ya riwaya katika mtihani wa kitaifa kati ya mwaka 2015-2019. Ripoti za KNEC zinaonyesha asilimia kubwa ya maswali yalilenga wahusika na watahiniwa hawakufanya vizuri.

**Jedwali 1.4: Maswali ya Mitihani ya KCSE Fasihi Kuhusu Wahusika**

| Mwaka | Idadi ya maswali | Idadi ya maswali kuhusu wahusika | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **2015** | 4 | 4 | 100 |
| **2016** | 4 | 2 | 50 |
| **2017** | 5 | 4 | 80 |
| **2018** | 6 | 5 | 83 |
| **2019** | 5 | 4 | 80 |
| **Jumla** | **24** | **19** | **79** |

Tathimini ya maswali yaliyotahiniwa kati ya mwaka 2015-2019, inabaini maswali kuhusu wahusika kila mwaka huwa zaidi ya asilimia 50. Kwa jumla ya miaka mitano ni asilimia 79. Hali hii imechangia pakubwa matokeo yasiyoridhisha na sababu inaweza kukisiwa kuwa mbinu zinazotumiwa katika ufundishaji wa kipengele hiki namna inavyodaiwa katika ripoti za kila mwaka za Baraza la KNEC (KNEC. Matokeo ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili mwaka 2015-2019). Kwa hivyo utafiti huu unanuia kuchunguza namna mbinu ya maigizo inavyoweza kutumiwa katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya

za Kiswahili kama mojawapo wa mbinu zinazowashirikisha wanafunzi moja kwa moja katika mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji.

Vipengele muhimu katika ufundishaji wa riwaya ni dhamira, maudhui, fani za lugha, mtindo, mandhari na wahusika japo katika mtihani wa taifa, wanafunzi hutahiniwa katika sehemu tatu za Insha 102/1, Lugha 102/2 na Fasihi 102/3 (KNEC 2005). Katika somo la fasihi sehemu tano ndizo hufunzwa na kutahiniwa: riwaya, tamthlia, hadithi fupi, fasihi simulizi na ushairi. Utafiti huu ulilenga sehemu ya riwaya kuhusu matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufudishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

## 1.2 Suala la Utafiti

Tafiti zimeonyesha kwa ujumla kuwa matumizi bora ya maigizo yanaweza kuboresha pakubwa matokeo ya wanafunzi katika somo la Kiswahili.

Kuna tafiti ambazo zimefanywa kuhusu fasihi kwa jumla lakini kuna pengo katika matumizi ya maigizo katika kufundishia kipengele cha wahusika ambacho ni muhimu sana katika ufundishaji wa fasihi kwa jumla, jambo ambalo lilimsukuma mtafiti kutafutia.

Kitengo kikuu katika msuko wa riwaya ni wahusika. Kipengele hiki kimesawiriwa kama kiungo kikuu katika kazi nzima ya riwaya ya Kiswahili. Kwa hivyo umuhimu wa kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ni kuwezesha wanafunzi kuelewa ploti, dhamira, maudhui, fani za lugha na mandhari ya matukio katika riwaya ya Kiswahili.

Katika mtihani wa kitaifa maswali mengi hulenga kipengele hiki na hivyo mwanafunzi asipofunzwa vizuri hutatatizika katika kujibu maswali ya fasihi. Ripoti za KNEC

zinaonyesha maswali yanayolenga wahusika katika riwaya hayafanywi vizuri na hali hii inadhihirika katika kaunti ya Nairobi.

Maswali ya wahusika hulenga mtahiniwa kubaini sifa za wahusika, mandhari ya wahusika, ploti na mchango wa wahusika katika ukuzaji wa maudhui riwayani. Kwa hivyo, utafiti huu ulichunguza ikiwa mbinu ya maigizo ingeweza kuimarisha ufundishaji wa wahusika katika riwaya ili kuboresha uelewaji na matokeo ya Kiswahili (KNEC, 2019).

### 1.3 Lengo la Utafiti

Lengo la utafiti huu ni kuchunguza ikiwa mbinu ya matumizi ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili inaweza kuimarisha matokeo ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi. Lengo hili litaafikiwa kwa kupitia madhumuni yalioyoorodheshwa katika kipengele cha 1.4.

### 1.4 Madhumuni ya Utafiti

i) Kuchunguza mbinu zinazotumiwa kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi.

ii) Kuchunguza ni kwa kiwango kipi mbinu ya maigizo inatumiwa kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi.

iii) Kubaini athari ya mbinu ya maigizo kwa uelewa wa wanafunzi katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi.

iv) Kubaini mitazamo ya a) walimu b) wanafunzi katika utumizi wa mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi.

v) Kuchunguza ikiwa kuna changamoto katika matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi.

### 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo:

i) Ni mbinu zipi zinatumika kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi?

ii) Je, ni kwa kiwango kipi mbinu ya maigizo inatumika katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi?

iii) Mbinu ya maigizo ina athari gani katika uelewa wa wanafunzi katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi?

iv) Je, a) Walimu b) Wanafunzi wana mtazamo gani kuhusu utumizi wa mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi?

v) Je, kuna changamoto zozote zinazokumba matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unatarajiwa kutoa mchango mkubwa katika kuwaongoza watunga sera na walimu katika juhudi zao za kuboresha mbinu bora za ufundishaji kuzalisha matokeo bora katika somo la Kiswahili.

Utafiti utasaidia katika uboreshaji wa nadharia na mazoezi ya ukuzaji wa mitaala nchini Kenya kwa kuongeza ujuzi mpya katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi na lugha katika shule za upili nchini. Matokeo ya utafiti yanatazamiwa kuwa yenye manufaa kwa Wizara ya elimu katika kutoa mwelekeo, ulinganisho na marejeleo katika kufundisha na kuchambua kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

Zaidi ya hayo, matokeo ya utafiti huu yatasaidia katika kutoa tathimini ya kina na muhimu kuhusu namna ya kufanikiwa kwa wanafunzi kwa kutumia mbinu bora za kuchambua riwaya katika shule za upili nchini Kenya. Kwa kurejelea matokeo ya utafiti. Wakuza mitaala nchini Kenya (KICD) wataratibia kufanyika kwa warsha na makongamano ya walimu wa Kiswahili katika shule za upili. Katika mikutano hii washika dau watajadili na kuwaelekeza walimu kuhusu matumizi ya mbinu ya maigizo na mikakati inayofaa kushirikishwa katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

Matokeo ya utafiti yanatarajiwa kuwasukuma washika dau katika sekta ya elimu na watunga ruwaza za elimu kuwajibikia kuwaelekeza walimu namna ya kutumia mbinu ya maigizo kufundishia riwaya katika shule za upili. Kituo cha ushauri kwa walimu (TAC) na maafisa wa ukadiriaji wa ubora na viwango vya elimu (QASO) watashiriki kuwafunza walimu wa fasihi katika kozi za muda mfupi kuhusu mbinu za ufundishaji kwa

kujumuisha matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji na ujifunzaji wa wahusika katika riwaya za Kiswahili. Kwa upande mwingine matokeo ya utafiti yataisaidia wizara ya elimu kuweka mikakati mipya katika mbinu za ufundishaji kwa kuipa mbinu ya maigizo nafasi kubwa kutumiwa kufundisha wahusika katika kipengele cha riwaya ya Kiswahili

## 1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti ulilenga kubaini matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundishia wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi. Shule 4 pekee kati ya 101 zilichaguliwa kutoka katika kila kiwango, kuwakilisha shule zote. Mtindo wa utabakishaji ulitumika kutegemea kiwango cha shule, yaani iwapo ni ya kitaifa, kikanda, kaunti na kaunti ndogo. Wanafunzi wa kidato cha tatu waliokuwa wanachambua riwaya ndio walihusishwa katika utafiti. Riwaya ya Chozi la Heri (Assumpta, 2021) ilihusishwa kwa sababu ndiyo riwaya iliyoidhiniswa kutahiniwa shuleni na KICD

Ukusanyaji, uainishaji na uchanganuzi wa data ya utafiti ulijikita katika madhumuni ya utafiti yaliyochangia kubaini matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya kiswahili katika shule za upili.

## 1.8 Misingi ya Nadharia

Utafiti ulirejelea nadharia ya Ubunaji iliyoasisiwa na Piaget (1995). Ubunaji ni nadharia ya misingi ya uchunguzi na utafiti wa kisayansi kuhusu jinsi watu hujifunza. Elimu ya ubunaji ni msingi wa imani kwamba kujifunza hutokea ikiwa wanafunzi hushiriki kwa namna hai badala ya kuwa kimya kupokea maarifa (Mayer, 2004). Wanafunzi ni wazalishaji wa maarifa na ufahamu. Mafundisho ya ubunaji yanaelekeza wanafunzi kuwa

wasomi muhimu na kuwafanya kuwa na motisha ya kujitegemea. Mfumo huu wa kinadharia unaonyesha kwamba maarifa mapya hujengwa juu ya maarifa miliki huku mazingira yakiongoza kujifunza huko. Kwa hiyo, wakati mwalimu anapochanganua wahusika, wanafunzi wanapaswa kushiriki kikamilifu kwa kuigiza sifa za wahusika hao. Wahusika hutoa maamuzi katika kujifunza badala ya kujifunza kuwa watazamaji tu. Hii itasaidia wanafunzi katika kujenga uelewaji wao juu ya mchakato mzima binafsi wa kujifunza. Mwanafunzi apewe nafasi ya kushiriki katika mchakato wa kujifunza ili kuimarisha uzoefu wa kujifunza. Hali hii humpa motisha ya ndani ya kujifunza mwenyewe. Mihimili ya nadharia hii ni matumizi ya mazingira ya mtu kujifunza kwa kushiriki kwa namna iliyo hai. Huzingatia namna ya kushiriki na ujifunzaji wenyewe katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, mwalimu anapaswa kuwaelekeza wanafunzi kubaini ploti, mandhari ya wahusika, maudhui na fani za lugha.

Nadharia ya Ubunaji haitambui tu kuwa wanafunzi wana tofauti nyingi kutokana na mazingira waliyolelewa na tamaduni zao, bali hutia motisha wanafunzi kuhifadhi tamaduni hizo kama sehemu muhimu ya mchakato wa kujifunzia (Wertsch, 1997). Nadharia hii husisitiza ya kuwa mtu lazima apewe nafasi kufikia malengo yake kwa mujibu wa mtazamo wake.Hii inaweza kufanikishwa na msukumo kutoka kwa mazingira alimolelewa yakifungamanishwa na utamaduni katika mtazamo wake wa dunia. Panapokosekana mijadala baina ya wanafunzi limbukeni na kutengemea majadiliano ya watu walio na ujuzi ambao ni walimu. Husababisha wanafunzi hao kukosa kupata ufahamu wa kudumu (Tam, 2000). Kwa kurejelea muktadha huu, mtafiti anabaini kuwa

nadharia ya Ubunaji ndio njia bora ya kufafanua kuhusu kusoma na kupata maarifa mapya. Inaelezea zaidi kuwa ili kukuza ueleewaji mwepesi wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili ni muhimu kuwahusisha wanafunzi na kile wanachosoma moja kwa moja. Kwa hivyo ili kujenga ufahamu wao wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili ni lazima pawepo na mazingira madhubuti yanayowezesha wanafunzi kushiriki moja kwa moja. Nadharia hii inasisitiza kuwa ili kumjenga mwanafunzi katika mtazamo chanya lazima awekwe katika mazingira shirikishi. Kwa hivyo, matumizi ya maigizo yatawapa wanafunzi motisha ya kushiriki zaidi wanaposoma.

Watoto wadogo hukuza uwezo wao wa kufikiri kwa kuzungumza na watoto wengine, watu wazima na mazingira inayowazunguka. Kufuatia hayo nadharia hii inasisitiza kuwa muhimu kuzingatia mazingira na utamaduni wa mwanafunzi katika mchakato wa kujifunza. Mazingira  na utamaduni ni muhimu kwa kufanikisha ufahamu hasa kwa kutumia mifano inayofahamika na mwanafunzi (Huitt, 2003).

Aidha, nadharia hii inashadidia kuwa msukumo wa nafsi ya mwanafunzi ndio unapaswa kumpa jukumu la kujifunza na kuelewa dhana mbalimbali za mazingira yake (Glasersfeld, 1989). Kwa hivyo, nadharia hii inasisitiza umuhimu wa kushirikisha mwanafunzi ipasavyo  katika ufundishaji, tofauti na mbinu za hapo awali ambapo jukumu ya kufunza na kujifunza iliwachiwa mwalimu na mwanafunzi alibaki kuwa mtazamaji tu Oliver, (2000). Anasema kuwa mtu anapokumbana na kitu kigeni hujaribu kukifahamu kwa kukifungamanisha na mawazo yake pamoja na uzoefu wake wa jadi. Wakati mwingine hukubali kubadilisha fikra zake kwa kukubali kuongezea maarifa mapya,

wakati mwingine mawazo yake humsukuma kutupilia mbali ujumbe aliojifunza kuwa hauna umuhimu. Hata hivyo binadamu ni muumbaji wa maarifa na akili yake. Kufanya hivi tunapaswa kujiuliza maswali, tuchunguze na tutathimini yale tunayoyajua.

Nadharia ya Ubunaji ilikuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti huu kwa sababu ilirejelea ubunifu kama mbinu ya kufundishia. Kwa hivyo wanafunzi walijijengea maarifa wenyewe badala ya kutegemea kupokea kutoka kwa walimu wenye tajiriba katika taaluma ya uchambuzi wa wahusika katika riwaya ya kiswahili. Nadharia hii inahimiza uzoefu wa watu kujenga maarifa mapya wanapotangamana na mazingira mapya. Kwa hivyo, kwa kusudi la kufunza wahusika katika riwaya za Kiswahili, mwalimu lazima apange shughuli ambazo hazijumuishi tu kile wanafunzi wana uwezo wa kufanya peke yao bali pia kile wanachoweza kujifunza kwa kushirikiana na wengine.


Nadharia hii ilifaa utafiti huu kwa kutambua mbinu zilizotumiwa kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili, kuchunguza kwa kiwango kipi mbinu ya maigizo ilitumiwa kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili, kubaini athari ya mbinu ya maigizo kwa uelewa wa wanafunzi katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili, kuchunguza mtazamo wa walimu na wanafunzi katika utumizi wa mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili na kutambua ikiwa kuna changamoto katika matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

### 1.9 Kielelezo Dhanifu

Kielelezo dhanifu kinaonyesha mwingiliano wa vigeu huru, vigeu viingilizi na vigeu tegemezi. Mbinu tofauti za maigizo huamsha ari ya wanafunzi kutaka kushiriki katika maigizo hivyo kuelewa usawiri wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Ikiwa patakuwa na changamoto kubwa katika matumizi ya nyezo hizi, itakuwa vingumu wanafunzi kufunzwa na kujifunza.

Vigeu huru katika utafiti huu ni; mbinu zinazotumika kufundisha kipengele cha wahusika, mbinu za maigizo na mitazamo ya wanafunzi na walimu kuhusu mbinu ya maigizo. Katika vigeu tegemezi kuna matokeo bora katika mtihani, uchambuzi mwafaka wa wahusika, uwezo wa wanafunzi kuigiza darasani na mielekeo ya wanafunzi. Hata hivyo, uhusiano baina ya matumizi ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili ulikuwa na vigeu viingilizi kadhaa kama Idadi ya vipindi vya fasihi, mazingira ya wanamofundishiwa, vitabu vya riwaya na motisha na uzoefu wa mwanafunzi katika uchambuzi wa riwaya. Vigeu viingilizi huingiliana na vigeu huru ili kuzalisha vigeu tegemezi.

Kielelezo dhanifu cha utafiti huu kimesawiriwa katika mchoro ufuatao.




**Mchoro 1.1 Uhusiano kati ya Matumizi ya Mbinu ya Maigizo katika Ufundishaji wa Wahusika na Matokeo katika Riwaya ya Kiswahili.**

### 1.10 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu

**Athari ya Mbinu :** Matokeo ya mbinu za ufundishaji

**Changamoto katika Matumizi:** Matatizo katika matumizi ya mbinu za ufundishaji.

**Mbinu za Ufundishaji:** Njia mahususi zinazotumiwa katika ufundishaji wa riwaya.

**Maigizo**: Ni sanaa katika kazi ya fasihi inayohusisha matendo ya wahusika katika jamii. Waigizaji huyaiga matendo hayo na kuyaonyesha mbele ya hadhira.

**Riwaya:** Nathari ndefu iliyotungwa yenye visa vinavyosimulia kuhusu utangamano na tajiriba ya mwanadamu.

**Ubunifu:** Uvumbuzi wa mbinu zinazorahisisha mawasiliano katika ufundishaji.

**Ufundishaji:** Kitendo kinachomwezesha mtu kupata ujuzi, maarifa, maadili au mwelekeo.

**Ujifunzaji:** Kitendo cha kupokea mafunzo, maarifa, mwelekeo, ujuzi, maadili, kwa wanafunzi ili waelewe.

**Vigeu:** Vibadala vinavyoweza kuathiri au kuathiriwa katika utafiti

**Wahusika**: Ni viumbe hai au wasiokuwa na uhai ambao huchorwa na mwandishi ili kufikisha ujumbe kwa wasomaji wa riwaya

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, tafiti za awali za wasomi zinazohusiana na mbinu za ufundishaji ziliangaziwa. Tafiti hizi zilichanganuliwa kwa kuzingatia lengo la utafiti ambalo ni matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi. Maigizo ni sanaa katika kazi ya fasihi inayohusisha matendo ya wahusika. Waigizaji huiga matendo yanayofanywa na watu katika jamii na kuyaonyesha mbele ya hadhira.

Wamitila (2003) anasema kwamba riwaya ni kazi iliyoandikwa kwa mtindo wa kinathari ambayo ina urefu wa kiasi fulani, ni pana, ina uchangamano wa kimtindo na kidhamira na inashughulikia masuala kadha katika mtazamo mpana wa wakati. Kwa ujumla, riwaya ni aina ya utanzu mojawapo wa fasihi andishi na ni hadithi ndefu ya kubuni yenye kutumia lugha ya kinathari, yenye mwingiliano wa visa na mikasa mbalimbali, wahusika wengi wenye kushikamana, pamoja na fani na maudhui yaliyotimia kwa lengo la kuwasilishwa kwa jamii husika. Mada zilipangwa kwa kurejelea madhumuni ya utafiti kama ifuatavyo**:**

i) Mbinu zinazotumiwa kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili

ii) Kiwango cha matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili

iii) Athari ya mbinu ya maigizo kwa uelewa wa wanafunzi katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

iv) Mtazamo wa walimu na wanafunzi katika utumizi wa mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

v) Changamoto katika matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

## 2.2 Mbinu Zinazotumiwa Kufundisha Kipengele cha Wahusika Katika Riwaya ya Kiswahili

Mbinu za kufundishia ni sehemu muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mbinu ya kufundishia inapaswa kuwa na mwelekeo wa kupitisha habari kutoka sehemu moja hadi nyingine kupitia vyombo mwafaka vya mawasiliano ili kufanikisha suala hili, maagizo hujumuisha yaliyomo,mbinu za mawasiliano, mwalimu na mwanafunzi (Kafu, 2010). Kwa hivyo mbinu za ufundishaji huhusisha njia mbalimbali za kufundishia wanafunzi (Otunga, Odeo na Barasa, 2011). Kutokana na haya mbinu za ufundishaji tofauti zinazotumiwa na mwalimu katika kufundisha wanafunzi zinapaswa kutoa maelewano bora kupitia mawasiliano kwa vile mawasiliano bora hupaswa kutoa matokeo yaliyokusudiwa. Ni bora mawasilano haya yatoe mwingiliano madhubuti wa maelewano baina ya mwalimu na mwanafunzi.

mbinu ya mafundisho iliyochaguliwa inapaswa kuwa nzuri katika kufanikisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kufundisha kupitia kusoma hakusaidii tu wanafunzi katika kupata ufahamu wa lugha bali huongeza utendaji wao katika masomo mengine yaliyo katika mtalaa wa shule. Kwa hivyo, mwalimu anapaswa kutoa fursa kwa wanafunzi kukuza stadi tofauti za kusoma ili kuweza kusoma ufahamu juujuu na kwa undani. Anapendekeza mafundisho ya kusoma yanapaswa kujumuishwa na mafundisho mengine ya lugha na sarufi. Hii inapaswa kufanywa kupitia mijadala au kazi ya kuandika kutoka kwa sehemu za maandishi ya fasihi. Kwa bahati mbaya wanafunzi wengi hawapendi kusoma riwaya za Kiswahili. Athari ni kwamba wengi wa wanafunzi hawa hawawezi kusoma wala kuandika kikamilifu wanapofikia kidato cha nne. Wengine husoma kifungu bila kuwa makini na kisha hujaribu kujibu maswali bila kurejelea ufahamu.

Stadi ya kuandika huhitaji mwanafunzi kufahamu lugha vizuri ndiposa aweze kuwasilisha mawazo yake kwa ufanisi mkubwa. Hali hii humfunza mwanafunzi kuandika vizuri na vilevile kuwaza kwa ubatini anapoandika. Hujenga pia ubunifu wa mwanafunzi na kujenga nidhamu yake ya kufanikiwa katika elimu. Tunafahamu kuwa uandishi ni taaluma ya maisha ambayo mwanafunzi huhitaji hata baada ya kufuzu shuleni. Gathumbi na Ssebbunga (2005) wanasema kuwa walimu wengi wanaofundisha fasihi na stadi ya kuandika wamelalamika kwa muda mrefu kuhusu mbinu za kitamaduni zinazotumika kufundishia dhana hizi darasani. Kwa hivyo, utafiti wa uchunguzi wa kina wa maendeleo ya uwezo bora wa uandishi umeamsha haja ya kutafiti kuhusu mbinu mpya za uandishi. Kwa kuzingatia majadiliano haya, mbinu za ufundishaji wa wahusika

darasani katika riwaya ya Kiswahili zinapaswa kufuata kanuni zinazo boresha nafasi rahisi ya kuelewa kwa mwanafunzi na kujenga maarifa ya kudumu katika maisha yake ya baadaye. Wamokhela (2012) aligundua kuwa wanafunzi wengi walikubaliana kuwa majadiliano ya vikundi yaliongeza maarifa ya kujifunza. Kwa hivyo, ni muhimu kwa mwalimu kuandaa vizuri somo ili kumpa mwanafunzi fursa ya kufurahia mchakato wa kufundisha na kujifunza.

Ahmad na Aziz (2009) walibaini kuwa baadhi ya mbinu zinazotumiwa na walimu kama kitovu cha ufundishaji ni za kale na hazifai kamwe. Mwalimu kuwa mshiriki mkuu kwa kazi ambazo wanafunzi wanafaa kushirikishwa ni jambo ambalo limepitwa na wakati, hivyo mbinu hii inafaa kufutiliwa mbali. Babusa (2010) anasema kuwa walimu wanafundisha tu stadi andishi na kusoma kwani ndizo stadi ambazo zinatahiniwa na kupuuza stadi zingine kama za kusikiliza na kuzungumza. Utafiti kuhusu mbinu za ufundishaji na matokeo ya wanafunzi uliofanywa na Tella, Indoshi na Othuon (2010) uligundua kuwa mbinu zinazozingatia mwalimu kama kitovu cha ufundishaji, zilisababisha wanafunzi kutofurahia masomo na pia zilinyima wanafunzi nafasi ya kujigundulia mambo wao wenyewe. Hii iliwafanya wanafunzi kukosa namna ila kubaki watazamaji tu wakati wa mchakato wa kufundisha na kujifunza. Kulingana na utafiti wao Ahmad na Aziz (2009)) walibaini kwamba katika mfumo wa elimu ya kale, madarasa ya jadi yalikuwa na mtazamo kuwa majukumu ya mwanafunzi darasani yalikuwa ni kutulia tuli na kujifunza yote yale waliofunzwa na walimu wao.

Murunga (2013) anasema kwamba mbinu ya kufundisha isiyofaa inapochaguliwa na kutumiwa na mwalimu katika kufundisha wahusika na ushairi katika Kiswahili, ufunzaji huathiriwa vibaya sana. Kwa hivyo mbinu anayotumia mwalimu kufundisha inaweza kumotisha au kukosa kumotisha mwanafunzi darasani. Aligundua kuwa walimu walitumia mbinu ya wao kutawala vipindi vya mashairi. Walikosa kutilia maanani maoni ya wanafunzi na kuwashirikisha katika vipindi. Walimu walikosa kufahamu kuwa ufunzaji wa mashairi ulipaswa kumshirikisha mwanafunzi. Alipendekeza kuwa katika ufunzaji wa mashairi mwanafunzi alipaswa kuhusishwa kikamilifu na kutawala vipindi hivyo. Alibaini kuwa mbinu bora za ufundishaji mashairi zilihusisha uigizaji, ufanani, mijadala, sanaa tuli na ukariri wa mashairi. Utafiti ulikuwa tofauti na huu kwa sababu uliangazia matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya.

Wasike (2011) alibaini kuwa ufanani na maigizo yanapotumika wakati wa kufundisha ushairi, uchunzaji, sauti na hisia za mwanafunzi huboreshwa katika mafunzo ya vipindi vya ushairi. Hali hii huchangia na kuondoa mtazamo hasi kuhusu kusoma na kufunzwa mashairi. Hali hii inapotumika vizuri wanafunzi huelewa vizuri dhamira ya mshairi, hisia, mtazamo wa kazi yake na historia ya utamaduni wake. Wamokhela (2012) anapendekeza kwamba matumizi bora ya majadiliano ya kikundi, huhitaji maandalizi ya kutosha kabla ya kutumiwa.Hii ni pamoja na kutilia maanani mambo yaliyotajwa awali kama kuzingatia wakati, rasilimali na ukubwa au udogo wa darasa. Kwa kuelewa uwezo na viwango vya wanafunzi,humwezesha mwalimu kupanga makudi ya wanafunzi ipasavyo.

Wasike (2011) anakubali kwamba wahusika wepo katika kila tamaduni na ushairi ni zana ambayo mwandishi hutumia kuelezea hisia zake za ndani ambazo wanafunzi wanahitaji kubaini ili kuelewa. Kwa hivyo, shughuli zinazomshirikisha mwanafunzi humsaidia kuibua hisia hizo na kumsaidia kuzielewa zaidi. Kwa upande mwingine mbinu ambapo mwalimu anatawala somo, wanafunzi hukosa kuelewa maana ya shairi linalowasilishwa na hivyo kusalia kuwa watazamaji tu. Mafundisho yenye ufanisi yanajumuisha kuwapa wanafunzi mafunzo ya kupata maarifa ya kusoma ili waweze kujifunza pekee yao, na hili hufanikiwa kupitia mazoezi endelevu. Mwalimu anayefundisha mashairi huanza kwa kutoa utangulizi wa maana ya ushairi kabla ya kuwaelekeza wanafunzi kuchambua vipengele vya ndani zaidi. Hii ndio sababu silabasi ya Kiswahili imepangwa kwa njia ya mipito ambapo mwalimu anatarajiwa kuifundisha hatua kwa hatua (Otunga na wengine, 2011).

Kang'ahi, Chisikwa, Omusonga na Osodo (2004) walifanya utafiti kuhusu ufundishaji wa mitindo na mafanikio ya wanafunzi katika lugha ya kiswahili katika shule za upili. Matokeo yao yalionyesha mbinu ya mhadhara ndio ilizingatiwa zaidi (43.20%), ikifuatiwa na ya walimu kuwauliza wanafunzi maswali (22.49%) kisha ya wanafunzi kujibu maswali yaliyoulizwa na walimu wao kwa asilimia (20.30%). Takwimu zinaonyesha kategoria ya 3 (mhadhara) ndiyo ilitumiwa sana. Hii inamaanisha kuwa vipindi vya lugha madarasani vinawasilishwa kwa matumizi ya mbinu za jadi ambapo wanafunzi wanasalia kuwa watazamaji huku walimu wakijiona wao ndio kitovu cha pekee cha kutoa maarifa. Wanafunzi hushiriki tu pale wanapopewa fursa finyu na walimu wao.

Suter na Busienei (2013), walichunguza vifaa na mbinu za kufundishia zilizotumiwa katika somo la fasihi simulizi ya Kiswahili kwenye shule za upili katika wilaya ya Marakwet, Kenya. Msukumo wa utafiti ulitokana na changamoto ambazo zingejiri kutokana ufundishaji wa fasihi simulizi, mada mpya ambayo ilikuwa imeanzishwa na KICD mnamo mwaka 2002. Kutokana na matokeo hayo, idadi kubwa ya walimu na wanafunzi walikubali kuwepo kwa vitabu vya kiada vya wanafunzi. Kwa kuongezea, wengi waliohojiwa walikiri  kuwa mbinu ya mjadala ilikuwa mojawapo ya njia zilizotumiwa sana kudumisha motisha ya wanafunzi darasani wakati wa somo la fasihi simulizi ya Kiswahili. Kulingana na matokeo ya mwisho ya utafiti, wasailiwa wengi, 13 (65.0%), ya walimu na 73 (45.6%), ya wanafunzi walitumia kazi ya makundi kama mbinu ya kufundisha katika darasa la fasihi simulizi ya Kiswahili. Hii inamaanisha walimu na wanafunzi waliona ni rahisi kutumia kazi ya makundi kama mbinu ya kufundishia kuliko mbinu  zingine zilizotumika kwa nadra sana darasani kama kuigiza, ufanani na mijadala.

Agonya, Koross na Murunga (2019) walichunguza ushawishi wa njia za kufundisha utendaji katika ushairi kwa wanafunzi wa shule ya upili, kwenye kaunti ndogo ya Lugari, Kenya. Matokeo kutoka kwa hojaji za walimu yalionyesha walimu wote 12 (100%) wa Kiswahili walitumia mbinu ya kuuliza maswali wakati wa kufundisha, 11 (91.7%) kati ya wahojiwa 12 walitumia njia ya mihadhara, 10 (83.3%) walitumia majadiliano, 7 ( 58.3%) walitumia kazi ya makundi, 6 (50%) walitumia mbinu ya kukariri, 2 (16.7%) walitumia uigizaji, hakuna (0%) waliotumia ufanani na pia (0%) kuigiza kwa kuiga.

Matokeo kutoka kwa ratiba ya uchunzaji wa vipindi vya masomo darasani yalionyesha kuwa kati ya vipindi 12 vilivyozingatiwa katika masomo. Kiwango cha juu 10 (83.3%), kilimilikiwa kwa kuuliza maswali, ikifuatiwa na 9 (75%), ambao walitumia mbinu ya mhadhara kufundisha mashairi.Ukariri ulichukua nafasi ya tatu, ambapo mwalimu 1 (8.3%) alitumia ukariri kama mbinu ya kufundisha mashairi. Hakuna (0%) aliyetumia majadiliano, kazi ya makundi, ufanani na kuigiza kwa kuiga. Utafiti huu unaafikiana na matokeo ya Murunga (2013) yaliojadili hapo awali.

Ufundishaji na ujifunzaji mzuri wa fasihi ya Kiswahili hujiri mbinu inayomhusisha mwanafunzi inapotumika. Japo mbinu hizi ni nadra sana kutumiwa katika madarasa ya lugha ya Kiswahili (Perry 2004). Ikiwa walimu wa lugha ya Kiswahili watakosa kuwa wabunifu kwa kubuni mbinu zinazowasaidia kujitayarisha vizuri kwa somo, wanafunzi hukumbwa na shida nyingi za kujifunza lugha hiyo. Walimu wengine wa lugha hawawezi kutumia mbinu fulani kwa sababu ari yao huwasukuma kuchagua mikakati inayowawezesha tu kutimiza malengo yao ya somo, bila kuzingatia madhumuni ya jumla ya kufundisha na kujifunza lugha.

Kwa kuangalia jinsi wasomi mbalimbali walipoelezea kuhusu mbinu mbalimbali za kufundisha wahusika. Inabainika kuwa hawatoi mbinu maalumu zinazofaa kutumiwa kufundisha wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Utafiti huu ulilenga matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundisha wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Kulingana na mapitio ya maandishi haya ni dhahiri kwamba walimu wanapendelea njia tofauti tofauti za kufundishia fasihi. Njia hizi ni pamoja na; mbinu ya kusoma na kueleza, mijadala ya

makundi, mihadhara, mashairi, maigizo na matumizi ya maswali na majibu. Hata hivyo, hakuna utafiti maalum ulioangazia njia maalum katika kufundisha wahusika kama sehemu maalum ya fasihi lakini wanapendekeza mbinu za jumla katika kufundishia fasihi. Tafiti chache zimechunguza mitindo ya ufundishaji inayotumiwa na walimu katika kufundisha wahusika katika fasihi. Kwa hivyo kunakosekana uchambuzi wa kina kwa kipengele cha wahusika katika kazi ya fasihi. Utafiti wa sasa ulilenga kujaza pengo hili kwa kutafiti njia madhubuti ya kufundishia kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili badala ya matumizi ya mbinu za jumla za kufundishia fasihi.

## 2.3 Kiwango cha Matumizi ya Mbinu ya Maigizo katika Kufundisha Kipengele cha Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili

Masinjila na Okombo (inavyotajwa na Nandwa, 1994) wanasema mwanafunzi anaweza akaigiza vizuri ikiwa amefunzwa kipera cha maigizo katika fasihi simulizi. Huwa vizuri talanta hii ikikuzwa katika madarasa ya chini, japo kuna wengine ambao huzaliwa na talanta au hukuzwa na mazingira wanamokulia. Galante na Thomson (2017) wanadhihirisha kuwa mchezo wa kuigiza unapotumiwa kufundishia lugha, wanafunzi huinga na kuweka katika ulimwengu wa fikra unaojenga ushirikiano, uzoefu, tajiriba, uwasilishaji, mipangilio na mtagusano mzuri baina yao. Kwa hivyo, maigizo hufungua fikra za mwanafunzi na wakati huo huo kuchochea na kutoa changamoto kwa wanafunzi kumakinika katika mawasiliano, sarufi na katika uwanja wa fasihi. Mchezo wa kuigiza huchangia wanafunzi kuelewa zaidi wanachosoma na yale wanayojifunza. Maelezo haya yalifafanuliwa zaidi kwamba maigizo huwa na athari chanya katika ukuaji wa mtazamo

wa wanafunzi na kuchangia ubora wa mawasiliano, viwango vya ushirikiano, makuzi ya akili, ustadi wa kijamii na mwingiliano mzuri na jamii (Dunn na Stinson, 2011).

Katika utafiti uliofanywa na Beena (2016) kuhusu nafasi ya maigizo katika kufaulu kwa wanafunzi. Ripoti ya majaribio ilionyesha kwamba wanafunzi waliofunzwa kwa kutumia maigizo walimakinika kwa kiwango kikubwa katika matokeo ya stadi ya kuzungumza, kusikiliza, kuandika na kusoma kuliko wale ambao hawakufundishwa kwa kutumia mbinu ya maigizo. Jaribio la T- test la kulinganisha lilionyesha alama zilizoimarika. Sehemu waliyokuwa na alama za wastani vilevile ziliimarika wakati wanafunzi walipofafanuliwa kuhusu jukumu la maigizo na masimulizi katika masomo. Utafiti ulionyesha kuwa maigizo huvutia na kuwamotisha wanafunzi wakati wa kusoma. Utafiti huu ulibaini kuwa mbinu ya kuigiza inaweza kuvutia wanafunzi wanaposoma na wakiwa katika vikundi hasa wanapopewa majukumu na maswali yaliyo na majibu. Wanafunzi wanapozungumza kuhusu mambo haya, wao huanza kujihusisha na makundi yanayowavutia. Hali hii huwahamasisha wanafunzi wavivu na hivyo, kuboresha matokeo yao. Hali hii hujenga mazingira ya mashindano ya kitaaluma ambapo hata wanafunzi wavivu huboresha mawasiliano na mazungumzo yao. Aina hii ya maigizo inayoambatana na maswali ya fasihi na lugha huwapatia wanafunzi fursa ya kuboresha ujuzi wao wa kujibu maswali ya mtihani ya KCSE.

Kwa kutumia mbinu za maigizo darasani, majukumu ya mwalimu hubadilika kuwa mwezeshaji badala ya mwenye mamlaka au chanzo cha maarifa (Sirengo, 2013). Wanafunzi wanasalia kuwa makini darasa na kushiriki zaidi badala ya mwalimu

kuongoza kila mara. Clark (2013) aligundua kwamba maigizo huchangia kujifunza kwa ukamilifu kwa kushirikisha akili, mwili, sauti na hisia kwa kufanikisha habari na maoni kwa wengine. Mchezo wa kuigiza katika elimu ni zana yenye nguvu ya kufundishia na kujifunzia yenye athari chanya juu ya utambuzi wa mwanafunzi, kijamii na ukuaji wa mwili.

Hertzberg (2009) anatambua kuwa shughuli za ufundishaji na ujifunzaji zinazohusisha mchezo wa kuigiza zinaweza kurudufiwa kwenye vikao vya mijadala ya vitabu ambavyo hufanyika wakati wa kusoma badala ya shughuli ya ziada inayolenga kukamilisha makala ya kitabu. Wakati mchezo wa kuigiza unatumiwa kwa njia hii, hukuza wanafunzi katika mazoea ya lugha na wakati huo huo kutoa majibu sahihi. Mchezo wa kuigiza husaidia wanafunzi kupata ujasiri na kujithamini wanapohitaji kutumia lugha kwa hiari au kwa jukumu la kushiriki katika maigizo (Chepkoech, 2012).

Kulingana na Albalawi (2015), mafunzo bora yanaweza kupatikana wakati mwanafunzi anajihusisha moja kwa moja na majukumu anayopashwa kutekeleza. Hali hii inamhamasisha kutumia lugha inayolenga kutatua majukumu tatanishi. Mchango wa wasomi ulitiliwa maanani katika utafiti huu kwa sababu ushiriki wa wanafunzi katika somo la fasihi ya Kiswahili ni kuwaandaa kukabiliana na hali halisi ya maisha katika mawasiliano. Kutokana na utumiaji wa maigizo, wanafunzi hujenga imani chanya ya kujiamini zaidi katika kutumia Kiswahili na kuleta ufasaha na uwezo wa mawasiliano bora (Sirengo, 2013). Maigizo huwapa wanafunzi uzoefu wa kuwasiliana katika mazingira yao na kufaulu katika hali halisi ya maisha. Hali hii inapaswa kuimarisha kwa

kuwapa ujasiri wa kukabiliana na ulimwengu wa nje ya darasa. Hata hivyo, hakuna utafiti wa ndani uliofanywa ili kuhakikisha hali hii na hivyo, hii itawezesha utafiti uliopendekezwa kuchunguza uhusiano kati ya mafanikio ya wanafunzi wa kundi dhabiti na kundi majaribio kulingana matokeo ya mjarabu wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

Tafiti hizi zinapendekeza matumizi ya maigizo katika kufundisha fasihi badala ya kutoa mwelekeo mahususi kuhusu namna mbinu ya maigizo inavyopaswa kutumiwa katika kufundisha wahusika katika fasihi. Hivyo, kuna maelezo finyu katika utumiaji wa mikakati ya maigizo katika kufundisha wahusika na hili hivyo linadhihirisha pengo la matumizi ya maigizo kwenye nyanja maalum ya ufundishaji wa fasihi. Utafiti huu utanuia kiziba pengo hili kwa kuanzisha mikakati maalum ya matumizi ya mbinu maigizo katika ujifunzaji na ufunzaji wa wahusika katika fasihi.

## 2.4 Athari ya Mbinu ya Maigizo kwa Uelewa wa Wanafunzi katika Ufundishaji wa Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili.

Taskin (2013) alichunguza athari ya kufunzia maigizo ya kimsingi katika kufaulu kwa wanafunzi wa sayansi wa gredi ya tano katika mada ya mwanga, sauti na maarifa ya kisayansi. Utafiti huu wa majaribio ya kadiri ulifanywa katika shule moja ya msingi nchini Uturuki kati mwaka ya 2009-2010. Wanafunzi 60 waliteuliwa kwa njia ya kinasibu na kupewa mtihani bora uliotungwa. Mtihani huu ulilenga mada ya sauti. Kikundi cha majaribio kilitahiniwa kwa mujibu wa njia ya maigizo. Kikundi dhabiti hakikuhusishwa moja kwa moja na mbinu ya maigizo. Vifaa vya kufundishia pamoja na vipindi vitano

vya masomo vilitengwa pamoja na kiongozi wa kusimamia maagizo ya msingi wa maigizo. Jaribio la sampuli ya kujitegemea lilibaini kulikuwa na tofauti kubwa kwa njia ya matumizi ya maigizo ya ubunifu, mafanikio ya sayansi na ujuzi wa mchakato wa kisayansi. Hata hivyo, utafiti huu ulifanywa katika somo lingine, kwa hivyo utafiti huu ulipendekezwa kujaza pengo hili kwa kubaini athari ya kuwahusisha wanafunzi kwa mbinu ya maigizo juu ya utendaji wao katika fasihi ya Kiswahili.

Mchezo wa kuigiza ni kifaa cha kukuza na kuboresha mawasiliano ya wanafunzi, fikra za ubunifu na maadili. Stephanie (2011) alionyesha kuwa uchanganuzi wa dhana kwa njia ya msisimko ni mzuri katika kuhamasisha wanafunzi. Matokeo ya utafiti yanaendana na maoni ya Prasad (2011) ambaye alisema kwamba kufundisha wahusika katika riwaya kwa kutumia uigaji wa sauti huwachochea wanafunzi kujifunza na kuwapatia mazingira ya masomo yenye uchangamfu.

Bashayer (2014) alifanya utafiti kutaka kubaini athari ya kufundisha lugha ya Kiingereza kwa kutumia mbinu ya maigizo katika kukuza ubunifu wa wanafunzi. Utafiti wake ulilenga madarasa ya kati katika shule ya wasichana ya Tabuk. Alitumia mbinu nasibu kuchagua wanafunzi 24 wa kundi dhabiti na 23 wa kundi jaribio. Wanafunzi wote walifanya mjarabu wa kwanza. Kundi jaribio lilifunzwa kwa kutumia mbinu ya maigizo katika somo la sura ya kumi. Kundi dhabiti lilifunzwa kwa kutumia mbinu za kawaida. Wanafunzi wote walifanya mjarabu uliolenga kutathimini ubunifu. Matokeo yalipochanganuliwa ilibainika kuwa kundi jaribio lilikuwa na matokeo yaliyoimarika

kuliko kundi dhabiti. Utafiti uliofanywa ulikuwa tofauti na huu kwani ulilenga matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

Katika kazi iliyofanywa na Beena (2016) juu ya athari za sanaa kwa watahiniwa, matokeo yalionyesha jukumu la nafasi ya uigajizi na usimulizi unaweza kusababisha aibu, usumbufu na utumiaji wa lugha legevu ama mbovu haswa miongoni mwa wanafunzi waoga. Walimu waliogopa kwamba wanaweza kupoteza udhibiti wa madarasa yao wakati mchezo wa kuigiza ukitumiwa katika kujifunzia lugha. Zaidi ya hayo, walimu waliohojiwa walieleza ya kwamba wakati wa kutumia mbinu ya maigizo kufundishia, umakini wa wanafunzi unaweza kuvurugika na mafunzo kutofanyika itakikanavyo. Vile vile ni vigumu kutabiri idadi ya muda na vipindi ambayo shughuli itachukua kutegemea maarifa ya wanafunzi na mada ya vipindi.

Hata hivyo, changamoto hizi zinaweza kusuluhishwa ikiwa itawaziwa vizuri na mipango itengwe kwa shughuli kuu ya mada darasani. Utafiti huu ulichunguza kuhusu athari ya matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya na kuboresha matokeo ya Kiswahili katika shule za upili.

Wanafunzi wasio na tajiriba ya kuigiza wahusika katika vitabu vya riwaya huwa ni vigumu kuwasawiri wahusika kwa njia inayofaa. Hali hii humsukuma mwalimu kutumia muda mwingi kuwafunza namna ya kuigiza kabla wao kushiriki vizuri kwenye kipindi. Suala hili wakati mwingine humchusha mwalimu ikiwa linachukuwa muda mrefu wanafunzi kulitekeleza kwa kiwango anachotaka (KICD, 2002). Moja ya malengo ya

kufundisha Kiswahili katika mtalaa wa 8-4-4 ni kuendeleza uwezo wa wanafunzi kujieleza bayana kimantiki, waziwazi na mawazo kwa mazungumzo na katika hali ya maandishi.

Kuna makundi ya kibinafsi yanayoandaa vikao vya kuigiza riwaya inayotahiniwa. Waigizaji wake hulenga kuigiza kwa ujumla bila kuzingatia sifa za wahusika pekee. Makundi haya ni kama *Jicho Four Productions*, *Fanaka -Arts*, *KCA University*, *Mabingwa Theatre* na mengine.

Uchunguzi umeonyesha mbinu ya maigizo inapotumiwa katika ufundishaji, hutoa athari chanya katika matokeo ya masomo. Hata hivyo utafiti huu ulirejelea masomo mengine kama ya sayansi badala ya fasihi hivyo kuacha pengo la kubaini ikiwa matokeo haya yanaweza kulingana mbinu ya maigizo inapotumika kufundisha fasihi. Utafiti huu utalenga kujaza pengo kwa kuchanganua tofauti ya matokeo ya mtihani kuhusu wahusika katika riwaya ya Kiswahili baina ya kundi jaribio na kundi dhabiti.

## 2.5 Mtazamo wa Walimu na Wanafunzi katika Utumizi wa Mbinu ya Maigizo katika Ufundishaji wa Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili

Utafiti unaonyesha kuwa mitazamo ya walimu kuhusu majukumu ya michezo ya kuigiza hutofautiana. Majukumu haya ni pamoja na; michezo ya kuigiza, kuigiza kwa kutoa hadithi na mchezo wa kuigiza wa kijamii, mijadala na mahojiano. Maigizo kwa ujumla hutoa fursa kwa wanafunzi kuchukua majukumu ya wengine na kwa hivyo kufahamu na kutilia maanani mchango na maoni ya wengine. Inatoa fursa ya uchunguzi wa hali na nafasi ya kufanyia mazoezi. Mwalimu yuko huru kupima na kutoa maoni yake kuhusu

mapungufu na wajibu wa hali, shida na majukumu ya maigizo darasani. Kwa mfano huenda yasiwe na manufaa kwa kundi kubwa la wanafunzi au yanatatiza mwingiliano wa mjadala wao. (Chepkoech, 2012).

Kisanda (2018) katika maelezo yake alielezea jinsi walimu wa Kiswahili wanavyotumia mbinu za maigizo katika shule za upili wanapofundisha sarufi. Matokeo ya utafiti wake yalifafanua kuwa mbinu za kuigiza zilitumika katika jukumu la kuigiza, michezo ya kuigiza na majadiliano. Ilibainika kuwa ukubalifu wa walimu kutumia maigizo ulikuwa wa kiwango cha chini mno. Walimu wengi waliripoti kwamba wanafunzi walikuwa tayari kuchukua majukumu waliyopewa wakati mbinu ya maigizo ilipotumiwa. Mapendekezo ya utafiti yalipendekeza walimu wa Kiswahili watumie mbinu za maigizo katika kufundisha sarufi. Walisema walimu walipaswa kupewa fursa ya kuongeza ujuzi, maarifa na ukakamavu. Walimu wengi walilemewa kung'amua kwa urahisi maneno tofauti yaliyotumika katika maigizo kama vile kuigiza kwa ubunifu, kuigiza, mchezo wa kuigiza usio rasmi, mchezo wa kuigiza darasani miongoni mwa mengine. Utafiti uliopendekezwa pia utachunguza kiwango cha matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

Kulingana na Pinter (2006) na Doff (2000), mojawapo wa michezo ya kuigiza iliyofana sana ni mchezo wa sanaa bubu. Kwa kushiriki mchezo wa kuigiza, wanafunzi huhisi wameburudika, wamefurahi, hufikiri na huwasiliana na wenzao. Hutoa maelezo bora kuhusu nafasi zao za uigizaji. Shughuli hii huzalisha wao kutoa sifa fiche za wahusika na hivyo kuchangua mafunzo ya sanaa ya lugha na mtindo wa fasihi. Amato (2007) alisema

kuwa njia madhubuti ya kukuza na kuimarisha dhana kadhaa za fasihi ya Kiswahili ni mwingiliano wa ndani baina ya waigizaji na mazingira yakishirikishwa na mawasiliano bora baina ya wahusika wanaoigiza. Beena na wengine (2015) walionyesha kuwa maonyesho ya michezo ya kuigiza husaidia wanafunzi kuimarika kimawazo. Huwapa pia wanafunzi ukakamavu wakuigiza mbele ya wenzao bila kutilia maanani lugha. Munther (2013) alielezea kuwa maonyesho ya michezo ya kuigiza yanahusu sanaa ya kufundisha kupitia mawasiliano tuli, maneno, vitendo na ishara.

Teresa (2007) anaelezea kuwa walimu wanazidiwa kwa urahisi na maneno anuwai yanayotumika katika maigizo kama vile maigizo ya ubunifu, mchezo wa kuigiza, maigizo yasiyokuwa rasmi, mchezo wa kuigiza darasani miongoni mwa mengine. Walimu wa lugha ya Kiswahili hutumia shughuli mbalimbali katika maigizo ili kuwashirikisha wanafunzi na kukuza wajibu wa kujifunza na kufunzwa kwa bidii darasani (Mgulu, 2002)

Lorna (2016) alichunguza athari ya uigizaji kwa matokeo ya mwanafunzi katika kujifunza lugha ya Kiingereza katika shule za upili za umma, kwenye Wilaya ya Igembe Kaskazini na Imenti Kusini, nchini Kenya. Utafiti huu ulibaini kuwa mbinu za maigizo kama ufanani, kuigiza kwa kuiga, michezo ya lugha na sanaa tuli zina ushawishi mkubwa katika kutoa matokeo bora ya mwanafunzi. Ilibainika mbinu ya uigizaji ilikuwa na umuhimu mkubwa katika ufundishaji wa lugha ya Kiingereza kuliko matumizi ya mbinu ya mhadhara.

Tafiti nyingi zimeonyesha walimu na wanafunzi wana mitazamo tofauti kuhusu matumizi ya mchezo wa kuigiza katika ufuzaji na ujifunzaji wa fasihi. Hata hivyo hakuna tafiti maalumu zilizoangazia mitazamo ya walimu kuhusu matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundisha wahusika katika riwaya ya Kiswahili, hivyo kuna maelezo finyu kuhusu matokeo haya. Utafiti huu ulilenga kuziba pengo kwa kutathmini mitazamo ya walimu na wanafunzi katika utumizi wa mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili.

## 2.6 Changamoto katika Matumizi ya Mbinu ya Maigizo katika Ufundishaji wa Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili

Masinjila na Okombo (inavyotajwa kwa Nandwa, 1994) wanatambua kuwa muigizaji lazima atilie maanani fani za lugha anapoigiza. Upuuzaji wa dhana hii huchusha hadhira na kuifanya kukosa kuwa makini na hivyo kutotaka kushiriki na kuelewa anachowasilisha fanani. Miima (2014) alitambua uhaba wa muda wa kufunza Kiswahili kuwa changamoto kubwa kwa somo. Aliongezea kuwa walimu waliegemea kutumia maelezo yaliyo vitabuni kuwa ndio matini mufidi ya kufunzia vipindi darasani.

Uigizaji huhusisha wahusika wanaokabiliwa na shida na hatimaye kujipata kwenye migogoro. Kama mbinu ya kufundisha wahusika katika riwaya, inajumuisha hali halisi ya maisha ambayo wanafunzi wanaweza kujihusisha wenyewe (Vodickova, 2009). Wanafunzi huelewa na kujua zaidi wanaposhiriki katika maigizo darasani (Wasike, 2011). Kwa hivyo, ni muhimu kwanza mwalimu kuchagua wahusika ambao wanahusiana na mahitaji ya mwanafunzi. Ni bora kufahamu kuna wahusika wengine katika riwaya

wanaotumia lugha isiyostahili kwa mwanafunzi. Ni bora kuchuja wahusika hawa kabla ya kuwapa wanafunzi kuigiza majukumu yao.

Kujifunza lugha nyingine inaweza ikatatiza kwa sababu ya tofauti katika muundo na mpangilio wa lugha hiyo (Asfaha na Kroon, 2011) na maelewano katika utumiaji wa lugha kwa kawaida ambayo inasababisha wanafunzi kuzoea na kuchanganya lugha. Clegg na Afitska (2011) wanaonyesha ya kwamba, ili kuwezesha mawasiliano kati ya walimu na wanafunzi, kunatokea mazoea ya ubunifu wa lugha mbili kwa sababu ya kukosekana kwa ufasaha katika lugha ya kawaida haswa katika madarasa ya Kiafrika ambayo yana lugha nyingi. Zhang (2009) anasisitiza kwamba wanafunzi hawana msamiati muhimu wa kudumisha mazungumzo. Hii inaweza kuwa matokeo ya ustadi duni wa mawasiliano na uwezo duni wa kimkakati. Ukosefu wa motisha ya kuongea lugha pia kwa kiasi kikubwa inachangia wanafunzi kutokuwa na uwezo wa kuendeleza mazungumzo kwa muda mrefu katika lugha inayolengwa.

Babusa (2010) anatambua moja ya changamoto zinazowakumba walimu wa Kiswahili ni mielekeo hasi ya wanafunzi wengi kuhusu lugha. Kwa hivyo sera za lugha katika shule zafaa kutilia maanani uwezo wa mwanafunzi kujieleza kikamilifu na kwa njia fasaha katika lugha. Katika utafiti wa Suter (2013) anagundua walimu walishughulikia fasihi ya Kiswahili kwa nafasi finyu na hii inaweza kuwa sababu sehemu hii inatahiniwa kwa jaribio lakini katika sehemu kubwa ni maswali ya kuchaguliwa na mwanafunzi.

Kutokana na matokeo kwenye ripoti za KNEC (2015-2020), ni wazi kuwa kuna shida katika matokeo ya fasihi ya Kiswahili. Matokeo ya watahiniwa katika somo la fisihi ya Kiswahili kwa muda mrefu yamekuwa duni yakilinganishwa na vipengele vingine vya somo la lugha. Kwa kuongezea utendaji wake umekuwa na pandashuka nyingi ukilinganishwa na vipengele vingine vya Kiswahili japo wanafunzi wengi hupendelea somo la fasihi kuliko uandishi wa Insha, Sarufi na matumizi ya lugha. Kwa hivyo ni dhihirisho tosha kuwa wanatarajiwa kufanya vizuri zaidi katika kitengo hiki kwenye mtihani ya kitaifa. Matokeo haya hafifu yameibua swali. Je, inaweza ikawa ni matumizi ya mbinu zisizofaa za kufundisha kipengele cha fasihi ya kiswahili?. Mukwa (2002) anakiri kuwa kufanikiwa kwa malengo kamili ya kufundisha masomo mbalimbali, mbinu inayotumiwa lazima ilenge kumwelekeza mwanafunzi kujenga maarifa na uzoefu, kufikiria kwa kina na kushiriki katika utendaji hai. Anaendeleza kusema kuna haja ya kuchunguza jukumu la mchezo wa kuigiza katika kutimiza madhumuni ya fasihi ya Kiswahili katika mtalaa wa shule ya upili. Tafiti chache zimefanywa kubaini wajibu wa maigizo katika ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo, tafiti zilizofanywa zilichunguza matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji mashairi, uandishi, usomaji na ufahamu.

El-Helou (2010) alitafiti kuhusu changamoto zinazowakabili walimu wa lugha katika kufundisha fasihi (ushairi, hadithi fupi na maigizo) kwa wadaraji 12 wa Kipalesitina. aligundua kwamba hakukuwa na tofauti za kitakwimu katika jinsia ya walimu kuhusiana na kufundisha. Wengi wa walimu waligundua matatizo kadhaa yaliyowakabili katika ufundishaji wa mchezo wa kuigiza: (1) hakukuwa na faida ya kusoma mchezo wa kuigiza

kwa sababu lugha yake haikuwa ya kisasa, (2) mchezo wa kuigiza hukuwa na maana kwa sababu ulijaa utata ulioufanya uwe mgumu kwa wanafunzi kuelewa (3) yaliyomo katika maigizo na lugha hayakuzingatia umri wa wanafunzi na mahitaji yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia muktadha wa utafiti wa sasa, mtafiti alitafuta njia nyingine ya kupata namna bora na mahitaji ya utafiti katika matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundisha wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule ya upili.

Kwa mujibu wa tafiti za awali, changamoto nyingi zimetambuliwa kuhusu mbinu ya maigizo inapotumiwa katika kufundisha kipengele cha wahusika katika fasihi. Hata hivyo hakuna utafiti ambao umefanywa kubaini ikiwa kuna usawa wa matokeo katika mazingira yaliyo sawa kama kaunti ya Nairobi. Utafiti huu ulilenga kujaza pengo hili kwa kutambua ikiwa kuna changamoto katika matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi.

Kwa ujumla utafiti huu ulichanganua tafiti za wasomi wengine na mbinu zilizopo za maigizo za kufunzia Kiswahili. Mbinu hizi zilihitaji maandalizi ya walimu kama mbinu za maigizo katika vipindi vyao, athari za utumiaji wa maigizo kwenye matokeo ya wanafunzi na changamoto katika utumiaji wa maigizo. Masomo haya yalikuwa muhimu sana kwa sababu kila uwanja wa utafiti ulikuwa na matokeo tofauti.

Sababu za matokeo tofauti ni kwamba kila mtafiti alikuwa katika mazingira tofauti. La muhimu ni kuwa, wasomi wote wanaafiki kwamba kuna faida kubwa katika matumizi ya mbinu za kuigiza katika ufundishaji na kujifunza lugha. Hata hivyo, hakiki ya kazi hizi

za fasihi na lugha iligundua kuwa kuna pengo katika utafiti huo wa matumizi ya mbinu ya maigizo na walimu wa shule za upili nchini. Utafiti uliofanywa nchini Kenya unaonekana kuegemea lugha nyinginezo (Sirengo, 2013; Mbithe, 2014; Oseno, 2015) na yanayopatikana katika Kiswahili yanayozingatia nyanja zingine za utumiaji wa malengo ya mtalaa (Luvisia, 2003; Mbito, 2013).

Aidha, tafiti hizi zinahitilafiana kwani zimekosa kuthibitisha mitazamo ya walimu moja kwa moja namna inavyoathiri ufundishaji wa riwaya. Hata kama tafiti hizi zimebaini mitazamo ya walimu kuhusu mbinu zinazotumiwa kufundisha riwaya katika shule za upili, tafiti hizi kwa upande mwingine zimetoa tu picha ya uhusiano kati ya mitindo, mafundisho na mafanikio ya kitaaluma. Hata hivyo, mengi hayawezi kujumuishwa katika tafiti hizi. Kwa mfano, kutothibitishwa kwa manufaa ya ufundishaji wa riwaya kwa kurejelea tu ujuzi wa kusoma miongoni mwa wanafunzi likiwa ni jambo kuu. Katika kazi za awali na makala yaliyopo, kulikuwa na sababu ya utafiti huu kufanywa ili kubaini jinsi walimu wanavyotumia mbinu za maigizo katika kufundisha wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

Kwa kutazama matokeo haya ni dhahiri kuwa kuna haja ya kuchunguza kiini cha matokeo duni. Kumekuwa na tofauti ya maoni kati ya walimu na wanafunzi kuhusu ni mbinu zipi zinafaa kufundisha wahusika katika riwaya. Hali hii inaashiria ya kuwa kuna haja ya ufumbuzi wa haraka unaolenga kubaini mbinu zinazofaa kufikia mahitaji na kufaulu kwa mwanafunzi katika somo la fasihi. Kutokana na masimulizi haya, ni dhahiri kwamba wasomi tofauti walibaini changamoto tofauti katika mazingira tofauti huku wengine

wakionyesha changamoto zinazofanana kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, hakuna utafiti uliyobaini ikiwa kuna changamoto zilizofanana katika shule zote za upili mbinu ya maigizo ilipotumiwa, Mbinu ambayo utafiti huu unanuia kushughulikia katika shule za upili.

### 2.7 Pengo la Utafiti

Gathumbi na Ssebbunga (2005) walitafiti kuhusu kanuni na mbinu katika ufundishaji wa lugha. Matokeo yao yalibaini kuwa nakala za wakufunzi wa walimu na walimu wanaohudhuria kozi za kujipiga msasa, zilitawaliwa na mbinu za kitamaduni katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Ni bayana kuwa utafiti haukushughulikia hasa suala la wahusika na namna mada hii inavyofundishwa katika riwaya ya Kiswahili. Pia Murunga (2013) alitafiti kuhusu ushawishi wa mchakato wa ufundishaji na kufahamu stadi za kusikiliza katika lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Matokeo ya utafiti yalibainimbinu ya kufundisha isiyofaa inapochaguliwa na kutumiwa na mwalimu katika kufundisha wahusika na ushairi katika Kiswahili hutoa matokeo yasiyoridhisha. Licha ya utafiti kushughulikia swala la wahusika, haukuelezea matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa somo. Utafiti huu unanuia kujaza pengo hili. Wamokhela (2012) naye alitafiti kuhusu wajibu wa mbinu za majadiliano ya makundi katika kufundisha fasihi ya Kiswahili. Katika matokeo, aligundua kuwa mbinu ya majadiliano ya vikundi iliongeza maarifa ya kujifunza. Utafiti huo ni tofauti na wa sasa kwa sababu mtafiti hakushughulikia athari ya uigizaji kwa mafanikio ya wanafunzi katika uchambuzi wa wahusika katika fasihi ya Kiswahili. Taskin (2013), alifanya utafiti kuhusu athari ya kufunzia maigizo ya kimsingi katika kufaulu kwa wanafunzi wa somo la sayansi.

Matokeo yalionyesha kulikuwa na tofauti kubwa katika matumizi ya maigizo ya ubunifu, mafanikio na ujuzi wa mchakato kwa wanafunzi katika somo la Sayansi. Utafiti huo ulifanywa katika somo lingine, kwa hivyo utafiti huu ulipendekezwa kujaza pengo hili kwa kubaini athari ya kuwahusisha wanafunzi katika matumizi ya mbinu ya maigizo ili kutoa matokeo bora katika fasihi ya Kiswahili.

Wasike (2011) alifanya utafiti kuhusu mbinu za kufundisha mashairi kwa ufahamu na uelewa wa wanafunzi, katika shule za upili. Matokeo yalionyesha kuwa wahusika wapo katika kila tamaduni na ushairi ni zana ambayo mwandishi hutumia kuelezea hisia zake za ndani ambazo wanafunzi wanahitaji kuzichambua vizuri ili kuelewa ushairi. Hata hivyo utafiti huu ulilenga kipengele cha mashairi na haukuzingatia suala la mbinu ya maigizo katika kufundishia wahusika katika riwaya ya Kiswahili ndio sababu utafiti huu ulilenga kuziba pengo hili.

Suter na Busienei (2013) walitafiti kuhusu vifaa na mbinu za kufundishia fasihi simulizi ya Kiswahili kwenye wilaya ya Marakwet, Kenya. Katika matokeo ya utafititi waligundua mbinu ya mjadala ilikuwa mojawapo ya mbinu zilizotumiwa sana kukuza motisha ya wanafunzi darasani wakati wa somo la fasihi simulizi ya Kiswahili. Utafiti ulihusisha wanafunzi wengi katika mazingira tofauti na eneo la utafiti wa sasa. Utafiti huu unashughulikia moja kwa moja matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili kwenye, kaunti ya Nairobi.

Chepkoech (2012). Alifanya utafiti kubaini mikakati ya ufundishaji iliyotumiwa na walimu wa lugha ya Kiingereza. Matokeo yalibaini kuwa maigizo husaidia wanafunzi kupata ujasiri na kujithamini wanapohitaji kutumia lugha kwa hiari au kwa jukumu la kushiriki katika maigizo darasani. Mtafiti anaweka mkazo katika mikakati ya kufundishia kwa ujumla somo la Kiingereza. Utafiti wa sasa unarejelea mbinu moja ya matumizi ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili kwa shule za upili. Utafiti wa Kisanda (2018), ulilenga kubaini namna walimu wa Kiswahili wanavyotumia mbinu za maigizo katika shule za upili kufundisha sarufi kwenye kaunti ndogo ya Kimilili, Kaunti ya Bungoma, Kenya. Matokeo ya utafiti huu yaligundua walimu wengi hawakutumia mbinu ya maigizo kama mbinu ya kufundishia sarufi shuleni. Utafiti wa sasa utarejelea matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

# SURA YA TATU

# MUUNDO NA MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii ilirejelea muundo wa utafiti, eneo la utafiti, vigeu vya utafiti, wasailiwa lengwa, mchakato wa kuteua sampuli, mbinu na vifaa vya utafiti, majaribio ya vifaa vya utafiti, utaratibu wa ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na maadili katika utafiti.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa kwa kutumia mbinu ya utafiti ya Muundo Majaribio, ambayo ni mojawapo ya mbinu ya miundo kimajaribio. Katika muundo huu mtafiti aliwatia watafitiwa katika makundi mawili makuu ya kundi jaribio na kundi dhabiti. Watafitiwa katika makundi yote mawili walifanya mtihani wa kwanza. Kundi jaribio lilifunzwa kwa matumizi ya mbinu ya maigizo kufundisha wahusika katika riwaya ya Kiswahili nalo kundi dhabiti likafunzwa kwa kutumia mbinu za kawaida kufundisha wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Watafitiwa wote walitiwa katika mazingira maalum kwa takriban mwezi mmoja kabla ya kufanyiwa mtihani wa pili. Matokeo ya makundi mawili yalichanganuliwa ili kubaini athari ya matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika. Kulingana na Kothari (2004), njia za majaribio ni nzuri katika kuanzisha uhusiano kati ya vigeu huru na vigeu tegemezi. Mbinu ya Muundo Majaribio ilisaidia kupata matokeo ya maswali ya utafiti kuhusu matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika, katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi, Kenya.

### 3.2.1 Vigeu vya Utafiti

Vigeu vya utafiti vilihusisha mwingiliano wa vigeu vitatu. Vigeu huru vilikuwa ni; mbinu zilizotumika kufundisha kipengele cha wahusika, mbinu za maigizo, mitazamo ya wanafunzi na walimu kuhusu mbinu ya maigizo. Katika vigeu tegemezi kulikuwa na utendaji bora katika mtihani wa fasihi. Hata hivyo, uhusiano baina ya matumizi ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili ulikuwa na vigeu viingilizi kadha kama idadi ya vipindi vya fasihi, mazingira ya wanamofundishiwa, vitabu vya riwaya, motisha na uraibu wa mwanafunzi.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti ulifanywa katika kaunti ya Nairobi kwa sababu ya matokeo duni yaliyorekodiwa katika somo la Kiswahili kwenye mtihani wa (KCSE) kuanzia mwaka wa 2015 hadi 2019 (KNEC, 2019). Matokeo yalionyesha kuwa ya kiwango cha chini ya asilimia hamsini katika kategoria ya alama ya wastani. Kipengele cha fasihi ambacho maswali mengi kuhusu wahusika hulenga, kilidhihirika kutofanywa vyema. Kaunti hii ilikuwa na uwezo zaidi wa kutoa picha ya hali halisi ya matokeo ilivyo nchini Kenya kuhusu matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya. Hii ni kwa sababu ndilo jiji kuu la Kenya lililo na shule nyingi baadhi yazo zikitoa matokeo ya juu zaidi katika mtihani wa taifa wa kidato cha nne.

## 3.4 Idadi Iliolengwa

Mugenda na Mugenda (2013) walifafanua watafitiwa kama kundi zima la matukio au watu binafsi wenye tabia zinazoweza kufananishwa. Idadi lengwa ya shule 4 zilizorejelewa katika utafiti huu ilitolewa katika orodha ya shule 101 za upili za serikali

katika iliyoko katika ofisi kuu za elimu jijini Nairobi. Utafiti ulilenga walimu 8 wanaofundisha Kiswahili na wanafunzi 240 wa kidato cha tatu kwa sababu walikuwa wakichambua riwaya ya Chozi la Heri (Assumpta, 2021). Wanafunzi wa kidato cha nne hawakuhusishwa kwa sababu walikuwa wanajiandaa kwa mtihani wa kitaifa, hivyo hawangepata muda wa kutosha.

### 3.5 Sampuli Mahususi

Sampuli ni kiwango kidogo kilichoteuliwa cha wasailiwa wanaotafitiwa ili kubaini sifa sawa katika idadi kubwa ya watu kwa ajili ya kupata matokeo yanayoweza kuaminika. Kauli yoyote inayotolewa kuhusu sampuli yaweza kuwa sawia na ile ya idadi lengwa kwa ujumla (Mugenda na Mugenda, 2009). Katika utafiti huu, mbinu ya utabakishaji ilitumiwa kuchagua shule ili kuhusisha shule za makundi yote. Shule nne (4) zilichaguliwa kutoka katika kategoria ya kitaifa, kikanda, kaunti na kaunti ndogo. Baada ya kuweka shule katika kategoria 4 kwa kutumia mbinu ya utabakishaji. Mbinu ya kinasibu ilitumika kuchagua shule moja moja kutoka katika kila kiwango. Walimu wawili (2) wanaofunza Kiswahili waliteuliwa kwa njia ya kimakusudi kutoka kwa kila shule.Walimu walioteuliwa ndio waliyoshirikishwa katika ufundishaji wa makundi mawili ya wanafunzi yaliyohusishwa katika utafiti. Mbinu  ya sampuli nasibu ilitumika kuchagua wanafunzi thelathini (30) kutoka katika kila shule. Kwa ujumla utafiti huu ulikuwa na sampuli ya watafitiwa mia mbili na arubaini na nane (248). Guthrie (2010) anasema kuwa hata sampuli ikiwa ndogo, huzalisha matokeo ya kutegemewa ikiwa itateuliwa kwa makini na data kuchanganuliwa vyema. Mbinu ya nasibu ilitumika kuwateua watafitiwa wa kidato cha tatu. Mbinu hii ilitumika ili kumpa kila mlengwa

nafasi ya kushiriki katika utafiti. Aidha mbinu ya kimaksudi ilitumika kuwateua walimu wanaofunza Kiswahili katika madarasa hayo.

**Jedwali la 3.1: Sampuli ya Utafiti**

| Shule/Wasailiwa | Jumla | Jumla ya Sampuli |
|---|---|---|
| **Shule** | 101 | **4** |
| **Wanafunzi** | 3450 | **240** |
| **Walimu wa Kiswahili** | 584 | **8** |

**Jedwali la 3.2: Sampuli ya Kiwango cha Shule**

| Kiwango | Shule | Walimu | Wanafunzi | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Taifa** | 1 | 2 | 60 | 62 |
| **Kikanda** | 1 | 2 | 60 | 62 |
| **Kaunti** | 1 | 2 | 60 | 62 |
| **Kaunti ndogo** | 1 | 2 | 60 | 62 |
| **Jumla** | **4** | **8** | **240** | **248** |

### 3.6 Vifaa vya Kukusanya Data

Vifaa vya utafiti vilivyotumiwa kukusanya data ni: Mitihani, hojaji ya walimu, uchunzaji darasani na mahojiano. Matumizi ya vifaa hivi kwa pamoja yalimarisha uthabiti wa data.

#### 3.6.1 Mitihani kuhusu Wahusika katika Riwaya

Mtafiti alitumia riwaya ya Chozi la Heri (Assumpta, 2021) kwa sababu ndio riwaya iliyochambuliwa na kutahiniwa wanafunzi wa kidato cha tatu. Riwaya hii iliidhinishwa na Taasisi ya Kukuza Mitalaa Nchini Kenya (KICD). Maswali yaliyolenga wahusika yalitungwa kwa azma ya utafiti kwa sababu walikuwa kipengele mojawapo mahususi cha

utafiti. Utahini huu ulifuata maagizo yaliyowekwa na Baraza la Mtihani Nchini Kenya (KNEC) katika utahini wa mitihani ya fasihi katika shule za upili nchini.

### 3.6.2 Mahojiano kwa Makundi lengwa ya Mijadala ya Wanafunzi

Mbinu ya mahojiano ilitumika kuwahoji wanafunzi katika makundi lengwa ya mijadala. Maswali wazi ndio yaliyotumika kwa wanafunzi walioshiriki kwenye vikundi. Maswali wazi yalitumika ili kupata mtazamo wao wa kina wa wanafunzi kuhusu matumizi ya maigizo katika kufundishia wahusika katika riwaya ya Kiswahili. (Litosseliti, 2004). Matumizi ya makundi lengwa ya mijadala ya wanafunzi humsaidia mtafiti kuelewa vizuri namna  wanafunzi wanavyotambua na kushiriki katika shughuli za  maigizo kutegemea na tajiriba na ufahamu wao. Kwa ujumla kulikuwa na manufaa makubwa katika matumizi ya kifaa hiki kwa sababu kilitoa fursa ya kukusanya data kutoka kwa makundi lengwa yaliyoshiriki katika  mijadala iliyolenga mada ya utafiti.

### 3.6.3 Hojaji ya Walimu

Cohen, Manion na Morrison (2011), walifafanua hojaji kama kifaa cha ukusanyaji data chenye maswali yaliyochapishwa kuhusu hoja muhimu ambayo mtafiti angependa kupata maoni au majibu kutoka kwa wasailiwa. Hojaji za maswali funge na maswali wazi zilizosambazwa kwa walimu wa Kiswahili na wanafunzi wa kidato cha tatu. Wanafunzi waliteuliwa katika shule za taifa, kikanda, kaunti na kaunti ndogo. Hojaji zilizosambazwa kwa walimu na wanafunzi wa kidato cha tatu zilikuwa na maswali ya aina mbili. Maswali funge yalilenga kumwezesha mtafiti kupata ujumbe usiyo na maelezo ya ndani.Kwa upande mwingine, maswali huru yalimsaidia mtafiti kupata data yenye maelezo ya kina

kuhusu madhumni ya utafiti kama vile mbinu zinazotumiwa kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya, kiwango cha matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya, athari ya mbinu ya maigizo kwa uelewa wa wanafunzi katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili, mtazamo wa walimu na wanafunzi katika utumizi wa mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili na changamoto katika matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili, katika shule za upili.

### 3.6.4 Mwongozo wa Mahojiano ya Walimu

Katika utafiti huu, mwongozo wa mahojiano ya walimu ulitoa nafasi ya mtafiti kukutana ana kwa ana na walimu kwa kubaini na kukusanya data kuhusu mitazamo ya washiriki, changamoto na mipango ya kukabili pengo la matumizi ya mbinu ya maigizo. Mwongozo wa mahojiano ya walimu ulikuwa na umuhimu mkubwa kwa sababu ulihusishwa kupata habari ya kina zaidi kutoka kwa wasailiwa kuhusu matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika kuliko ilivyokuwa kupitia vifaa vingine vya ukusanyaji wa data. Mahojiano yanaweza kutoa mazingira tulivu wakati wa ukusanyaji data ambapo wasailiwa huhisi kuwa huru zaidi na mtafiti kuliko wanapohusika katika kujaza hojaji (Cohen, Manion na Morrison, 2011).

### 3.6.5 Uchunzaji Darasani

Kwa mujibu wa MacMillan na Schumacher (2006) data inayokusanywa kwa uchunzaji huwa halisi na ya kutegemewa. Mtafiti alitembelea shule zote 4 zilizoteuliwa na kuhudhuria vipindi vya fasihi ili kuchanganua matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya. Uchunzaji ni mbinu mojawapo bora zaidi ya

kuchunguza na kubaini uhusiano kati ya mwalimu na wanafunzi wakati kipindi cha somo. Uchunzaji hurejelewa kama ndiyo njia ya pekee isiyo na ubaguzi katika kukadiria utendaji wa mwalimu na hulka za wanafunzi darasani. Mbinu hii ya ukusanyaji data ilitumika kuchunguza uhusiano wa mwalimu na wanafunzi darasani wakati wa somo la uchambuzi wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Mtafiti alidokeza machache kuhusu vigezo mbalimbali na mambo aliyokuwa akitafiti wakati wa kipindi cha somo la riwaya na baadaye kuchanganua data iliyokusanywa kwa mujibu wa swala la utafiti.

Shughuli ya uchunzaji ilitekelezwa kwa kuzingatia idadi ya vipindi vya somo la riwaya ambavyo walimu walifundisha darasani, changamoto zilizoibuka katika utumizi wa mbinu ya maigizo wanafunzi waliposhiriki darasani, mbinu zilizotumiwa kufundishia kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili na kubaini ikiwa wanafunzi walielewa na kuweza kutumia mbinu ya maigizo.

### 3.7 Majaribio ya Vifaa vya Utafiti

Kabla ya mtafiti kufanya shughuli kamili ya kukusanya data katika shule zilizoteuliwa. Alivifanyia vifaa vya utafiti majaribio mara mbili katika shule moja ambayo haikuhusishwa katika utafiti kamili. Mbinu ya kinasibu ndiyo ilitumiwa kuteua shule iliyofanyiwa majaribio ya vifaa vya utafiti. Shughuli hii ilitekelezwa majuma matatu kabla ya kuanza kwa utafiti kamili. Haya yalifanywa kwa mujibu wa kuimarisha uaminifu na uthabiti wa vifaa vya utafiti, kusahihisha makosa ambayo yalijitokeza kwenye vifaa hivyo na kujenga uzoevu wa kutumia nyenzo katika kukusanya data. Uimarishaji wa

tajiriba katika kitengo hiki kulirahisisha ukusanyaji wa data iliyokusanywa katika utafiti kamili.

### 3.8 Uthabiti na Uaminifu wa Vifaa vya Utafiti

Uthabiti na uaminifu wa vifaa vya utafiti umejadiliwa katika sehemu zifuatazo:

#### 3.8.1 Uthabiti wa Vifaa vya Utafiti

Orodho (2012) anaelezea uaminifu kama kipimo cha kiwango ambacho vifaa vya utafiti vitatoa matokeo yanayooana baada ya majaribio radidi. Ili kuboresha uthabiti wa vifaa vilivyotumika katika ukusanyaji wa data ya utafiti huu, nyenzo za utafiti ziliwasilishwa kwa wataalamu kutoka Idara ya Mawasiliano ya Elimu na Teknolojia ya Chuo Kikuu cha Kenyatta ili kuchunguzwa na kutahiniwa. Maoni na mapendekezo yao yalitiliwa maanani na kuhusishwa ili kuboresha ufanisi wa vyombo hivi vya utafiti. Hojaji za majaribio zilitolewa mara mbili kwa wasailiwa baada ya majuma mawili ili kuwezesha uaminifu kukadiriwa

#### 3.8.2 Uaminifu wa Vifaa vya Utafiti

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006) uaminifu wa mbinu ya utafiti inaashiria kipimo cha jinsi chombo cha utafiti kinaweza kuleta matokeo thabiti na imara kila wakati kinapofanyiwa majaribio. Utumainifu wa nyenzo ni kiwango ambacho vifaa vya utafiti vinaweza kutoa matokeo yanayofanana vinapofanyiwa majaribio radidi (Orodho, 2009). Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (2013) utumainifu ni hali ambayo vifaa vya utafiti vina uwezo wa kutoa matokeo yanayotegemewa kila mara vinapotumiwa kuamua uaminifu wa mbinu ya utafiti wa majaribio.

Utafiti wa majaribio ulifanyiwa walimu na wanafunzi wa shule moja, katika kaunti ya Nairobi. Uaminifu wa vifaa uliamuliwa kwa kutumia fomula ya alpha ya cronbach kwa ajili ya kubaini msimamo wa ndani wa chombo hiki cha utafiti. Borg na Gall (1989) walibaini ya kuwa wakati mtafiti anapopata swali katika chombo cha utafiti lililojibiwa kwa mitazamo tofauti, ni vyema kutumia fomula ya alpha ya cronbach kutathimini chombo kile. Ikiwa matokeo ya utathimini huo ni 0.7 au yamepita mgao huo wa uaminifu basi maadili haya yatachukuliwa kuwa ya hali ya juu kutoa uamuzi ya kwamba chombo kile kinaaminika kufanya utafiti (Orodho, 2012).

### 3.9 Utaratibu wa Ukusanyaji Data

Kabla ya kwenda nyanjani kafanya utafiti, mtafiti aliomba waraka wa kumtambulisha kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta. Barua hii ilimwezesha kupewa kibali cha utafiti kutoka kwa Kamati ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI). Baadaye aliomba idhini kutoka kwa wasimamizi wa shule zilizohusishwa katika utafiti. Kabla ya kuwasilisha hojaji, mtafiti alitenga muda wa kuwapa wasailiwa maagizo na kuwahakikishia kuwa maoni yao yatatumika kwa utafiti pekee wala hayatafichuliwa kwa watu wengine nje ya utafiti. Mtafiti alikusanya hojaji zilizojazwa kabla ya kutekeleza mahojiano na uchunzaji darasani. Baada ya mtafiti kapata ratiba ya vipindi vya riwaya, aliwataarifu walimu wanaofundisha vidato vya tatu walioteuliwa siku na saa ya kuhudhuria vipindi kwa ajili ya shughuli za kufanya utafiti.

Uchunzaji darasani ulifanywa kwa awamu nne; mara ya kwanza ilikuwa kufahamiana na watafitiwa, awamu ya pili, tatu na nne ikawa ya kufanya utafiti wa kukusanya data kwa dakika 40 zilizotengewa kipindi cha somo la riwaya. Data ya mjarabu ilikusanywa kwa kuwapa wanafunzi wa makundi yote mawili mjarabu. Mjarabu wa kwanza ulifanywa kabla ya kuanza utafiti kwa kutumia mbinu ya maigizo katika kufundisha wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Mjarabu wa mwisho ulifanywa baada ya mwezi mmoja. Mijaribu yote miwili ilisahihishwa na alama kurekodiwa. Muda wa mahojiano ulitengwa ambapo wanafunzi walihojiwa wakiwa katika vikundi darasani na walimu wakiwa pekee yao. Utaratibu huu ulifanywa kwa kujikita katika madhumuni ya utafiti yaliyohusu matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

### 3.10 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Majibu ya wasailiwa yalipangwa na kuwasilishwa kwa njia ya majedwali, pia chati, maelezo na grafu. Vitengo vya majibu chanya na hasi vilitenganishwa na kisha kulinganishwa kutegemea asilimia. Maelezo yaliyoona yalijumuishwa pamoja na kuwasilishwa kwa kutumia asilimia pia. Uchanganuzi maelezo ulitumika kusimulia baadhi ya data zilizokusanywa kupitia kwa njia ya mahojiano, uchunzaji na hojaji. Habari zilizopatikana zilikuwa na umuhimu mkubwa kwa utafiti.

Data ya tarakimu ilikuwa alama ambazo wanafunzi walituzwa kwa kufanya mijarabu miwili na majibu ya hojaji. Mbinu ya T-test ilitumiwa kubaini athari ya uhusiano wa matokeo ya kundi jaribio na kundi dhabiti. Data iliyokusanywa iliwekwa katika makundi,

ikachujwa na kuchanganuliwa kulingana na madhumuni ya utafiti. Data iliyokusanywa kwa kutumia hojaji, mahojiano na uchunzaji darasani na kuchanganuliwa kwa kutumia asilimia, mirudio na maelezo.

Kwa upande mwingine, tarakimu elezi ya asilimia, majedwali na grafu zilitumika kuchanganua data. Data hiyo iliandaliwa na kuwasilishwa kupitia michoro, mgao wa kiasilimia huku zikiambatana na majedwali na takwimu za data kueleza matokeo. Mtafiti alitekeleza uchanganuzi huu wa data akiazimia kuonyesha ukamilifu, ukubalifu na usahihi wa data yake ili kupata suluhu kamili ya suala la utafiti na mwishowe kutoa mapendekezo. Data ya kitakwimu iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa mtindo wa kisayansi wa SPSS. Suala hili lilimwezesha mtafiti kukadiria iwapo madhumuni ya utafiti yaliafikiwa kwa namna bora.

### 3.10.1 Mbinu Zilizotumiwa katika Ukusanyaji, Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Mbinu hizi zilifafanuliwa kwa kurejelea madhumuni yafuatayo ya utafiti.

a) Mbinu zinazotumiwa kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Kitovu cha data kilihusisha walimu na wanafunzi. Hojaji na mwongozo wa uchunzaji ndizo zilitumiwa kukusanya data kutoka kwa wasailiwa. Uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti ulifanywa kwa kurejelea mirudio, asilimia, majedwali, maelezo na baa grafu.

b) Kiwango kipi mbinu ya maigizo ilitumiwa kufundisha kipengele cha wahusika

Walimu na wanafunzi ndio walikuwa kitovu cha data. Vifaa vilivyotumiwa kukusanya data vilikuwa ni hojaji na mwongozo wa uchunzaji darasani huku mirudio, asilimia, majedwali, maelezo na baa grafu zikitumiwa kuchanganua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti.

c) Athari ya mbinu ya maigizo kwa uelewa wa wanafunzi katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Katika madhumini haya kitovu cha data kilikuwa ni wanafunzi na mijarabu miwili. Mbinu ya T-test ndio ilitumiwakuchanganua data huku majedwali na maelezo yakirejelewa katika uwasilishaji wa matokeo.

d) Mitazamo ya a) walimu b) wanafunzi katika utumizi wa mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika. Walimu na wanafunzi ndio walikuwa kitovu cha data. Vifaa vya ukusanyaji data vilivyotumiwa ni mahojiano, hojaji na mwongozo wa uchunzaji darasani huku mirudio, asilimia, maelezo na majedwali yakitumiwa katika uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti

e) Ikiwa kuna changamoto katika matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili. Katika madhumuni haya, walimu na wanafunzi ndio walikuwa kitovu cha data iliyokusanywa. Hojaji na mahojiano ndio vifaa vilivyotumiwa kukusanya data huku mirudio, asilimia, maelezo, majedwali na grafu vikitumiwa katika uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti

### 3.11 Suala la Maadili

Kabla ya kuanza utafiti, Mtafiti alipata waraka wa utambulisho kutoka Chuo kikuu cha Kenyatta. Barua hii ilimsaidia kupata kibali cha kufanya utafiti kutoka Kamati ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI). Mtafiti aliwasilisha kibali hicho kwa wizara ya elimu kaunti ya Nairobi. Mtafiti alipeleka barua za kibali na idhini ya kufanya utafiti kwa wakuu wa shule zilizoteuliwa kufanyia utafiti. Utafiti ulitekelezwa kwa njia ya uwazi na uaminifu na kuhakikisha kuwa data iliyokusanywa ilikuwa sahihi. Majibu, maoni na matokeo yaliyopokelewa kutoka kwa watafitiwa yaliheshimiwa na kutumiwa tu kwa shughuli za utafiti wala si kwa shughuli zingine za nje ya utafiti. Uhalali wa kazi ulitiliwa maanani ikizingatiwa kuwa wizi wa kitaaluma ni kinyume na maadili ya kiakademia. Kulingana na Miller, Shoptaught na Wooldridge (2012) wizi wa kitaaluma huhusisha wizi wa maandishi, fikra au vifungu vya maandishi ya watafiti au wasomi wengine bila kubaini kwa nukuu kuhusu asilia ya kazi hiyo. Utafiti huu ulitilia maanani sheria zote za kitaaluma kwa kutambua mchango wa watafiti wengine na kuzingatia unukuzi sahihi wa mawazo na tafiti zao.

# SURA YA NNE

# UWASILISHO, UCHANGANUZI NA MAJADILIANO YA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii iliwasilisha uchanganuzi wa data ya utafiti, matokeo na mijadala. Lengo la utafiti lilikuwa ni kuchunguza ikiwa mbinu ya matumizi ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili inaweza kuimarisha matokeo ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi. Takwimu za utafiti ziliingizwa kwa tarakilishi na kukokotolewa kwa kutumia programu ya tarakilishi ya SPSS (Huduma ya Tarakilishi katika Uchunguzi wa Tarakimu). Uchanganuzi wa data ulitokana na maswali yafuatayo ya utafiti:

i) Ni mbinu zipi zinazotumika kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili?

ii) Je, ni kwa kiwango kipi mbinu ya maigizo inatumika katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili?

iii) Mbinu ya maigizo ina athari gani katika uelewa wa wanafunzi katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili,

iv) Je, a) Walimu b) Wanafunzi wana mtazamo gani kuhusu utumizi wa mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili?

v) Je, kuna changamoto zozote zinazokumba matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili?

### 4.2 Demografia ya Wahojiwa

Matokeo ya sehemu hii yaliwasilishwa kwa kuzingatia sifa za kibinafsi za wasailiwa waliyoshiriki katika utafiti. Sifa za wasailiwa ziliwakilishwa kwa kurejelea jinsia, umri na kiwango cha elimu. Kulingana na Mugenda na Mugenda (2013) Matokeo ya utafiti yanaweza kulinganishwa na idadi nzima ya watu kwa sababu sifa za sampuli iliyotumika ni kielelezo mwafaka cha idadi hiyo. Hivyo basi demografia ya watafitiwa huchangia matokeo yanayoweza kutegemewa kwa kukipa kila kipengele uhalisia unaofaa.


#### 4.2.1 Usambazaji wa Hojaji

Hojaji 248 zilisambazwa kwa wanafunzi 240 na walimu 8 wakati wa utafiti huu. Hojaji zilizosambazwa zililenga kupata habari kuhusu matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi. Mtafiti alizingatia kuchunguza shughuli za ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule 4 zilizoteuliwa kwa minajili ya utafiti.

Hata hivyo, jumla ya hojaji 200 ndizo zilirejeshwa na wanafunzi, kumaanisha kuwa wanafunzi 200 ndio walioshiriki kikamilifu katika utafiti wa mwisho, kutoa kiwango cha asilimia 83.3. Hojaji zote nane za walimu zilirejeshwa kutoa asilimia 100. Sampuli hii ya asilimia 83.3 ya hojaji za wanafunzi na asilimia 100 ya walimu ilizingatiwa kuwa bora kwa sababu iliafiki vizuri maoni ya Mugenda na Mugenda (2013) kwamba kiwango cha asilimia 60 na zaidi ya sampuli iliyokusanywa inaafiki malengo ya kinachotafitiwa.

### 4.2.2 Jinsia ya Walimu Wanaofundisha Fasihi

Data kuhusu jinsia ya walimu kutoka kwa shule zilizoshirikishwa katika utafiti imewakilishwa katika mchoro 4.1





**Mchoro 4.1 Jinsia ya Walimu Wanaofundisha Fasihi**

Matokeo kuhusu jinsia ya walimu waliokuwa wanafundisha riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, yanabaini jinsia ya kike iliwakilishwa na idadi ya asilimia 63 ya walimu wa fasihi nayo jinsia ya kiume ikiwakilishwa na asilimia 37. Matokeo haya yanaashiria walimu wa kike wametawala ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili katika shule za upili kaunti ya Nairobi. Utafiti huu unaafiki matokeo ya Babusa (2010), yanayoonyesha ya kwamba, pana tofauti ya kijinsia katika ufundishaji wa lugha. Jinsia ya kike ikitazamiwa kufanya vyema katika masomo ya lugha.

### 4.2.3 Umri wa Walimu Wa Fasihi

Utafiti huu ulichunguza umri wa walimu wanaofundisha somo la Kiswahili na hasa fasihi na matokeo yameonyeshwa katika mchoro 4.2





**Mchoro 4.2 Umri wa Walimu wa Fasihi**

Matokeo katika mchoro 4.2 yanadhihirisha kuwa asilimia 50 ya walimu wa Kiswahili wana umri wa kadri ya miaka (41-50), umri wa miaka kati ya (31-40) waliwakilishwa kwa asilimia 25 nao waliokuwa baina ya miaka (21-30) wakiwakilishwa kwa asilimia 12.5. Umri wa juu zaidi, kati ya miaka (51-60) waliwakilishwa kwa asilimia 12.5. Kutokana na matokeo haya, utafiti ulibaini ya kwamba idadi kubwa ya asilimia 50 ya walimu wa fasihi katika shule za upili walikuwa kati ya miaka miaka (41-50).

Matokeo haya yanaonyesha kuwa walimu wanaofundisha fasihi wana tajiriba ya miaka mingi kwa hivyo wana uwezo mkubwa wa kuelewa mikakati ya kufundisha fasihi katika shule za upili.

### 4.2.4 Kiwango cha Elimu

Matokeo ya utafiti kuhusu kiwango cha elimu ya walimu wa fasihi yamewasilishwa katika mchoro 4.3.





**Mchoro 4.3 Walimu wa Fasihi Kulingana na Kiwango cha Elimu**

Matokeo katika mchoro 4.3 yanaonyesha kuwa asilimia 50 ya walimu walioshiriki katika utafiti walimiliki shahada ya elimu ya chuo kikuu na asilimia 25 walimiliki vyeti vya stashahada na asilimia 25 shahada ya uzamili. Kwa kuzingatia matokeo haya ni bayana kuwa walimu wa fasihi ya Kiswahili katika shule za upili wamehitimu vyema kimasomo hivyo kuwawezesha kufundisha fasihi kwa njia bora zaidi. Hivyo basi, kiwango chao cha elimu cha walimu hawa hakiwezi kuwazuia kutekeleza ujifunzaji na ufundishaji wa wahusika katika riwaya kwa kitumia mbinu ya maigizo. Matokeo haya yanaafikiana na ya Momanyi (2012), anayesema kuwa uhakiki wa tajiriba, taaluma na mafunzo ya awali ya walimu yaliboresha matokeo ya wanafunzi katika stadi ya lugha ya Kiswahili. Hali

hii imethibitishwa pia katika uchunguzi wa Sifuna, Chege na Oanda (2006) kwamba mabadiliko ya elimu kutofaulu hujiri kwa sababu ya kozi duni wanazofanya wakufunzi vyuoni kwani baadhi ya walimu hawapati mafunzo sahihi ya kuwawezesha kuwa na uwezo wa kufundisha fasihi ya Kiswahili.

### 4.2.5 Tajiriba Katika Ufundishaji wa Kiswahili

Katika utafiti tajiriba ya walimu ilitofautiana kwa kiasi kikubwa. Kuna walimu waliyokuwa wamefunza hadi miaka ishirini. Tajiriba ya ufundishaji imewakilishwa katika mchoro 4.4.




**Mchoro 4.4 Tajiriba katika ufundishaji wa Kiswahili**

Utafiti huu ulionyesha kuwa asilimia kubwa (50%) ya walimu walikuwa na tajiriba ya miaka (11-15) katika ufundishaji wa riwaya, asilimia 25 kwa miaka (6-10) ilhali asilimia 13% ya walimu waliripotiwa kuwa na tajiriba ya kufunza kwa muda wa miaka kati ya (16-20). Hali hii inaafika kauli ya Gathumbi na Ssebbunga (2005) kuwa kuna walimu wengi katika shule za upili waliohitimu vyuoni.

Matokeo haya yanabaini, licha walimu wengi kuwa na tajiriba kubwa, hawakuwa na mwao kuhusu mbinu mbora za ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili

### 4.2.6 Vipindi vya Riwaya

Somo la Kiswahili kwa mujibu wa ratiba za shule za upili lilitengewa vipindi sita. Katika vipindi hivi, shule mbalimbali zilitenga somo la fasihi kuwa na vipindi tofauti tofauti ilivyoonyeshwa katika jedwali 4.1.


**Jedwali 4.1: Vipindi vya Riwaya vilivyoripotiwa kufunzwa na Walimu**

| Idadi ya vipindi | Mirudio | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| **Kipindi kimoja** | 1 | 12.5 |
| **Vipindi viwili** | 4 | 50.0 |
| **Vipindi vitatu** | 2 | 25.0 |
| **Vipindi vinne** | 1 | 12.5 |
| **Vipindi vitano** | 0 | 0 |
| **Vipindi sita** | 0 | 0 |
| **Jumla** | **8** | **100** |

Matokeo ya utafiti kulingana na Jedwali 4.1 yanaonesha asilimia 50 ndiyo ilikuwa idadi ya juu kwa walimu walioripoti kuwa na vipindi viwili pekee vya uchambuzi wa riwaya ya Kiswahili kwa juma moja. Haya yanathibitisha kuwa ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili haujapewa muda wa kutosha.

### 4.2.7 Jinsia ya Wanafunzi


Mtafiti alikusanya data ya jinsia ya wanafunzi kutoka shule zilizoshirikishwa na kuwasilishwa katika mchoro 4.5.




**Mchoro 4.5: Uwasilishaji wa Wanafunzi wanaofundishwa riwaya Kijinsia**

Matokeo yaliyolenga jinsia ya wanafunzi walioshiriki katika utafiti yanaonyesha idadi kubwa 104 (52%) ya wanafunzi walikuwa wa jinsia ya kike huku idadi ya jinsia ya kiume ikiwakilishwa na 96 (48%). Matokeo haya yanabaini ya kwamba, hakuna tofauti kubwa ya kijinsia tunaporejelea hali ya usajili wa wanafunzi katika shule za upili. Hii inaonyesha kwamba jinsia zote mbili zilihusishwa kikamilifu katika utafiti huu.

**4.2.8 Umri wa Wanafunzi Walioshiriki katika UtafitiSehemu hii ilibaini miaka ya wanafunzi walioshiriki katika utafiti huu.** Mchoro 4.6 uliwakilisha umri wao.




**Mchoro 4.6   Umri wa Wanafunzi**

Utafiti huu ulibaini asilimia ya juu (68.5%) ya wanafunzi walikuwa kati ya miaka 15-19, waliyokuwa na miaka kati ya 10-14 waliwakilishwa kwa asilimia 28.0 ilhali waliokuwa kati ya miaka 20 na zaidi waliwakilishwa kwa asilimia 3.5. Matokeo haya yanamaanisha wanafunzi wengi walioshiriki katika masomo walikuwa katika umri unaostahili kuwa katika shule ya upili na kushiriki kikamilifu katika mbinu zinazotumiwa kufundishia masomo darasani. Kwa mujibu wa utafiti wa Aysun, Meziyet na Mübeccel (2013), watu wenye umri mdogo wanapenda kuigiza na huchangia kukuza ubunifu wakati wanapoigiza.

### 4.3 Mbinu za Ufundishaji wa Kipengele cha Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili

Madhumuni ya kwanza ya utafiti huu yalikuwa ni kuchunguza mbinu zinazotumiwa kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili. Katika utafiti huu walimu walitumia mbinu tofauti katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Mbinu hizi zimewakilishwa katika jedwali 4.2.

**Jedwali 4.2: Mikakati Iliyotumiwa na Walimu Kufundisha Wahusika katika Riwaya**

| **Mbinu** | **Kila wakati** | | **Mara moja** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Idadi ya walimu** | **Asilimia (%)** | **Idadi ya walimu** | **Asilimia (%)** |
| **Usomaji wa kipekee** | 1 | 12.5 | 7 | 87.5 |
| **Usomaji wa pamoja** | 1 | 12.5 | 7 | 87.5 |
| **Usomaji wa unachopenda** | 3 | 37.5 | 5 | 62.5 |
| **Usomaji wa kimya** | 5 | 62.5 | 3 | 37.5 |
| **Usomaji kwa sauti** | 6 | 75.0 | 2 | 25.0 |
| **Usomaji wa mzunguko** | 4 | 50.0 | 4 | 50.0 |
| **Maigizo** | 1 | 12.5 | 7 | 87.5 |

Kutokana na uchanganuzi katika jedwali la 4.2, ilibainika kuwa usomaji kwa sauti (75.0%) ni mojawapo ya mbinu kuu iliyotumiwa na walimu kufunza fasihi katika shule za upili. Usomaji wa kipekee, usomaji wa pamoja na maigizo ndizo mbinu ambazo hazikupendelewa na walimu katika kufundisha riwaya ya Kiswahili. Mbinu ya maigizo inapaswa kujumuishwa katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili kila wakati ili kuboresha matokeo ya fasihi. Usomaji kwa sauti ulijitokeza kama mbinu

iliyopendelewa na walimu kufundisha fasihi madarasani. Hii imechangiwa na ukweli kwamba walimu wengi wanaamini kuwa wanafunzi wanaposoma kwa sauti, wanaweza kusikiliza , kuelewa,kutoa maoni na kufanya uchambuzi wa riwaya kwa kina.

Mbinu ya maigizo kama mbinu ya kufunza wahusika katika riwaya ya Kiswahili ilitumiwa mara moja tu. Matokeo haya yanamaanisha kuwa matumizi ya mchezo wa kuigiza hayatekelezwi vyema na walimu licha ya umuhimu wake katika kukuza dhana ya kibinafsi na ubunifu miongoni mwa wanafunzi wakati wa kufundisha riwaya ya Kiswahili.

Matokeo haya yaliafikiana na ya Chepkoech (2012), aliyetafiti kuhusu kutathimini mikakati ya ufundishaji iliyotumiwa na walimu wa Kiingereza, anakiri kuwa kusoma kupitia maigizo ndiyo mbinu mwafaka inayotakikana kutumiwa shuleni, kwa sababu husaidia wanafunzi kupata ujasiri na kujitathimini wanapohitaji kutumia lugha kwa hiari au kwa jukumu la kushiriki katika maigizo. Kwa hivyo, ni wazi kwamba matumizi ya mbinu ya maigizo yakizingatiwa na walimu matokeo ya Kiswahili yataimarika.

### 4.3.1 Mbinu za Kufundisha Wahusika katika Riwaya ilivyoripotiwa na Wanafunzi

Mbinu mbalimbali zilitumiwa kufundisha riwaya ya Kiswahili darasani. Matumizi ya mbinu hizi ilivyoripotiwa na wanafunzi imewasilishwa katika jedwali 4.3.

**Jedwali 4.3: Mbinu zilizotumiwa Kufundisha Wahusika zilivyoripotiwa na Wanafunzi**

| Mbinu | Mara Nyingi | | Mara Chache | | Haitumii | | Jumla N=200) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % |
| **Majadiliano** | 79 | 39.5 | 56 | 28.0 | 65 | 33 | 200 | **100** |
| **Kazi ya makundi** | 89 | 44.5 | 45 | 22.5 | 66 | 33 | 200 | **100** |
| **Maigizo** | 12 | 6.0 | 87 | 43.5 | 101 | 51 | 200 | **100** |
| **Mhadhara** | 98 | 49.0 | 24 | 12.0 | 78 | 39 | 200 | **100** |
| **Mdahalo** | 46 | 23.0 | 76 | 38.0 | 78 | 39 | 200 | **100** |
| **Ziara nyanjani** | 26 | 13.0 | 122 | 61.0 | 52 | 26 | 200 | **100** |
| **Alama wastani** | **58.33** | **29.20** | **68.33** | **34.20** | **73.33** | **36.80** | **200.00** | **100.0** |

**N**=200; **CI**=95%

Matokeo yanaonyesha idadi ya juu ya asilimia 98 ya wanafunzi walikiri kwamba mbinu ya mhadhara ndiyo ilitumiwa mara nyingi darasani kufundishia riwaya ya Kiswahili. Kwa upande mwingine, asilimia 51 ya wanafunzi walisema kwamba mbinu ya maigizo haikutumika kamwe katika shule zao ilhali asilimia 6.0 ya wanafunzi walikubali kwamba ilitumika kila wakati.

Matokeo haya yanaonyesha kuwa ufundishaji na usomaji wa wahusika katika riwaya za Kiswahili katika shule za upili yametawaliwa na mbinu ya mhadhara. Matokeo haya yanaungwa mkono na utafiti wa Kang'ahi na wengine (2004), waliyotafiti kuhusu nyenzo za ufundishaji na matokeo ya wanafunzi katika somo la Kiswahili katika shule za upili. Kategoria ya tatu katika mbinu za ufundishaji, yalionyesha mbinu ya mhadhara (43.20%) ndiyo ilitumika zaidi katika kufundisha lugha ya Kiswahili.

Matumizi mengi ya mbinu ya mhadhara yanamaanisha kwamba madarasa ya lugha ya Kiswahili yamejikita katika matumizi ya mbinu za jadi za kufundishia ambapo walimu wanajiona kama ndiyo kitovu cha pekee katika kutoa maarifa. Kwa hivyo wanafunzi wanasalia kuwa watazaji na hushiriki katika utendaji pale tu wanapopewa fursa na walimu wao. Zaidi ya hayo, uchunzaji ulifanywa darasani ili kubaini mbinu ambazo walimu walitumia kufundisha wahusika katika riwaya za Kiswahili. Matokeo yaliwasilishwa katika Jedwali 4.4.

**Jedwali 4.4: Uchunzaji kuhusu Mbinu zilizotumiwa na Walimu wa Riwaya ya Kiswahili Darasani**

| **Mbinu za ufundishaji** | **Waliotumia mbinu** | **Asilimia** | **Wasiotumia mbinu** | **Asilimia** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Kuuliza maswali** | 7 | 87.5 | 1 | 12.5 | 8 |
| **Mihadhara** | 5 | 62.5 | 3 | 37.5 | 8 |
| **Mijadala darasani** | 4 | 50.0 | 4 | 50.0 | 8 |
| **kazi ya makundi** | 3 | 37.5 | 5 | 62.5 | 8 |
| **Kusoma** | 6 | 75.0 | 2 | 25. | 8 |
| **Uigizaji** | 2 | 25.0 | 6 | 75.0 | 8 |

Matokeo ya uchunzaji darasani yalionyesha kuwa walimu 7 (87.5%) waliratibia kutumia mbinu ya kuuliza maswali walipokuwa wakifundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Zaidi ya hayo, walimu 5 (62.5%) walitumia mbinu ya mhadhara, walimu 4 (50.0%) walitumia mbinu ya mijadala darasani nao 3 (37.5%) wakitumia mbinu ya kazi ya makundi. Hata hivyo, mbinu ya uigizaji ilitumiwa na walimu 2 (25.0%) pekee.

Matokeo haya yanaonyesha vipindi vya fasihi katika shule za upili nchini Kenya vimetawaliwa na mbinu ya kuuliza maswali na mihadhara. Matokeo haya yanaafikiana na utafiti wa Murunga (2013) kuwa mwalimu ndiye alitawala ufundishaji na ujifunzaji wa mashairi ya Kiswahili ,hivyo kuathiri kwa njia hasi matokeo ya wanafunzi. Haya yalibainika aliposhiriki uchunzaji wa vipindi kumi na viwili darasani kwa kuchunguza namna walimu walipofundisha. Matokeo haya pia yanaungwa mkono na utafiti wa Wasike (2011) aliyetambua na kuripoti kwamba mwalimu anapotawala somo, wanafunzi hawakuweza kuelewa maelezo katika mada za ushairi. Ilibainika, ingawa mbinu ya maigizo na majadiliano ziliratibiwa kwenye maazimio ya kazi, hakukuwa na ushahidi wa kutosha kwamba mbinu hizo zilitumika darasani kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Isayi (2007) anakubaliana na maoni ya Wasike (2011) kwa kupendekeza wanafunzi kuhusishwa katika shughuli za uigizaji katika vipindi vya masomo.

Matokeo haya yanaungwa mkono na utafiti wa Agonya na wengine (2019) waliotafiti kuhusu athari ya mbinu za kufundishia kwa matokeo ya wanafunzi. Utafiti ulibaini kuwa walimu wote wa Kiswahili walioshiriki kwenye utafiti walitumia mbinu ya kuuliza maswali kama mbinu ya kufundishia. Asilimia 91.7 ya walimu walitumia mbinu ya mhadhara, asilimia 83.3 walitumia majadiliano, asilimia 58.3 walitumia kazi ya makundi, huku asilimia 16.7 wakitumia ufanani, hata hivyo hakuna yeyote aliyetumia mbinu ya sanaa tuli na kuigiza kwa kuiga. Ni wazi kwamba walipendelea mbinu ya kuuliza maswali badala ya kurejelea mbinu zingine ambazo zingeboresha zaidi matokeo ya wanafunzi.

Ni dhahiri kutokana na matokeo kwamba kazi ya makundi haikutumika sana na walimu wa shule za upili za umma katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya, kaunti ya Nairobi. Kinyume na matokeo ya utafiti, Suter na Busienei (2013) katika utafiti wao kuhusu vifaa na mikakati iliyotumiwa na walimu wa shule ya upili kufundishia fasihi simulizi ya Kiswahili katika kaunti ya Marakwet walibaini kuwa mbinu ya mijadala ni mojawapo ya mbinu iliyotumiwa mara kwa mara ili kudumisha ilhamu ya kusoma fasihi simulizi ya Kiswahili darasani. Kwa kuongezea, Wamokhela (2012) aliangalia mjadala kama njia bora ya kufundisha fasihi ya Kiswahili. Alipendekeza kwamba, ili mbinu hii itumiwe ipasavyo ni vyema maandalizi ya kutosha yafanywe kabla ya kuitumia darasani.

## 4.4 Kiwango cha Matumizi ya Mbinu ya Maigizo kwa Kufundisha Kipengele cha Wahusika

Madhumuni ya pili ya utafiti huu yalikuwa ni kuchunguza kiwango cha matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili. Matokeo yaliwasilishwa katika sehemu zifuatazo:

### 4.4.1 Kiwango cha Matumizi ya Mbinu ya Maigizo katika Ufundishaji wa Wahusika

Walimu na wanafunzi waliulizwa kuhusu kiwango cha matumizi ya mbinu ya maigizo ya wahusika katika riwaya ya Kiswahili Matokeo yaliwalishwa katika jedwali 4.5.

**Jedwali 4.5: Uzoefu wa Kutumia Mbinu ya Maigizo katika Ufundishaji wa Wahusika**


| Uzoefu wa Kutumia Mbinu ya Maigizo | Walimu (N=8) | | Wanafunzi (N=200) | |
|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| **Kila wakati** | 2 | 25.0 | 12 | 6.0 |
| **Mara moja** | 6 | 75.0 | 87 | 43.5 |
| **Haitumiki** | 0 | 0.0 | 101 | 50.5 |
| **Jumla** | **8** | **100.0** | **200** | **100.0** |

Kulingana na matokeo ya utafiti uliofanywa, idadi kubwa (75.0%) ya walimu waliosailiwa walikubali ya kwamba mbinu ya maigizo ilitumika katika ufundishaji wa wahusika mara moja tu kwa mwezi. Matokeo ya wanafunzi yalioyesha asilimia kubwa (50.5) walibaini matumizi ya mbinu ya maigizo haikutumiwa kamwe katika ufundishaji wa vipindi vya fasihi.

Matokeo haya yanamaanisha kuwa walimu wengi katika shule zilizofanyiwa utafiti wanatumia mbinu ya maigizo mara chache sana katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya za Kiswahili.

### 4.4.2 Wanafunzi Walivyopatiwa Mazoezi Kupitia Nyenzo ya Ufanani

Wanafunzi waliulizwa kutaja idadi ya vipindi walivyofunzwa wahusika katika riwaya ya Kiswahili kwa kutumia mbinu ya ufanani. Matokeo haya yameonyeshwa katika Mchoro 4.7.




**Mchoro 4.7 Zoezi la kusoma kwa matumizi ya mbinu ya ufanani**

Kwa mujibu wa matokeo ya Mchoro 4.7, ni bayana kuwa asilimia ya juu (49.0%) ya wanafunzi waliripoti kuwa walipewa zoezi la kuchambua wahusika katika riwaya kwa kutumia ufanani mara moja tu kwa wiki. Zaidi ya hayo, matokeo yalionyesha asilimia 39.0 walipewa zoezi kwa kutumia ufanani baada ya mwezi mmoja. Hata hivyo, asilimia 4.0 ya wanafunzi waliripoti hawakupewa mazoezi ya kusoma namna ilivyotakikana katika somo la wahusika. Matokeo katika utafiti huu yanaonyesha kuwa walimu hawatilii maanani matumizi ya nyenzo ya maigizo wakati wa kufundisha wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Matokeo haya yanaungwa mkono na utafiti wa Buiaya na Mkumbwa (2017) waliotafiti kuhusu ufungamanisho wa fasihi simulizi na riwaya ya Kiswahili ya kimajaribio, ambapo walibaini kuwa mchango wa walimu ni muhimu katika ufundishaji wa fasihi darasani. Kwa hivyo ni wazi kwamba walimu wanapaswa kujenga mwelekeo chanya ili kuzalisha mabadiliko yanayostahili katika usomaji na uchambuzi mwafaka wa riwaya ya Kiswahili kwa kutumia nyenzo inayowashirikisha wanafunzi kama mbinu ya maigizo.

### 4.5 Athari ya Matumizi ya Mbinu ya Maigizo katika Matokeo ya Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili

Madhumuni ya tatu ya utafiti huu yalikuwa ni kubaini athari ya mbinu ya maigizo kwa uelewa wa wanafunzi katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili. Matokeo katika sehemu hii yaliwasilishwa chini ya mada zifuatazo.

#### 4.5.1 Jinsi Mbinu ya Maigizo Ilivyowavutia Wanafunzi Nyakati za Mafunzo ya Wahusika

Wanafunzi walipokuwa wakifundishwa kipengele cha wahusika katika riwaya ya *Chozi la Heri* (Assumpta, 2021). Uelewa wao uliathiriwa na mbinu mbali mbali zilizotumiwa na walimu wakati wa kufundisha. Athari hizi zimewasilishwa katika jedwali 4.6.

**Jedwali 4.6: Athari ya Mbinu ya Maigizo katika Somo la Wahusika**

| Stadi | Naelewa haraka | | Naelewa wastani | | Naelewa pole pole | | Sielewi | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % |
| **Fanani** | 102 | 51.00 | 46 | 23.00 | 48 | 24.00 | 4 | 2.00 |
| **Sanaa tuli** | 97 | 48.50 | 58 | 29.00 | 43 | 21.50 | 2 | 1.00 |
| **Kuigiza kwa kuiga** | 156 | 78.00 | 37 | 18.50 | 4 | 2.00 | 3 | 1.50 |
| **Wastani** | **118.3** | | **47.0** | | **31.7** | | **3.0** | |
| **Alama tenganisho** | **32.72** | | **10.54** | | **24.09** | | **1.00** | |

**Jumla 200**

Kutokana maoni ya waliohojiwa, idadi ya juu ya asilimia 78.0 ya wanafunzi walioshiriki katika utafiti walibaini kwenye hojaji kuwa, kufundishwa kwa matumizi ya mbinu ya kuigiza kwa kuiga iliwasaidia kuelewa na kukumbuka wahusika kwa haraka. Matokeo katika Jedwali 4.6 yalionyesha zaidi katika safu ya 'naelewa haraka' ilikuwa na alama

wastani kubwa zaidi (Wastani 118.3) katika mikakati yote mitatu ya maigizo.Kwa upande mwingine, washiriki waliokiri kwamba hawakuelewa uchambuzi wa wahusika kwa matumizi ya mbinu hizo zilizotumika ndio waliopata alama ya chini zaidi (wastani 3.0).

### 4.5.2 Matokeo Kutokana na Uchunzaji

Uchunzaji ulibaini kuwa mwingiliano wa mwalimu na wanafunzi ulihimairika darasani mbinu ya maigizo ilipotumika. Wanafunzi pia walionekana kuwa makini wakati wa vipindi vya uchambuzi wa riwaya .

Utafiti uliofanywa kupitia uchunzaji ulidokoa kuwa nafasi ya kushirikishwa kwa wanafunzi ulihiniwa katika vipindi vingi vya fasihi ambapo mwalimu alitawala somo kwa kusimulia na kufafanua dhana mbalimbali akitumia mbinu ya mhadhara. Utafiti uligundua zaidi kuwa wakati wa uchambuzi wa riwaya, wanafunzi walishirikishwa kwa kugawana na kusoma aya za riwaya ukurasa baada ya mwingine huku mwalimu akiingilia kati mara kwa mara kuwachambulia wahusika. Hali hii ilionyesha, wanafunzi walinyimwa majukumu ya kuigiza wahusika ili waelewe vizuri kwa kushiriki kwa namna hai.

### 4.5.3 Mjarabu wa Fasihi (Riwaya ya Chozi la Heri)

Mjarabu ulilenga kutathmini uelewa wa mwanafunzi katika uchambuzi wa wahusika katika riwaya ya Chozi la Heri (Assumpta, 2021). Mwanafunzi alipaswa kusoma na kujibu maswali yote kwa usahihi kuhusu wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

Utafiti huu ulilenga sampuli ya wanafunzi 240 ambapo 120 walikuwa katika kundi dhabiti sawa na wengine 120 katika  kundi jaribio. Hata hivyo, wakati wa mjarabu, jumla

ya wanafunzi 200 ndio walioshiriki kati yao 100 walikuwa katika kundi dhabiti sawa na wengine 100 walikuwa katika kundi jaribio.Sehemu hii ilichambua awamu zote mbili za matokeo ya mjarabu kwa kuelezea, kulinganisha na kujadili. Matokeo haya yaliwasilishwa ifuatavyo.

### 4.5.4 Uchanganuzi wa Mjarabu wa Kwanza

Mjarabu wa kwanza ulifanywa na makundi yote mawili ya kundi jaribio na kundi dhabiti. Matokeo yaliwasilishwa katika jedwali 4.7.

**Jedwali 4.7: Utuzaji wa Alama (Mjarabu wa Kwanza)**

| Kiwango cha alama (x/40) | Kundi dhabiti (Jumla=100) | | Kundi jaribio (Jumla=100) | |
|---|---|---|---|---|
| | **Idadi** | **Asilimia (%)** | **Idadi** | **Asilimia (%)** |
| **1 – 10** | 27 | 27.0 | 31 | 31.0 |
| **11 – 20** | 59 | 59.0 | 57 | 57.0 |
| **21 – 30** | 12 | 12.0 | 11 | 11.0 |
| **31 – 40** | 2 | 2.0 | 1 | 1.0 |
| **Jumla** | **100** | **100.0** | **100** | **100.0** |

Matokeo yalibainisha kuwa alama za juu zilizorekodiwa zilikuwa ni asilimia 59.0 katika kundi dhabiti na asilimia 57.0 katika kundi jaribio. Alama hizi zilijitokeza katika kiwango cha alama 11-20. Alama za chini zaidi zilibainiwa katika kiwango cha 31-40 ambapo kundi dhabiti lilirekodi asilimia 2.0 na kundi jaribio asilimia 1.0.

Katika uchanganuzi zaidi wa data, tofauti ya matokeo ya wastani baina ya kundi dhabiti na kundi jaribio yalipatikana kwa kutumia takwimu za maelezo kama vile alama wastani na alama tenganisho. Jaribio la T-test lilifanywa kutathmini ikiwa kuna tofauti za kitakwimu katika alama za matokeo baina ya kundi dhabiti na matokeo ya kundi jaribio. Takwimu za data iliyochanganuliwa ziliwasilishwa katika jedwali 4.8.

**Jedwali 4.8: Takwimu za Uchanganuzi wa Mjarabu wa Kwanza kati ya Kundi Jaribio na Kundi Dhabiti**

| **Vikundi** | **Idadi** | **Wastani** | **Alama tenganisho** | **T** | **Tofauti ya alama wastani** | **Umuhimu (p≤5%)** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kundi dhabiti | 100 | 44.40 | 22.2047 | 0.33 | 1.64 | 0.76 |
| **Kundi jaribio** | 100 | 42.76 | 17.8312 | | | |

**Kiwango cha p≤.05; Kiwango cha CI=95%**

Uchanganuzi wa data ulibaini kulikuwa na tofauti ndogo katika matokeo ya alama wastani ya 1.64, kati ya gredi wastani ya kundi dhabiti na kundi jaribio. Matokeo katika Jedwali 4.8 yalionyesha zaidi hapakuwa na tofauti kubwa ya kitakwimu katika matokeo ya kundi dhabiti na kundi jaribio kwa sababu alama ya umuhimu (p) ilikuwa zaidi ya **.**05 (p =**.**76>.05). Matokeo haya yanamaanisha hapakuwa na tofauti kubwa ya matokeo ya alama wastani kati ya kundi dhabiti na kundi jaribio katika mtihani wa kwanza.

### 4.5.5 Uchanganuzi wa Mjarabu wa Mwisho

Mjarabu wa mwisho ulifanywa na wanafunzi wa kundi jaribio na kundi dhabiti.

Matokeo yalirekodiwa na kuwasilishwa katika jedwali 4.9.

**Jedwali 4.9: Utuzaji wa Alama (Mjarabu wa Mwisho)**

| Kiwango cha alama (x/40) | kundi dhabiti (Jumla=100) | | kundi jaribio (Jumla=100) | |
|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Asilimia (%) | Idadi | Asilimia (%) |
| **1 – 10** | 22 | 22.0 | 2 | 2.00 |
| **11 – 20** | 55 | 55.0 | 12 | 12.00 |
| **21 – 30** | 15 | 15.0 | 57 | 57.00 |
| **31 – 40** | 8 | 8.0 | 29 | 29.00 |
| **Jumla** | **100** | **100.0** | **100** | **100.00** |

**N=100**

Matokeo yalibainisha kuwa alama za juu zilizorekodiwa zilikuwa ni asilimia 55.0 za kundi dhabiti katika kiwango cha alama 11-20 na asilimia 57.0 katika kundi jaribio katika kiwango cha alama 21-30. Alama za chini zaidi zilibainika katika kiwango cha 31-40 ambapo kundi dhabiti lilirekodi asilimia 8.0 huku asilimia 2.0 zikirekodiwa katika kundi jaribio katika kiwango cha alama 1-10. Matokeo haya yalibaini kuwa wale wanafunzi waliokung'uta alama kati ya 21-31 katika kundi jaribio walikuwa ni wengi kwa asilimia 57 wakilinganishwa na asilimia 15 pekee wa kundi dhabiti. Hii inaashiria kuwa matokeo yaliimarika miongoni mwa wanafunzi wa kundi jaribio baada ya kufundishwa kwa matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika.

Katika uchanganuzi zaidi wa data, tofauti ya matokeo ya wastani baina ya kundi dhabiti na kundi jaribio yalipatikana kwa kutumia takwimu za maelezo kama vile alama wastani na alama tenganisho. Jaribio la *T-test* lilifanywa kutathmini ikiwa kuna tofauti za kitakwimu katika alama za matokeo baina ya kundi dhabiti na matokeo ya kundi jaribio. Data ya matokeo haya imewasilishwa katika Jedwali 4.10.

**Jedwali 4.10: Takwimu za Mjarabu wa Kundi Dhabiti na Kundi Jaribio**

| Vikundi | Idadi | Wastani | Alama tenganisho | T | Tofauti ya alama wastani | Umuhimu (p<5%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **kundi dhabiti** | 100 | 57.15 | 19.45 | | | |
| **kundi jaribio** | 100 | 84.86 | 8.73 | | | |
| **Kundi dhabiti x kundi jaribio Kiwango cha p≤ .05** | | | | 7.27 | 27.31 | 0.001 |

Uchanganuzi wa data ulibaini kulikuwa na tofauti kubwa ya alama wastani ya 27.31 baina ya kundi dhabiti na kundi jaribio. Matokeo katika Jedwali 4.10 yalionyesha zaidi kuwa kulikuwa na tofauti kubwa ya kitakwimu katika matokeo ya kundi dhabiti na kundi jaribio kwa sababu alama ya umuhimu (p) ilikuwa chini ya **.**05 (p=.001< **.**05). Matokeo haya yanamaanisha palikuwa na tofauti kubwa ya matokeo kati ya kundi dhabiti na kundi jaribio katika mtihani wa pili. Alama wastani ya kundi jaribio ilizidi alama wastani ya kundi dhabiti. Hii inaashiria kuwa matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundisha wahusika katika riwaya ya Kiswahili ni bora zaidi katika uchambuzi na uelewa wa wahusika. Utafiti unaafikiana na matokeo ya utafiti wa Bashayer (2014) ambaye alifanya utafiti kutaka kubaini athari ya kufundisha lugha ya Kiingereza kwa kutumia mbinu ya maigizo katika kukuza ubunifu wa wanafunzi. Matokeo yake yalipochanganuliwa ilibainika wazi kwamba kundi jaribio lilikuwa na matokeo yaliyoimarika kuliko kundi dhabiti. Kwa hivyo ni wazi kwamba matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundishia wahusika yana manufaa makubwa kwa kutoa matokeo bora ya mwanafunzi.

Matokeo haya pia yaliafikiana na maoni ya O'gara (2008) aliyetafiti kuhusu kujifunza sarufi ya lugha kupitia maigizo. Katika utafiti huo alitumia vikundi viwili vya wanafunzi. Matokeo katika mjarabu wa mwanzo na mjarabu wa mwisho yalipolinganishwa kuonyesha ufanisi wa mbinu ya maigizo na matumizi ya mbinu za kawaida. Matokeo yake yalibaini kuwa matumizi ya maigizo yalikuwa na matokeo bora kuliko mbinu za kawaida. Vile vile, matokeo ya utafiti huu yanaungwa mkono na Taskin (2013) aliyechunguza athari ya kufunzia maigizo kwa matokeo ya mtihani wa Sayansi. Matokeo yake yalibaini kulikuwa na tofauti kubwa mbinu ya maigizo ilipotumiwa katika kukuza ubunifu, mafanikio ya sayansi na ujuzi wa mchakato wa kisayansi.

Matokeo haya yanaungwa mkono na utafiti wa Lorna (2016) aliyetafiti kuhusu athari ya uigizaji katika mafanikio ya wanafunzi katika kujifunza lugha ya Kiingereza katika shule za upili za umma katika kaunti ya Meru. Matokeo yalionyesha kuwa mbinu za maigizo za kufundisha kama ufanani, kuigiza kwa kuiga, michezo ya lugha na sanaa tuli zilikuwa na ushawishi mkubwa katika kufaulu kwa mwanafunzi. Ilibainika uigizaji ulikuwa na umuhimu katika ufundishaji wa lugha ya Kiingereza ambapo matumizi yake yalikuwa bora kuliko mbinu ya mihadhara pia kulingana na Munther (2013), alisema kuwa kufundisha lugha ya Kiingereza kupitia mchezo wa kuigiza huwapatia wanafunzi nafasi ya kushiriki kutumia lugha hiyo darasani. Matumizi ya mbinu ya ufanani miongoni mwa wanafunzi iliimarisha mawasiliano yao na hivyo kuboresha matokeo ya wanafunzi. Hali hii inasaidia wanafunzi kuondoa hofu ya kimhemko, makosa ya sarufi na vikwazo vya kijamii. Kwa hivyo ni wazi kwamba matumizi ya mbinu ya maigizo inapotumika hukuza na kuimarisha jukumu la lugha ya Kiswahili na kufanikisha kufaulu kwa wanafunzi

### 4.6 Mitazamo ya Walimu na Wanafunzi kuhusu Mbinu ya Maigizo katika Ufundishaji wa Riwaya

Utafiti huu pia ulilenga kubaini mitazamo ya walimu na wanafunzi katika utumizi wa mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili. Matokeo yalichanganuliwa kwa mujibu wa maudhui kisha yakawasilishwa kwa njia ya nukuu kwa kurejelea mada zifuatazo

#### 4.6.1 Mitazamo ya Wanafunzi kuhusu Matumizi ya Mbinu ya Maigizo katika Ufundishaji wa Riwaya

Wanafunzi waliulizwa kuelezea jinsi matumizi ya mbinu ya maigizo ilivyoathiri uelewa na ujifunzaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Mhojiwa mmoja kutoka shule A alisema:

> *"Nilipenda matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundishia wahusika katika riwaya ya Chozi la Heri. Hii ilinisaidia kuelewa kwa ubatini sifa na umuhimu wa wahusika ambao hapo awali ilikuwa vigumu kuelewa uchambuzi wao.Hii ni kwa sababu wanafunzi hatukushirikishwa kikamilifu kama ilivyo katika matumizi ya mbinu ya maigizo."*

Mshiriki mwingine kutoka shule C alisema:

> *"Ilikuwa na athari chanya katika uelewa wangu wa dhana nyingi katika riwaya ya kiswahili. Imenipa motisha ya kujifunza zaidi, kwa sababu inahusika na maisha yetu ya kila siku."*

Katika uchanganuzi zaidi, mhojiwa kutoka shule B aliongeza kuwa:

> *"Ilibadilisha mtazamo wangu kuhusu uchambuzi na kuelewa wahusika wote katika riwaya.Kwa sasa nalipenda somo la fasihi kwa sababu naelewa mada yake vizuri"*

Mbali na hawa, mhojiwa mwingine kutoka shule D aliunga mkono maelezo ya wasailiwa wengine kwa kusema:

> *"Iliniathiri sana na kunifanya nipende zaidi somo la fasihi.Napenda sana matumizi ya mbinu ya maigizo. Kwa hakika uchambuzi wa wahusika kwa njia ya maigizo umekuwa wa kuvutia zaidi. Nimevutiwa sana kusoma fasihi ya Kiswahili na mbinu hii imenipa mshawasha wa kujihusisha sana na somo la Kiswahili.Kwa sasa nina utulivu wa nafsi kwa sababu ninaelewa vizuri uchambuzi wa wahusika katika riwaya ya Chozi la Heri."*

Uchanganuzi zaidi wa maoni ya wasailiwa yalionyesha mmoja wa wahojiwa akisema:

> *"Tulipokuwa katika madarasa ya chini, hamna kipindi kilichohusisha matumizi ya mbinu ya maigizo darasani.Vipindi vyote vilikuwa vya kuchokesha mno.Kile nichomaanisha ni kuwa, kila wakati tulirejelea faharasa katika kurasa za nyuma na sehemu ya yaliyomo ili kusoma kikamilifu sura za vitabu vya kiada.Wakati mwingine nilijumuika katika makundi ya mijadala,nadhani kwa sababu sikuhusishwa kikamilifu katika vipindi vya somo, licha ya hayo bado nilipita mtihani."*

Maoni yaliafiki kwamba matumizi ya mbinu ya maigizo yalikuwa na faida kubwa wakati yalipotumika darasani kama mbinu nyingine ya kufundishia. Kundi nzima lilisema ndio ilikuwa mbinu bora zaidi. Maoni haya yaliungwa mkono wakati sehemu kubwa ya wasailiwa walionyesha kupendelea matumizi ya maigizo badala ya mbinu zingine za kawaida.

Mhojiwa mmoja alisisitiza kwamba ikiwa mbinu ya maigizo itatumika ni muhimu kuihusisha kuwa ni sehemu mojawapo ya kimsingi itakayo tathminiwa.

> *"Tulikuwa na haya hapo awali tulipoihusiha katika mazoezi, lakini mwalimu hakutuelekeza kuhusu umuhimu wa maigizo. Nadhani inapaswa kufanywa kuwa muhimu zaidi. Namaanisha tunajua kuwa uandishi wa ripoti ni kitu tunachotathminiwa shuleni, kwa hivyo ikiwa tungetathminiwa katika maigizo bila shaka ningefanya vizuri zaidi katika matokeo yangu. Ninahitaji kumotishwa kwa kutuzwa kitu fulani wakati wa kufanya kitu lakini nadhani kwa kuwa mazoezi haya hayakuwa ya kawaida na ya kufurahisha, nilihisi kwamba sikuhitaji kutuzwa kamwe."*

### 4.6.2 Maoni ya Wanafunzi Kuhusu Hisia Zao Kutokana na Matumizi ya Mbinu ya Maigizo

Swali la awali kuhusu hisia za wanafunzi kuhusu matumizi ya mbinu ya maigizo, lililitoa majibu ya kutia moyo.Walipoulizwa wajieleze wenyewe , mshiriki wa kundi nambari 4 kutoka shule D alijibu kuwa ilikuwa ni furaha kubwa kufanya mazoezi ya kuigiza mbele ya wanafunzi wengine. Maoni haya yaliungwa mkono na takriban nusu ya kikundi wakati nusu nyingine ilisema walifurahia shughuli hiyo lakini tatizo ilichukua muda kabla ya kuwavutiwa kushiriki kikamilifu:

> *"Tulikuwa na mazoezi haya mengi katika shule ya upili na ndio sababu nadhani inafurahisha. Lakini niliimarika zaidi nilipoendelea kufanya mazoezi ya kuigiza wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Nadhani maigizo yanapaswa kutathminiwa kama zoezi la stadi ya kusikiliza na kuzungumza ili kutoa nafasi ya asilimia kubwa wanafunzi kushiriki kikamilifu.Ilinichukua muda kabla ya kuichangamkia shughuli hii ya maigizo; Sikujali sana matumizi ya mbinu hii hapo mwanzo. "*

Maoni zaidi kuhusu uwezo wa mchezo wa kuigiza katika kuendeleza fasihi ya Kiswahili yalitolewa kama ifuatavyo:

> *"Kwa sababu wakati mwingine mimi huwa na haya ninapowasilisha mbele ya hadhira. Matumizi ya mbinu ya maigizo yamenisaidia kuwa mkakamavu na kuweza kujiendeleza katika somo la kiswahili;…Nadhani nina ari sasa ya kuzungumza zaidi mbele ya hadhira na kwa wazungumzaji wengine wa Kiswahili katika mazingira ya nje ya shule. Nadhani mbinu hii ikitumika zaidi inaweza kuondoa uwoga na kujenga ujasiri katika hotuba yetu kwa sababu ya mazoea ya kutumia lugha ya Kiswahili katika shughuli za kila siku."*

### 4.6.3 Mitazamo ya Walimu Kuhusu Matumizi ya Maigizo katika Ufundishaji wa Riwaya

Walimu waliulizwa kutoa maoni yao kuhusu matumizi ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Mmoja wa waliohojiwa katika shule B aliripoti:

> *"Mmm…kwa zaidi ya miaka thelathini, mbinu ya maigizo imetumika kama nyenzo muhimu ya kufundisha lugha hasa katika riwaya ya Kiswahili na vipengele vingine vya fasihi. Hii ni kwa sababu wanafunzi wanajieleza kwa kutumia maneno yao wenyewe na hivyo kufurahia vipindi vya masomo darasani. Walimu wanaweza kutumia ishara ili kuwapa wanafunzi nafasi ya kujieleza zaidi wanapokuwa wakiwasilisha darasani. Hii inasaidia wanafunzi kuelewa zaidi badala ya mwalimu kuwa ndiye kitovu cha kutawala somo darasani."*
> (Mwalimu wa kike)

Matokeo ya hivi karibuni ya utafiti yameimarisha msimamo huu, kwa mfano Dunn na Stinson, (2011); Culham (2003) walidadavua faida inayotokana na shughuli ya matumizi ya maigizo kwa kupitia kazi ya wanafunzi na makongamano ya walimu kama ifuatavyo: shughuli za maigizo hutoa fursa ya kujenga mazingira halisi darasani ambapo wanafunzi wa viwango tofauti katika lugha hushiriki kikamilifu; Wanafunzi, mara nyingi husita kuzungumza lakini wanaweza kujiamini wakati matarajio ya lugha yanapoondolewa kabisa. Panapojiri wao kutumia maigizo, mienendo yao hubadilika mara moja na hivyo

kushiriki kikamilifu. Haya yanapotokea mwalimu husalia kuwa mshiriki kimya, masomo yanapoendelea darasani.

Kwa upande mwingine, Burke na O'Sullivan (2002) waligundua sababu saba za matumizi ya mchezo wa kuigiza katika ufundishaji wa lugha ya pili: walimu na wanafunzi wanaweza kuzingatia matamshi; wanafunzi wawe na motisha; wanafunzi watulie;wanafunzi watumie lugha kwa madhumuni halisi; wazizingatie sana kufanya makosa iliwaimarishe uelewa na ufahamu wa lugha; na wanafunzi na walimu waweze kurejelea mada zinazotatiza kwa kurejelea umuhimu wa matumizi ya maigizo katika ufundishaji wa lugha.

Matokeo haya pia yaliungwa mkono na Eckersley (2016), aliyetafiti kuhusu kutumia maigizo katika kukuza stadi za mawasiliano katika darasa la Karne ya 21, ilibainika kuwa mchezo wa kuigiza unawaruhusu wanafunzi kushiriki darasani kikamilifu na kusaidiana wanapotangamana na wengine. Ishara za sauti, usemi halisi na matumizi ya vifaa vya usimulizi husaidia hadhira kuelewa masimulizi ya hadithi simulizi, ya maandishi, ya kutunga au isiyo ya kutunga. Kwa hivyo ni bayana kuwa matumizi ya maigizo huendeleza mwingiliano kati ya wanafunzi na lugha ya mawasiliano na kuunda ulimwengu wa majukumu ya kijamii na mahusiano ambayo mwanafunzi huwa ni mshiriki hai.

### 4.6.4 Maoni ya Walimu kuhusu Umuhimu wa Matumizi ya Maigizo katika Vipindi vya Riwaya

Katika kutathmini maoni ya walimu kuhusu matumizi ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili, utafiti ulibaini kuwa wale walimu ambao

walifurahia na kupenda kufundisha walitumia mbinu tofautitofauti kama vile; kuiga kwa kuiga, Sanaa tuli, ufanani na mbinu zingine za maigizo. Ilibainika mbinu kama hizo zilihitaji mwalimu kuweka bidii zaidi katika kuandaa na kuwashirikisha wanafunzi. Hata hivyo, walimu wengi walitoa maoni kwamba kulikuwa na muda mfupi sana wa maandalizi ya matumizi ya mbinu hii; wengine waliona mbinu hii ilikuwa na shughuli nyingi mbali na vikwazo vingine. Ilibainika kuwa palikuwepo na mtazamo chanya katika matumizi ya mbinu ya maigizo, hali hii ilimsaidia mwalimu katika uteuzi na matumizi ya mbinu ya maigizo.


Matokeo haya yanafanana na yake Suter (2008) ambaye alibaini kuwa walimu hawana mtazamo mzuri katika ufundishaji na ujifunzaji wa tungo za Kiswahili kama Riwaya. Utafiti ulionyesha, walimu walifahamu vizuri wanafunzi walifurahia vipindi vya mchezo wa kuigiza lakini, walimu wengine bado walikuwa na hisia kwamba masomo kama hayo yalipendeza tu wanafunzi ambao mwishowe hawakujifunza chochote kutokana na matumizi yake. Maoni hasi kama haya ndiyo yaliyotajwa kama sababu mahususi inayochangia kutotumiwa darasani mchezo wa kuigiza wakati wa ufundishaji wa vipindi vya riwaya.

**4.7 Changamoto katika Ufundishaji wa Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili**

Madhumuni ya tano ya utafiti huu yalikuwa ni kutambua ikiwa kuna changamoto katika matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili.

### 4.7.1 Changamoto za Ufundishaji Wahusika katika Riwaya Darasani

Matokeo ya changamoto walizokumbana nazo walimu katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili yamewasilishwa kupitia Mchoro 4.8.




**Mchoro 4.8 Changamoto za Ufundishaji Wahusika katika Riwaya**

Matokeo ya utafiti yalionyesha uhaba wa muda ukiwa ndio changamoto kuu katika ufundishaji wa fasihi katika shule za upili. Hii iliripotiwa na idadi kubwa (asilimia 42) ya walimu. Matokeo haya yanaugwa mkono na utafiti wa Kiplagat (2015) katika matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji na usomaji wa Kiswahili, yalionyesha walimu wengi walilalama kuhusu muda waliotengewa kwenye ratiba ya masomo haukutosha kuandaa matumizi ya mbinu ya maigizo. Matatizo mengine yaliyoripotiwa na walimu ni kutomudu kutimiza mahitaji ya wanafunzi wengi darasani, uhaba wa vitabu vya riwaya vinavyochambuliwa darasani na muda mfupi uliotengewa kuchambua riwaya ya Kiswahili.

### 4.7.2 Changamoto Zilizobainishwa na Wanafunzi

Sio wanafunzi wote walionyesha kuwa na uweledi wa kuigiza majukwani wakati wa shughuli za maigizo ya wahusika ama kuwa na uwezo wa kukabiliana na changamoto za uwasilishaji mbele ya hadhira. Wanafunzi wachache walikubaliana kutokuwa na uwezo wa kustahimili kuigizaji tena jukwani. Kipawa cha uigizaji kilidhihirika kutopatikana kwa wanafunzi wote.

Katika utafiti wa mwisho wa kipengele hiki, msailiwa msichana alipoulizwa alivyohisi kuhusu matumizi ya mchezo wa kuigiza darasani. Mwanafunzi nambari 17 katika kutoka shule B. Alisema.

> *"Nadhani matumizi ya mbinu ya maigizo ni wazo nzuri, lakini sio kwa kila mtu. Watu wengine ni waoga. Ni vigumu kuigiza kama mhusika katika riwaya, mbele ya umati wa vijana. Nafahamu wanafunzi wengine huathiriwa na haya wanapojitolea kuchukua majukumu ya kuigiza mbele ya wenzao"*

### 4.7.3 Changamoto Zilizobainika Kupitia Mbinu ya Uchunzaji

Walimu wanane waliteuliwa na kutathiminiwa mara mbili kwa kutumia mbinu ya uchunzaji darasani.Matokeo ya uchuzaji ya vipindi kumi na sita yalionyesha, mafundisho mengi kuhusu wahusika yalitawaliwa na mwalimu huku wanafunzi wakinyimwa nafasi ya kushiriki na kuchangia kikamilifu kwa namna iliyo hai katika somo la wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Licha ya ukweli kwamba kulikuwa na shughuli chache za maigizo zilizozingatiwa wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa wahusika, sio wanafunzi wote katika vikundi walihusika kwa sababu walimu waliona ni shughuli iliyohitaji muda mwingi. Matokeo haya yanafanana na maoni ya Kisanda (2018) aliyetafiti kuhusu matumizi ya mchezo wa kuigiza katika kufunzia lugha kwa wanafunzi wa shule za upili

kwenye kaunti ndogo ya Kimilili. Aligundua kuwa walimu wengi hawakutumia mbinu ya maigizo ingawa walikubaliana kuwa matumizi ya mbinu ya maigizo yaliongeza uelewa wa lugha. Kwa hivyo ni wazi kuwa walimu wengi hawakuwa tayari kushiriki utumizi wa mbinu ya maigizo katika uchambuzi wa wahuiska katika riwaya ya Kiswahili ingawa wengi waliripoti kwamba wanafunzi wengi walishiriki vyema darasani wakati wa vipindi vya masomo ya fasihi mbinu ya maigizo ilipotumika.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo kwa kurejelea matokeo na mapendekezo ya utafiti zaidi.

## 5.2 Muhtasari

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza ikiwa mbinu ya matumizi ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili inaweza kuimarisha matokeo ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi. Muhtasari wa matokeo ya utafiti ulijadiliwa kurejelea madhumuni ya utafiti.

### 5.2.1 Mbinu za Ufundishaji Kipengele cha Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili

Kutokana na uchanganuzi wa data, matokeo ya walimu wengi yalibaini kuwa usomaji kwa sauti ni mojawapo ya mbinu kuu iliyotumiwa kufunza fasihi katika shule za upili. Usomaji wa kipekee, usomaji wa pamoja na maigizo ndizo mbinu ambazo hazikupendelewa na walimu katika kufundisha riwaya ya Kiswahili. Wanafunzi wengi walikiri mbinu ya mhadhara ndiyo ilitumiwa mara nyingi darasani kufundishia riwaya ya Kiswahili. Matokeo ya uchunzaji darasani yalionyesha walimu saba kati ya wanane walikuwa wanatumia mbinu ya kuuliza maswali walipokuwa wakifundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

### 5.2.2 Kiwango cha Matumizi ya Mbinu ya Maigizo kwa Kufundisha Kipengele cha Wahusika

Walimu waliosailiwa walikubali ya kwamba mbinu ya maigizo ilitumika katika ufundishaji wa wahusika mara moja tu kwa mwezi. Wanafunzi wengi walibaini kuwa matumizi ya mbinu ya maigizo haikutumiwa kamwe katika ufundishaji wa vipindi vya fasihi.Vile vile walitaarifu walipewa zoezi la kuchambua wahusika katika riwaya kwa kutumia mbinu ya ufanani mara moja kwa wiki. Utafiti ulibaini kuwa mbinu ya maigizo haikutumiwa mara nyingi na walimu wengi katika vipindi vyao. Hata hivyo, walimu waliorejelea matumizi ya mbinu hii waliitumia kwa vipindi vichache mno.Mbinu ya mhadhara ndiyo ilitumiwa sana na walimu darasani katika uchambuzi wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

### 5.2.3 Athari ya Matumizi ya Mbinu ya Maigizo katika Matokeo ya Wahusika katika Riwaya

Utafiti ulibaini idadi kubwa ya wanafunzi walikiri kufundishwa kwa njia ya kuigiza kwa kuiga iliwasaidia kuelewa na kukumbuka wahusika kwa haraka. Takwimu za mjarabu wa kwanza zilionyesha hapakuwa na tofauti kubwa katika matokeo ya kundi dhabiti na kundi jaribio kwa sababu alama ya umuhimu (p) ilikuwa zaidi ya 0.05 ($p = 0.76 > 0.05$). Kwa upande mwingine uchanganuzi wa mtihani wa mwisho ulibaini kulikuwa na matokeo bora katika kundi jaribio baada ya wanafunzi kufundishwa kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili kwa matumizi ya mbinu ya maigizo kwa takribani ya mwezi mmoja. Iligunduliwa kuwa mbinu ya maigizo ilipotumika darasani, umakinifu wa wanafunzi uliimarika kwa sababu walipewa nafasi ya kushiriki kwa namna hai. Vipindi hivi pia

viliimarisha mwingiliano wa mwalimu na wanafunzi maradufu. Katika vipindi hivi kazi ya mwalimu ilikuwa ni kuwagawia wanafunzi majukumu ya kuigiza aya za riwaya. Japo hali hii haikufanyika darasani wakati wa vipindi vya uchanganuzi wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

### 5.2.4 Mitazamo ya Wanafunzi na Walimu kuhusu Ufundishaji wa Wahusika katika Riwaya kwa kutumia Mbinu ya Maigizo

Walimu wengi walioshiriki kwenye utafiti walikubali kwamba walifurahia kutumia maigizo kama mbinu ya kufundishia wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

Utafiti ulionyesha walimu wengi walihisi kwamba matumizi ya mbinu ya maigizo katika uchambuzi wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili yalikuwa ni bora na yaliimarisha matokeo ya Kiswahili. Japo wengi wao hawakupendelea kuitumia kwa sababu ya muda mfupi na vipindi vichache vilivyotengewa somo la riwaya ya Kiswahili. Hata hivyo, wanafunzi wengi walisema walifurahia uchambuzi wa wahusika mbinu ya maigizo ilipotumika nyakati za vipindi vya riwaya.

### 5.2.5 Changamoto Zinazokumba Ufundishaji wa Wahusika Katika Riwaya ya Kiswahili

Matokeo yalibaini uhaba wa muda ni changamoto kuu katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili. Matokeo ya uchunzaji ya vipindi kumi na sita yalionyesha mafundisho mengi kuhusu wahusika yalitawaliwa na mwalimu huku wanafunzi wakinyimwa nafasi ya kushiriki na kuchangia kikamilifu kwa namna hai. Licha ya ukweli kwamba kulikuwa na shughuli chache za maigizo zilizozingatiwa wakati

wa ufundishaji na ujifunzaji wa wahusika, sio wanafunzi wote katika vikundi walihusika kwa sababu walimu waliona ni shughuli iliyohitaji muda mwingi.

## 5.3 Hitimisho

Kwa kurejelea uchunguzi wa mbinu zinazotumiwa kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili, mbinu za mdahalo, mhadhara, mjadala wa makundi na ziara za nyanjani zilitumiwa na walimu kufundishia wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, Kaunti ya Nairobi. Kwa hivyo, kutokana na mbinu walizotumia kufundishia darasani, inaweza kuhitimishwa kuwa idadi kubwa ya walimu hawatilii umuhimu kipengele cha fasihi kwa sababu hawakushughulika kukuza mielekeo ifaao kwa wanafunzi katika uchambuzi wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

Kwa kurejelea kiwango cha matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili, ilibainika asilimia kubwa ya walimu walijikita katika matumizi ya mbinu ya mhadhara huku wachache wakitumia maigizo. Inaweza ikahitimishwa kuwa mbinu ya maigizo haikupewa kipaumbele katika ufundishaji darasani na walimu wengi wa somo la Kiswahili katika shule za upili za umma kwenye kaunti ya Nairobi. Utafiti ulihitimisha kwa kubaini kuwa walimu waliotumia mbinu ya maigizo walikuwa na ufanisi mkubwa katika ufundishaji wa kipengele cha riwaya ya Kiswahili.

Kulingana na athari ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili na matokeo bora ya wanafunzi, ni bayana kuwa mbinu ya maigizo

ilipotumika iliboresha uchambuzi wa riwaya, uelewa wa wahusika na matokeo ya Kiswahili. Utafiti huu ulihitimisha kwa kubaini kuwa matumizi ya mbinu ya maigizo yana umuhimu mkubwa katika shughuli za ufudishaji kwa sababu mwanafunzi hushiriki moja kwa moja kwa namna hai katika shughuli nzima za usomaji na ujifunzaji. Walimu wanaotumia mbinu za maigizo hutoa matokeo bora katika kipengele cha riwaya kuliko wale ambao hawaitumii.

Kwa hivyo, shughuli za uigizaji zinazojumuisha, kuigiza kwa kuiga, sanaa tuli na ufanani ni muhimu katika awamu zote za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Katika kitengo cha mitazamo ya walimu na wanafunzi kuhusu matumizi ya mbinu ya maigizo. Utafiti ulibaini kuwa wale walimu waliofurahia na kupenda kufundisha somo la Kiswahili, walitumia mbinu ya maigizo katika kufundisha kama vile sanaa tuli, kuigiza kwa kuiga na ufanani. Licha ya kufurahia matumizi ya mbinu hii, walimu wengi walilalama kwa kutoa maoni kwamba, kulikuwa na muda mfupi sana katika maandalizi ya matumizi ya mbinu ya maigizo; wengine walisema ilihusisha matayarisho mengi kabla ya kutumika. Matumizi ya mbinu hii, yanaweza yakahitimishwa kuwa wanafunzi walifurahia vipindi vya masomo ya kuigiza na walimu wengine walichangia kwa hisia zao kwamba wanafunzi walipenda masomo kama hayo japo mwisho wa vipindi hawakujifunza mengi darasani.

Kwa kurejelea chagamoto zilizokumba matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya. Somo la fasihi katika shule nyingi lilitengewa vipindi viwili pekee licha kuwa na sehemu tano; riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Hivyo shule hazikutengea walimu muda wa kutosha wa kufundisha kipengele cha riwaya ya Kiswahili

kwa sababu ya kuhofia kutohitimisha silabasi kwa muda ufaao. Utafiti ulihitimisha kuwa kufundisha kwa kutumia mbinu za maigizo kunahitaji ubunifu wa walimu sio tu kutumia vitabu vya kiada na nakala za riwaya wakati wa kufundisha. Inamhitaji mwalimu awe mbunifu katika matumizi ya rasilimali bila kuwasaza wanafunzi katika ubunifu ili vipindi kuimarika darasani waelewa kwa kina uchambuzi wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

**5.4 Mapendekezo ya Utafiti**

Mapendekezo yafuatayo yaliafikiwa na mtafiti kwa kurejelea hitimisho la utafiti

i) Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huu, vipindi vya fasihi katika shule za upili katika vimetawaliwa na mbinu ya kuuliza maswali na mihadhara. Kwa hivyo, utafiti huu unapendekeza kuwa walimu wahimizwe kutanguliza vipindi vya masomo kwa shughuli ambazo zitawachochea wanafunzi kama michezo ya kuigiza au dayalojia ili kuibua mtiririko mzuri wa mawazo na utoaji wa maoni. Walimu wanahitaji kutekeleza vipindi vyao vya masomo darasani kwa shughuli zinazochangamsha mawazo, kuuliza maswali pamoja na matumizi ya vifaa vilivyomo katika mazingira yao na mambo mengine ya kihalisia.

ii) Matokeo ya utafiti yalionyesha kwamba walimu wengi hawakutumia mbinu ya kuigiza mara nyingi walipoendesha vipindi darasani. Ni wajibu wa walimu wakuu ambao ndio viongozi wa shule kuhimiza walimu kutumia mbinu mbalimbali katika ufundishaji wa mada.Wanapaswa pia kufuatilia kuona mbinu hizo zinatumika darasani kama vile mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili ambayo inahitaji ushirikishaji wa wanafunzi inapofundishwa.

Matumizi ya mbinu ya kuigiza husaidia wanafunzi kubuni, kutoa maoni, kuwa na mawazo huria na kubaini vizuri wanachotaka kusema. Dhana hii pia hujenga mtiririko mzuri wa mawazo na kusaidia wanafunzi kugundua wanachotaka kuwasilisha kwa namna nzuri aidha kwa kuandika ama kwa kusimulia.

iii) Ilibainika matokeo ya idadi kubwa ya wanafunzi yalikuwa ya kiwango cha chini katika somo la riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi.Kwa hivyo ili kuboresha masomo na matokeo ya somo la fasihi, walimu wanapaswa kushawishiwa kubuni nyenzo bora za kufundishia ambazo zitaimarisha usomaji na ujifunzaji wa somo la riwaya kwa upeo wa cha juu. Wanafunzi waelekezwe pia kusoma na kudurusu kwa wingi vitabu na makala ya Kiswahili. Walimu wanapaswa kufundishwa jinsi ya kufundisha kwa kutumia mchezo wa kuigiza katika madarasa yao. Walimu wanapaswa kuhamasishwa kuhusu umuhimu wa matumizi ya mbinu ya maigizo na ubora wa majukumu yake katika kuathiri uelewa na uelewaji wa wanafunzi. Mara kwa mara walimu waandaliwe makongamano na semina za kuwaelekeza namna ya kuimarisha kutumia mbinu ya maigizo katika kufundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

iv) Ni dhahiri kuwa walimu wengi hawakutenga muda wa shughuli za maigizo kwa ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili. Utafiti unapendekeza wizara ya elimu ifanyie silabasi ya Kiswahili marekebisho ili pawepo na muda wa kutosha kwa wanafunzi kusoma na walimu kufunza. Walimu wanalazimika kutumia mbinu zinazowawezesha kukamilisha silabasi kwa muda mfupi iwezekanavyo kwa sababu wanalalamika somo la kiswahili lina vipengele vingi visivyoweza kukamilishwa vizuri kwa muda uliotengewa kwenye silabasi.

v) Matokeo ya utafiti yanaonyesha uhaba wa muda ni changamoto kuu katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili. Kwa hivyo, Walimu wanahimizwa kutumia mbinu za ufundishaji ambazo zinawawezesha kukamilisha silabasi kwa muda mfupi iwezekanavyo kwa sababu wanalalamika kuwa silabasi ni pana kukamilishwa kwa muda waliotengewa. Ni jukumu la washika dau wa elimu kuhakikisha silabasi inatengewa muda wa kutosha ili yaliyomo yafundishwe kwa mbinu zinazostahili kwa manufaa ya mwanafunzi. Utafiti unapendekeza kwamba walimu hawapaswi kufundisha kwa azma ya kukamilisha silabasi tu, bali kuwawezesha wanafunzi kupata ujuzi unaostahili kutoka kwa somo la fasihi ya Kiswahili.

vi) Ukubalifu wa matumizi ya mbinu ya maigizo kwa walimu na wanafunzi ni chanya. Wote wangependa mbinu ya maigizo itumiwe kufundisha riwaya ya Kiswahili.Kipengele cha wahusika katika riwaya kilitajwa na kuradidiwa kama mada muhimu kufunzwa kwa kutumia maigizo.

### 5.4.1 Mapendekezo kwa Utafiti Zaidi

1. Utafiti unaweza kufanywa kuhusu matumizi ya mbinu ya maigizo kwa kutumia vifaa vya teknolojia kufundisha wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili.
2. Utafiti zaidi unaweza kufanywa katika kaunti zingine zilizopo nchini Kenya. Tafiti hizo zinaweza kuwa sawa na utafiti huu lakini ziwe zinalinganisha zaidi jinsi ufundishaji unavyotekelezwa na walimu wanaofundisha fasihi darasani katika shule za upili.

3. Uchunguzi unapaswa kufanywa ili kubaini matumizi ya mbinu za maigizo katika kufundishia vipengele vingine vya fasihi na hata stadi tofauti za lugha.

## Marejeleo


Agonya, K., Koross, R. & Murunga, F. (2019). Influence of Teaching Methods on Students' Performance in Kiswahili Poetry in Secondary Schools in Lugari Sub-County, Kenya**.** British *Journal of Education Vol*.7, No.9, pp.105-114, September 2019

Ahmad, F. & Aziz, J. (2009). Students' Perceptions of the Teachers' Teaching of Literature Communicating and Understanding Through the Eyes of the Audience. *European Journal of social sciences, 7* (3), 17. Retrieved from www.eurojournals.com/ ejss7_3 02.pdf on 11/2/2011.

Albalawi, B. R. (2015). The Effect of Different Teaching Delivery Methods (Face-To-Face, Virtual and Blended) On Intermediate Students' Academic Achievement. *West East Journal of Social Sciences, 4*(1/2), 29-45.

Amato, P. (2007). *Make it Happen*. New York: Pearson Education.

Asfaha, Y. M., & Kroon, S. (2011). Multilingual Education Policy in Practice: Classroom Literacy Instruction in Different Scripts in Eritrea. Compare. *A Journal of Comparative and International Education*, 41(2), 229-246.

Assumpta, K.M. (2021). *Chozi la Heri: Fasihi Tambuzi ya Kiafrika, Riwaya*. Nairobi, Kenya: One Planet Publishing & Media Services

Awad, S. (2013). *Using Educational Drama and Role Playing in Teaching English in Gaza Governorates*. Gaza: The Islamic University of Gaza.

Aysun, G., Meziyet, A. & Mübeccel, G. (2013). The Effect of Drama on the Creative Imagination of Children in Different Age Groups. *Journal of Education*, 28(2), 206-220

Babusa, H. (2010). *Uchanganuzi Linganuzi wa Mielekeo na Umilisi wa Lugha ya Kiswahili wa Wanafunzi katika Mikoa ya Pwani na Nairobi Nchini Kenya* (Tasnifu ya uzaminifu haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.

Bashayer, R. (2014). *Effectiveness of Teaching English Subject using Drama on the Development of Students' Creative Thinking*. Retrieved from http://www.iosrjournals.org/iosr-jrme/papers/Vol-4%20Issue-6/Version1/H04615463.pdf

Beena L.M., Nyagah, G., Kibui, A. & Odundo, P. (2015). Effects of Dramatization on Learning of the English Language in Meru County, Kenya. *Journal of Literature, Languages and Linguistics*, *15*, 93-100.

Beena, L. M. (2016). *Effect of Dramatization on Learner Achievement in Learning English Language in Public Secondary* (Unpublished PhD thesis in Curriculum Studies). University of Nairobi Press, Kenya.

Brooks, E. na Huck, L. (1979). *Language and Thinking in School*. New York: Rinehart and Winston.

Buiaya, J., na Mkumbwa, A. (2017). Kufungamana kwa Fasihi Simulizi na Riwaya ya Kiswahili ya Kimajaribio: Uchambuzi wa Visasili katika Bina-Adamu. *Kioo cha Lugha*, *12*(1).

Burke, A. F., & O'Sullivan, J. (2002). *Stage by Stage: A Handbook for Using Drama in the Second Language Classroom*. Portsmouth, NH: Heinemann.

Bwire A. na Vikiru, I. (2008). *Approaches to the Teaching of Grammar and Vocabulary in Groenewegen Bencharks for English language Education*, Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Chepkoech, N. M. (2012). An Assessment of the Teaching Strategies Employed By English Language Teachers in Eldoret Municipality, Kenya. *Journal of Emerging Trends in Educational Research and Policy Studies, 3*(3), 352-357.

Chimerah, R. (2011). *Kiswahili Research and Development in Eastern Africa*. Mombasa, Kenya: National Museums of Kenya.

Clark, R. (2013). *Drama Techniques*. Exeter, IPC.

Clegg, J., and Afitska, O. (2011). Teaching and Learning in Two Languages in African Classrooms. *Comparative Education*, 47 (1), 61-77.

Cohen, L., Manion, L., & Morrison, K. (2011). *Research Methodology in Education* (7th ed.). New York: Routledge.

Collie, J. na Slater, S. (2000). *Literature in the Language Classroom: A Resource Book of Ideas and Activities*. United Kingdom: Cambridge University.

Crystal, D. (1997). *The Cambridge Encyclopedia of Language.* Cambridge: Cambridge University Press.

De Pauw & G.-M. de Schryver. (2008). Improving the Computational Morphological Analysis of Swahili Corpus for Lexicographic Purposes. *Lexikos*, 18:303–318.

Doff, A. (2000). *Teach English. Cambridge*: Cambridge University Press.

Dunn, J., & Stinson, M. (2011). Not Without the Art!! The Importance of Teacher Artistry When Applying Drama as Pedagogy for Additional Language Learning. *Research in Drama Education: the journal of applied theatre and performance, 16*(4), 617-633.Edition. Canada: Vicki Knight.

Eckersley, M. (2016). Using Drama to Develop Communication Skills in the 21st Century Classroom, *International Journal of Bilingual & Multilingual Teachers of English*4, No.1(July-2016).

El-Helou, H. (2010). *Difficulties Facing English Teachers in Teaching Literature in English for Palestine Grade Twelve Textbook* (Unpublished Master Thesis). Islamic University of Gaza, Palestine. Retrieved from: http://library.iugaza.edu.ps/book_details.aspx?edition_no=99085

Ellis, M. (2011). Taking A Hard Look at the Task-Based Approach: Do Learners' Speaking Skills Really Develop and If So, How? *Extending the boundaries of research on second language*. London: Macmillan

Galante, A., & Thomson, R. I. (2017). The Effectiveness of Drama as an Instructional Approach for the Development of Second Language Oral Fluency, Comprehensibility, and Accentedness. *TESOL Quarterly, 51*, 115-142.

Gall, M. D., Borg, W. R. & Gall, J. P. (2007). *Educational research: An introduction.* New York: Longman Publishers.

Gathumbi, A. Kimaliro, Mugambi, H., Bwanya, J., na Kiio, N. (2005). *New Integrated English Book. Students' Books 1, 2, 3 na 4* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Gathumbi, A. W. and Ssebbunga C. M. (2005). *Principles and Techniques in Language Teaching. A text for Teacher Educators, Teachers and Pre-service Teachers*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Glasersfeld, E. (1989). Cognition, Construction of Knowledge, and Teaching**.** *Synthese 80*(1), 121–140 (special issue on education).

Gomez, I. D. (2010). Using Drama to Improve Oral Skills in the ESL Classroom. *International School Journal*, 30 (21), 29-37.

Gorjian, B., Moosavinia, S.R. & Jabripour, A. (2010). Dramatic Performance in Teaching Drama in EFL Contexts. *The Electronic Journal for English as a Second Language*, *13*(4), 1-13. Retrieved from: http://www.tesl-ej.org/wordpress/issues/volume13/ej52/ej52a4/ [last accessed December 27, 2016)

Guthrie, G. (2010). *Basic Research Methods: An Entry to Social Science Research*. New Delhi: Sage Pulicatons India Pvt Ltd

Heather, S. (2011). *How drama facilitates Language Learning. A Case for Using Drama in the second Language Classroom* Retrieved from (http:// heatherswenddal-myefolio.com/port folio/papers).

Henson, K. (2004). *Constructivist Methods for Teaching in Diverse Middle-Level Classrooms.*

Hertzberg, M. (2009). Engaging Critical Reader Responses to Literature through Process Drama. *Reading Online, 6*(10).

Hong, L. (2010). *Using Games in Teaching English to Young Learners*. The Internet TESL Journal. Retrieved from:.*Journal of the institute of Kiswahili Research, 63*, 71-81.

Https://www.researchgate.net/publication/273602649_Book_Review_Lia_Litosseliti_ed_Research_Methods_in_Linguistics

Huitt, W. (2003). *Constructivism. Educational Psychology Interactive*. Valdosta, GA: Valdosta State University, Retrieved April 21, 2008 from http://chiron.valdosta.edu/whuitt/col/cogsys/construct.html

Isayi, P. L. (2007). The Use of Poetry in the Teaching of Language in Secondary Schools in Uasin Gishu District (*Unpublished Thesis*). Moi University, Kenya.

Kafu, P.A. (2010). *Planning for Instruction: The Secret of Effective Teaching*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Kang'ahi, M., Chisikwa, F., Omusonga, T. & Osodo, J. (2004). Teaching Styles and Learners' Achievement in Kiswahili Language in Secondary Schools. *International Journal of Academic Research in Progressive Education and Development July 2012, Vol. 1, No. 3*

Karuga, M. (2005). *Uhakiki wa Upokezi wa Fasihi ya Kiswahili ya Watoto katika Shule za Msingi nchini Kenya (*Tasnifu ya M.A Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.(

Kemboi, J. & Osman, A. (2015). Role-Play Technique as an Antecedent of Performance in English Language: Evidence from Secondary Schools in Wareng District, Uasin Gishu County, Kenya. *Journal of Education and Practice, 6*(5), 119-124.

Kenya Institute of Curriculum Development (2002). *Primary Education Syllabus* (Vol. 1). Nairobi: K.I.C.D

Kenya Institute of Curriculum Development (2016). *Kiswahili Upili. Mwongozo wa Mwalimu*. Nairobi: Kenya Institute of Curriculum Development.

Kenya Institute of Curriculum Development. (2002). *Silabasi ya Kiswahili Sekondari*. Nairobi: K.I.C.D.

Kenya National Examination Council (2005). Reports, Nairobi: KNEC

Kenya National Examination Council (2014-2018) Reports, Nairobi: KNEC

Kenya National Examination Council (2017) Reports, Nairobi: KNEC

Kenya National Examination Council (2019). 2019 KCSE Examination Report. KNEC, Nairobi.

Kiplagat, S.T. (2015). "The Use of Drama Techniques in Teaching and Learning of Kiswahili Language In Secondary Schools In Nandi South District, Kenya**."** Moi University.

Kirui, S.T. (2015). *The Use of Drama Techniques in Teaching and Learning of Kiswahili Language in Secondary Schools in Nandi South District, Kenya* (Unpublished Masters Thesis). Moi University, Kenya.

Kisanda, R. (2018). *Utilization of Drama in Teaching Kiswahili Grammar in Secondary Schools in Kimilili Sub - County, Bungoma County, Kenya* (Unpublished Master's Thesis). Moi University.

Kombo, D. na Tromp, D.L.A (2006), *Proposal and Thesis Writing, An Introduction.* Pauline Publications Africa, Nairobi.

Kothari, C. (2008). *Research Methodology (2nd Edition)*. New Delhi: New Age International.

Lorna, B. M. (2016). Effect of Dramatization on Learner Achievement in Learning English Language in Public Secondary Schools in Meru County, Kenya **(***Unpublished PhD thesis*). University of Nairobi, Kenya.

Magoma, C.M. (2011). *Curriculum Innovation in Kenya: A Case of the Introduction and Implementation of Secondary School Integrated English in Nairobi County* (Unpublished PhD Thesis). Kenyatta University, Kenya.

Mayer, R. (2004). *Should There Be A Three-Strike Rule Against Pure Discovery Learning? The Case for Guided Methods of Instruction. American Psychologist. 59 (1): 14–19. doi:10.1037/0003-066X.59.1.14. PMID 14736316.*

Mbae, J. (2004). Kenya: A Reading Nation. In Wajibu. *Journal of Social and Religious Concern*. Retrieved from: http://africa.peacelink.org/wajibu/articles/art 4487 html (3/4/2012).

Mbithe, C.N. (2014). *Influence of the New Integrated English Curriculum on Students' Performance in English at the Kenya Certificate of Secondary Education in Masinga Division, Kenya (*Unpublished MA Project). University of Nairobi, Kenya.

Mbito, J.K. (2013). *Challenges Facing Teachers and Students in the Process of Teaching and Learning Kiswahili in Public Secondary Schools in Kiambu District in Kiambu County, Kenya.* MED Project, Kenyatta University, Kenya.

Mbotela, J. (1959). *Uhuru wa watumwa*. London: Thomas Nelson and Sons LTD.

McMillan, J.H. & Schumacher, S. (2006). *Research in Education – Evidence-Based Inquiry*. (6th ed.) Boston: Pearson Education, Inc

Mgullu, R.S. (2002). *Mtaala wa Isimu.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Miima F.A (2014) Integration of Information Communication Technologies in Teaching and Learning of Kiswahili Language in Public Secondary Schools in Kakamega County, Kenya (Phd Thesis). Kenyatta University, Kenya.

Miller, A., Shoptaugh C. & Wooldridge, J. (2014) Reasons not to Cheat: Academic-Integrity Responsibility, and Frequency of Cheating. *Journal of Experimental Education* 79:169–84.

Momanyi, S.A. (2012*). Effectiveness of Teaching Methods on Students' Acquisition of Kiswahili Language Skills in Public Secondary in Manga Division* (Unpublished Master's thesis). University of Nairobi, Kenya.

Moore, M. M. (2004). "*Using Drama as an Effective Method to Teach Elementary Students" Senior* Honours Theses. Paper 113.

Msanjila, Y. P; Kihore, Y. M & Massamba, D.P.B. (2009). *Isimujamii: Sekondari na Vyuo.* Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mugenda, O. na Mugenda, A. (2013). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Research Approaches*. Nairobi: Act Press.

Muindi, M. & Mueni, K. (2002). *Instructional Methods in Education.* Nairobi: Somanga Educational Consultants.

Mukwa, C. W & Too, J. K (2002). *General Instruction Methods*. Eldoret, Moi University Press.

Munther, Z. (2013). *Using Drama Activities and Techniques to Foster Teaching English as A Foreign Language: A Theoretical Perspective (online) Al Quds Open University* (27/12/2013) retrieved from http:/www.qou.edu/English/

Murunga, F. (2013). *Influence of the Instructional Process on the Teaching and Acquisition of Listening Skills In Kiswahili Language in Kenya* (Doctoral dissertation, Moi University).

Mutembei, A. K. (2012) Korasi katika Fasihi, Nadharia Mpya ya Uhakiki (Taasisi ya Taaluma za Kiswahili). Chuo kikuu cha Dar es salaam, Tanzania.

Mwihaki, A. (2011). A Minimalist Approach to Kiswahili Syntax. *Kiswahili*, 70(1),11-23.

Nandwa, J. A. (1994). Teaching Oral Literature in the 8-4-4 System: A New Integrated Approach. In Masheti Masinjila & Okoth Okombo (eds.) *Teaching Oral Literature.* Nairobi: Kenya Oral Literature Association (Kola).

Ngunjiri, J. (2007). *Kenya's Best-Selling Authors and Titles*, Sunday Nation, September, 9, 2007. Nairobi. Nation Media Group Ltd.

Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Viziwani Zanzibar*. Nairobi: University Press

O'gara, P. (2008). To Be or Have Not Been: Learning Language Tenses through Drama. *Issues in Educational Research,* 18(2), 156-166

Oliver, R. (2000). Creating Meaningful Contexts for Learning in Web-based Settings. *Proceedings of Open Learning 2000*. (Pp; 53-62). Brisbane: Learning Network, Queensland.

Orodho, J.A. (2009). *Elements of Education and Social Science Research Methods* (2$^{nd}$ Ed.). Maseno: Kanezja Publisher.

Orodho, J.A. (2012). *Techniques of Writing Proposals and Reports in Education and Social Science.* Maseno: Kanezja Publisher.

Oseno, B. G. (2015). Teaching Speaking Skills in English Language using Classroom Activities in Secondary School Level in Eldoret Municipality, Kenya. *Journal of Education and Practice, 6*(35), 55-63.

Otunga, R. N., Odeo, I. I., & Barasa, L. P (2011). *A Handbook for Curriculum and Instruction. Eldoret*: Moi University Press.

Ozbek, G. (2014). Drama in Education: Key Conceptual Features. *Journal of Contemporary Educational Studies,* 1, 46-41.

Piaget, J. (1970). *The Development of Thought: Equilibration of Cognitive Structures*. New York: The Viking Press.

Pinter, A. (2006). *Teaching Young Language Learners*. Oxford: Oxford University Press.

Prasad, P. (2011). *The Functional Aspects of Communication Skills 4th Edition*. New Delhi: New A.S offset Press.

Prochazka, A. (2004). *Drama in Modern Language Teaching: Part 2 Follow Up*. Retrived from: https://www.kphvie.ac.at/fileadmin/Dateien_KPH/Forschung_Entwicklung/KPZ-Theaterpaed/downloads/Drama_in_MLT_2.pdf

Qorro, M. A. S. (2009). Parents and Policy Makers Insistence on Foreign Languages as Media of Education In Africa: Restricting Acess To Quality Education. – for whose Benefit? In B. Brock-Utne, & I. Skattum (Eds.), *Languages and education in Africa – a comparative and transdisciplinary analysis* (pp. 57–83). Oxford: Symposium Books.

Qorro, M. A. S. (2013). Parents' Views on the Medium of Instructions in post

Ranzau, S. (2016). *Teacher perceptions of Drama Pedagogy as a Teaching Tool* (Doctoral dissertation).

Republic of Kenya (1999). T*otally Integrated Quality Education and Training (Koech Report).* Nairobi: Government Printers.

Republic of Kenya. (2010). *Katiba ya Jamhuri ya Kenya*. Nairobi: Government Printer.

Senkoro, F.E.M.K (2011). *A Review of Various Swahili Literature Books Meant for Secondary School Students*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited, 2011

Sifuna, D.N, Chege F.N & Oanda, I.O (2006). *Themes in the Study of the Foundations of Education*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Sirengo, P.K. (2013). *The Role of Drama in the Development of Communicative Competence among Primary School Pupils in Nakuru Municipality, Kenya* (Unpublished MEd Thesis). Kenyatta University, Kenya.

Stephanie, C.W. (2011*). Activating Student Engagement Through Drama–Based Instructions.* Austin: The University of Texas.

Suter, E. & Busienei A. J. (2013). Materials and Instructional Approaches Used By Secondary School Teachers of Kiswahili Oral Literature in Marakwet District, Kenya. *Journal of Emerging Trends in Educational Research and Policy Studies* (JETERAPS) 4(3): 566-572

Suter, E. (2008); *Preparedness in Teaching Kiswahili Oral Literature in Secondary Schools in Marakwet District of Kenya.* Unpublished M. Phil thesis Eldoret, Moi University

Tam, M. (2000). Constructivism, Instructional Design, and Technology: Implications for Transforming Distance Learning.*Educational Technology and Society*, 3 (2).

Tan, P.T. (2008). Tips for Teachers: Using Mime in the Language Classroom. *TESL Reporter*, 41 (1), 56-66.

Taskin-Can, B. (2013). “The Effects of Using Creative Drama in Science Education on Students’ Achievements and Scientific Process Skills”. *IIkogretim Online.Vol. 12* (1), 120-131.

Tella, J., Indoshi, F. C., and Othuon, L. A. (2010). Relationship between Students’ Perspectives on the Secondary School English Curriculum and their Academic Achievement in Kenya. *Educational Research*. 1, 390–395. Available at: http://www.interesjournals.org/ER[Google

Teresa, L.H.Y. (2007). *Students’ Perceptions of Learning English Through Drama: A Case Study of a Hong Kong class* (MA Thesis). The University of Hong Kong, China.

Vodickova, M. (2009). Interpretation of Poetry through Drama Activities. *Journal of NELTA*, *1*(4),1-2.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wamokhela, N. C. (2012). *The role of Group Discussion in Teaching Kiswahili Literature: A case of Wareng District, Uasin Gishu County, Kenya* (M.Phil. Thesis). Moi University.

Wanjala, F. S. na Kavoi, J. M. (2013). *Stadi za Mawasiliano na Mbinu za Kufundishia Kiswahili.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Wasike, E. K. (2011). *Effects of Selected Methods of Teaching Poetry on Comprehension and Retention by Students in Secondary Schools Eldoret Municipality Schools* (Unpublished Thesis). Moi University.

Wertsch, J. V. (1997). *Vygotsky and the Formation of the Mind.* Cambridge: Harvard University Press

Yildiz N. D. & Evsen, M. D. (2013). Views of Teachers on the Use of Drama Method in Science and Technology Courses. *Turkish Online Journal of Qualitative Inquiry, 4*(2), 46-55.

Zhang, S. (2009). The Role of Input, Interaction and Output in the Developmentof Oral Fluency. *English Language Teaching*, 2(4),91–100.

Zyoud, M. (2010). *Using Drama Activities and Techniques to Foster Teaching English as a Foreign Language: A theoretical perspective.* Al Quds Open University.

# VIAMBATANISHO

## KIAMBATISHO A: HOJAJI YA MWALIMU

**Maagizo kwa walimu**

Hojaji hii inatarajia kukusanya data ya utafiti kuhusu matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundisha wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi, Kenya.Maoni yako yatasalia kuwa siri na yatatumika tu kwa shughuli ya utafiti huu. Tumia alama ya (√) kukubali au andika majibu kwenye nafasi zilizoachwa wazi

**SEHEMU A: MAELEZO YA JUMLA**

1. Jinsia yako

   Mwanamume [ ] Mwanamke [ ]

2. Umri: 18-30 [ ] 31-40 [ ] 41-50 [ ] 51-60 [ ]

3. Kiwango cha elimu

Diploma [ ] Shahada ya digrii [ ] BA/BSC pamoja na PGDE [ ]

Shahada ya uzamili [ ] BA/BSC [ ]

4. Una tajiriba ya miaka mingapi katika kufunza Kiswahili?

Miaka 0 – 5 [ ] Miaka 6 – 10 [ ] Miaka 11 – 15 [ ]

Miaka 16 – 20 [ ] Zaidi ya miaka 20 [ ]

5. Unafunza vipindi vingapi vya riwaya kwa wiki?

   1.Kipindi kimoja [ ] 4. Vinne [ ]

   2.Viwili [ ] 5. Vitano [ ]

   3.Vitatu [ ] 6. Sita [ ]

6. Je, kipindi/vipindi vilivyotengewa vinatosha ufundishaji wa riwaya?

La [   ]                                        Ndio [   ]

Toa Sababu…………………………………………………………………………

**SEHEMU B: MBINU ZA KUFUNDISHA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA**

7. Jibu kwa kuweka alama [ √ ] katika nyenzo inayorejelewa wakati wa kuchambua riwaya ya Kiswahili.

| | **Kila wakati** | **Mara moja moja** | **Situmii kabisa** |
|---|---|---|---|
| Usomaji wa kipekee | | | |
| Usomaji wa pamoja | | | |
| Usomaji wa unachopenda | | | |
| Usomaji wa kimya | | | |
| Usomaji kwa sauti | | | |
| Usomaji wa mzunguko | | | |
| Maigizo | | | |

**SEHEMU C: KIWANGO CHA MATUMIZI**

8. Je, ni mara ngapi wewe hushirikisha maigizo ya wahusika katika vipindi vya riwaya ya Kiswahili kwa mwezi?

| | (√) |
|---|---|
| Kila wakati | |
| Mara moja moja | |
| Situmii kabisa | |

9. Katika sehemu hii weka alama ya mkwaju [ √ ] kwa mbinu zilizotumiwa Kufundisha Wahusika

| Mbinu | **Mara nyingi** | **Mara chache** | **Situmii kabisa** |
|---|---|---|---|
| Majadiliano | | | |
| Kazi ya makundi | | | |
| Maigizo | | | |
| Mhadhara | | | |
| Mdahalo | | | |

**SEHEMU D: MTAZAMO WA WALIMU KATIKA UTUMIZI WA MBINU YA MAIGIZO**

10. Tafadhali jibu kwa kuweka (√) au kuandika majibu sahihi kwa nafasi zilizoachwa

Maelekezo: KK-Kukubali kabisa, K-Kukubaliana, KU-Kutokuwa na uhakika, KT-Kutokubali, KTK- kutokubali kabisa

Mitazamo kuhusu mbinu za ufundishaji

| **Mitazamo** | **KK** | **K** | **KU** | **KT** | **KTK** |
|---|---|---|---|---|---|
| Sanaa tuli, ufanani na mbinu zingine za maigizo zinahitaji mwalimu kuweka bidii zaidi katika kuandaa na kuwashirikisha wanafunzi | | | | | |
| Kuna muda mfupi sana wa maandalizi ya matumizi ya mbinu hii | | | | | |
| Mbinu ya maigizo ina shughuli nyingi mbali na vikwazo vingine | | | | | |
| Mbinu za maigizo husaidia kuelewa kwa ubatini sifa na umuhimu wa wahusika | | | | | |
| Maigizo hunipa motisha ya kufunza kwa sababu wanafunzi wanavutiwa na huelewa haraka | | | | | |

**SEHEMU E: CHANGAMOTO**

11. Ni matatizo gani wewe hukabiliana nayo unapochanganua wahusika kwenye riwaya darasani (Kwa taadhima jaza kwenye visanduku kwa kutumia alama (√ ) )

Darasa kubwa [ ]

Kukosa vifaa [ ]

Kukosa muda wa kutosha [ ]

Ukosefu wa vitabu [ ]

Mazingira duni [ ]

12. Taja changamoto zingine unazopitia wakati wa kufundisha wahusika katika riwaya

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

## KIAMBATISHO B: HOJAJI YA WANAFUNZI

**Maagizo kwa wanafunzi**

Hojaji hii inatarajia kukusanya data ya utafiti kuhusu matumizi ya mbinu ya maigizo katika kufundisha wahusika katika riwaya ya Kiswahili katika shule za upili, kaunti ya Nairobi, Kenya. Mchango wako utawekwa siri na utatumika tu kwa malengo ya utafiti huu.

**Maagizo**

**SEHEMU A: MAELEZO YA JUMLA**

1. Jinsia Kiume [ ] Kike [ ]
2. Umri………………………………………………………………………………
3. Ulipata alama ngapi katika mtihani wa mwisho wa muhula wa Kiswahili karatasi ya tatu (Fasihi)?
4. Chini ya 20 [ ] 20 – 30 [ ] 31 – 40 [ ] 41 – 50 [ ]
   51 – 60 [ ] 61 – 70 [ ] Zaidi 70 [ ]
5. Onyesha kwa alama ya kukubali (√) kiasi anachotumia mwalimu wako mbinu hizi anapochanganua wahusika katika riwaya ya Chozi la Heri darasani.

| Mbinu | Mara Nyingi | Mara Chache | Haitumii |
|---|---|---|---|
| Majadiliano | | | |
| Kazi ya makundi | | | |
| Maigizo | | | |
| Mhadhara | | | |
| Mdahalo | | | |
| Ziara nyanjani | | | |

6. Orodhesha stadi hizi kwa namna unapoelewa mwalimu afundishapo kipengele cha wahusika darasani kwa mujibu wa uchambuzi wa riwaya ya Chozi la Heri.

| **Stadi** | **Naelewa haraka** | **Naelewa wastani** | **Naelewa pole pole** | **sielewi** |
|---|---|---|---|---|
| Usomaji wa kipekee | | | | |
| Usomaji wa pamoja | | | | |
| Usomaji wa unachopenda | | | | |
| Usomaji wa kimya | | | | |
| Usomaji kwa sauti | | | | |
| usomaji kwa mzunguko | | | | |

7. Katika sehemu hii weka alama ya mkwaju [ √ ] kwa Mbinu zilizotumiwa Kufundisha Wahusika

| **Mbinu** | **Mara nyingi** | **Mara chache** | **Haitumiki kabisa** |
|---|---|---|---|
| Majadiliano | | | |
| Kazi ya makundi | | | |
| Maigizo | | | |
| Mhadhara | | | |
| Mdahalo | | | |

9.Weka alama ya kukubali (√) kuhusu mbinu inayotumika kuchambua wahusika katika zoezi linalotolewa na mwalimu katika riwaya ya Chozi la Heri darasani.

| **Mbinu** | **Kila siku** | **Kila wiki** | **Mara moja kwa mwezi** |
|---|---|---|---|
| Ufanani | | | |
| Kuigiza kwa kuiga | | | |
| Sanaa tuli | | | |

**KIAMBATISHO C: MWONGOZO WA MAHOJIANO YA WANAFUNZI**

1. Toa maoni kuhusu matumizi ya mbinu ya maigizo katika kusoma na kuelewa wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

2. Nini maoni yako kuhusu kuhusishwa kwa mbinu ya kuigiza kwa kuiga katika usomaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili?

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

3. Eleza changamoto zinazoathiri matumizi ya mbinu ya maigizo wakati wa kufunzwa na kusoma riwaya ya Kiswahili

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

4. Elezea jinsi matumizi ya mbinu ya maigizo ilivyoathiri uelewa na ujifunzaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

5. Mazoezi yapi ya mbinu za maigizo unayoyaona magumu kushiriki? Tafadhali eleza sababu

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

## KIAMBATISHO D: MWONGOZO WA MAHOJIANO YA WALIMU

1. Toa maoni kuhusu baadhi ya mbinu za ufundishaji ambazo zinaweza kutumika ili kuboresha ufundishaji riwaya katika shule ya upili.

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

2. Je, una maoni gani kuhusu matumizi ya mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili?

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

3. Je, mbinu ya maigizo imekusaidia kwa kiwango kipi kutimiza malengo ya ufundishaji wa riwaya?

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

4. Kwa maoni yako ni mbinu gani ya ufundishaji ambayo husaidia wanafunzi kukolea katika umilisi wa kusoma na kuchambua wahusika katika riwaya?

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

5. Eleza changamoto unayokabiliana nayo mbinu ya maigizo inapotumiwa wakati wa kusoma riwaya ya Kiswahili?

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
……6. Je, wewe hufurahia matumizi ya mbinu ya maigizo unapofundisha kipengele cha wahusika katika riwaya ya Kiswahili? Tafadhali fafanua jibu lako .

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

7. Je, ni kila wakati, Mara moja moja ama hutumii kabisa mbinu ya maigizo unapofundisha wahusika katika riwaya ya Kiswahili kwa kipindi cha mwezi mmoja? .
…………………………………………………………………………………………

8. Nini maoni yako kuhusu mitazamo ya wanafunzi na walimu katika matumizi ya mbinu ya maigizo katika kuimarisha usomaji wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili?

…………………………………………………………………………………………

## KIAMBATISHO E: MWONGOZO WA UCHUNZAJI DARASANI

**Nambari ya shule husika: ……………………………………………**

| **Vipindi vya masomo** | **Idadi** | (√) | | **Maoni mengine** |
|---|---|---|---|---|
| | Moja | | | |
| | Mbili | | | |
| | Tatu | | | |
| **Mbinu za ufundishaji** | **Mbinu** | **Hutumika (√)** | **Haitumiki (√)** | |
| | Kuuliza maswali | | | |
| | Mihadhara | | | |
| | Mijadala darasani | | | |
| | kazi ya makundi | | | |
| | Kusoma | | | |
| | Ufanani | | | |
| | kuiga kwa kuiga | | | |
| | Sanaa tuli | | | |
| | **Mbinu** | **Huelewa haraka (√)** | **Hawaelewi (√)** | **Maoni mengine** |
| **Wanafunzi kuelewa na kuweza kutumia mbinu ya maigizo baada ya vipindi vya riwaya.** | ufanani | | | |
| | Sanaa tuli | | | |
| | Kuigiza kwa kuiga | | | |
| **Changamoto zinazohusiana na kushiriki kwa wanafunzi katika shughuli za matumizi ya mbinu ya maigizo** | **Majibu ya wanafunzi** | **Ndio (√)** | **La (√)** | |
| | Wanafunzi wanauliza maswali kabla ya maigizo | | | |
| | Wanafunzi wanauliza maswali baada ya maigizo | | | |
| | Wanafunzi wote hushiriki | | | |

## KIAMBATISHO F: MJARABU KCSE KISWAHILI FASIHI (102/3)

**Mjarabu 1 wa Fasihi**

**Riwaya -Chozi la Heri**

***(Assumpta Matei)***

**Muda: Dakika Arubaini ( 40)**

**Maagizo:Jibu maswali yote**

1. " Hadithi yake mwanaheri ilisomeka kama ya Umu…."
   a) Eleza muktadha wa dondoo. (Alama 4)
   b) Wahusika wengi riwayani wana hadithi zinazosomeka sawa. Thibitisha. (Alama 12)
   c) Fafanua umuhimu wa mwanaheri. (Alama 4)

## MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

**Mjarabu wa 1**

**(Riwaya – Chozi la Heri)**

**1. "Hadithi yake mwanaheri ilisomeka kama ya Umu…"**

**a)** Weka dondoo hili kwenye muktadha wake.

Haya ni maneno ya mwandishi akiwarejelea Umulkheri na Mwanaheri. Mwanaheri alikuwa amemaliza kusimulia kadhia iliyokuwa imemkumba mamake, Subira mkewe Bw Kaizari. Mwandishi anatathmini kufanana na kutofautiana kwa masaibu yaliyowakabili mabanati hawa. Umu, Mwanaheri, Chandachema, Zohali na Kairu walikuwa katika bweni la shule ya Tangamano jioni wakati wa kulala walipokuwa wakisimuliana kuhusiana na aushi yao iliyofungamana na dhiki belele. (4x1= alama 4)

**b) Wahusika wengi riwayani wana hadithi zinazosomeka sawa. Thibitisha.**

i. Bw Kiriri na Lunga wanaachwa na wake zao yaani Annete na Naomi mtawalia.
ii. Bw Kiriri na Lunga wanakumbwa na dhika ilizalisha wote kufa kutokana na kihoro cha kufilisika na kuachwa na wake zao.
iii. Lunga, mzee Kero na Naomi wanapigwa kalamu kazini. Lunga anaachishwa kazi kwa kupinga ununuzi na uuzwaji wa mahindi sumu. Mzee Kero anafutwa kazi kutokana na upigaji mtindi naye Naomi anapuuzilia mbali ombi la kimbaumbau la kushiriki ngona naye.
iv. Subira na Selume wanalalama kukerwa na fitini za wakwe zao.
v. Rehema mamake Chandachema na Zohali wanaringwa wakiwa shuleni.

vi. Tuama, Tamira na Pete wanaathirika na mila za kitamaduni za kupashwa tohara.
vii. Mwangeka na Apondi wanafiwa na wapenzi wao. Mwangeka amefiwa na mkewe Lily Nyamvula naye Apondi anafiwa na Mumewe Bw Mandu.
viii. Chandachema na Pete wanalelewa na nyanya zao.
ix. Kairu na Pete wanakataliwa na baba zao. Kairu inadaiwa amezaliwa nje ya ndoa naye Pete inadaiwa hashabiani na babake.
x. Pete na Subira wanakunywa sumu ili kujitoa uhai. Hata hivyo, Pete ananusurika baada ya Selume kumhudumia naye Subira anapatikana ameaga dunia chumbani katika mji wa Karaha kando yake kukiwa na kinywaji kikali
xi. Ridhaa, Kaizari, Kangata na Wahafidhina waliomuunga Mwekevu mkono wanafurushwa kwao na kuishia kuwa wakimbizi kwenye msitu wa Mamba.
xii. Umulkheri na Mwanaheri wanaachwa na mama zao yaani Naomi na Subira.
xiii. Umu, Mwanaheri, Chandachema, Zohali na Kairu ni wanafunzi tena vijana waliopitia changamoto nyingi maishani wanajikuta kisadfa wakisomea shule ya Tangamano.
xiv. Riziki, Umu, Zohali, Chandachema na Kairu waliwahi kuokolewa na kulelewa katika makao ya watoto.
xv. Umu alitoroka kwao kama alivyo Zohali. Umu alikuwa akimhepa Sauna naye Zohali alikuwa akikimbia wazazi wake. (Zozote 12x1= alama 12)

**c) Fafanua umuhimu wa mwanaheri**

**a)** Ni mmoja kati ya wasimulizi wa Chozi la Heri.
**b)** Ametumiwa kuonyesha uwajibikaji wa viongozi.
**c)** Kupitia kwake mwandishi anaonyesha mshikamano wa kijamii.
**d)** Mwanaheri anatumiwa kuendeleza ubaguzi wa kikabila.
**e)** Anaendeleza ploti. Usimulizi wake unatupa sababu ya kuondoka kwa mama yake.
**f)** Anajenga tabia za wahusika kama vile ubinafsi wa mama yake Subira.
**g)** Kupitia kwake mwandishi anaendeleza maudhi ya malezi. Mama yao anawatekeleza yeye na Lime.
**h)** Kupitia kwake mwandishi anaonyesha jinsi vijana wanavyochangia katika kuizorotesha jamii yao.
**i)** Ametumiwa kusisitiza umuhimu wa kusuluhisha migogoro kwa njia mwafaka. (Zozote 4x1= alama 4)

**KCSE**

**KISWAHILI FASIHI (102/3)**

**Mjarabu 2 wa Fasihi**

**Riwaya -Chozi la Heri**

***(Assumpta Matei)***

**Muda: Dakika Arubaini ( 40)**

**Maagizo:Jibu maswali yote**

**1**.“Hakujali kuwa amemwacha mwenzake akitapatapa na maumivu ya kusalitiwa.”

Jadili na mwandishi wa riwaya alivyoshughulikia maudhui ya usaliti. (Alama 10)

**2**. Eleza kwa tafsili sifa za Bw Ridhaa (Alama 10)

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**Mjarabu wa 2**

**(Riwaya – Chozi la Heri)**

**1.** Hakujali kuwa amemwacha mwenzake akitapatapa na maumivu ya kusalitiwa.” Jadili na mwandishi wa riwaya alivyoshughulikia maudhui ya usaliti

i. Myunani anawasaliti raia wenzake kwa kuridhi na kuendeleza mfumo kandamizi kwa kunyakua ardhi ya kisiwa bora na kuishia kuwa masokwota.
ii. Kimbaumbau anamsaliti mfanyikazi wake Naomi kwa kumtesa, kumkata mshahara, kumsingizia wizi, kumsimanga kwa sababu ya kukataa kushiriki mapenzi.
iii. Mama Sauna anamsaliti bwana yake Bwana Kero na kuenda kuolewa na Bwana Maya.
iv. Bwana Maya anausaliti wajibu wa uzazi na kushiriki mapenzi na Sauna na kumpachika mimba.
v. Raia wa Wahafidhina wana usaliti wajibu wao wa kuendeleza uongozi kwa kupokea hongo na kuwachagua viongozi wasiostahili.
vi. Wazazi wake Zohali wanausaliti wajibu wao wa uzazi kwa kumsimanga na kumdhalilisha alipopachikwa mimba hivyo kutoroka nyumbani.
vii. Wanawake wanausaliti wajibu wao wa uzazi kwa kuavya na kuwatupa vijusi kwa mfano Neema anaokota kifusi.
viii. Wazungu walowezi wanazisaliti bidii za Waafrika kwa kuwalipa ujira duni ambao hauwawezeshi kujikimu kimaisha, kwa mfano Baba Kimondo.
ix. Wauguzi wanausaliti wajibu wao kwa wagonjwa kwa kutowatibu kwa mfano madaktari hawawatibu watoto wa wafanyakazi kama vile Kimondo.
x. Mzee Kedi anamsaliti Ridhaa kwa kuichoma familia pamoja na nyumba yake.

xi. Fumba anausaliti wadhifa wake kwa mwanafunzi wake Rehema kwa kuhusiana naye kimapenzi na kumpachika mimba.
xii. Naomi na Subira wanausaliti wajibu wao wa malezi kwa kutoroka waume wao, hivyo kuwaacha wanao taabani.
xiii. Annette anausaliti wito wa mumewe Kiriri anapoenda ughaibuni licha ya kumbembeleza abaki nyumbani.
xiv. Serikali inawasaliti raia kwa kuwauzia mahindi ambayo yameharibika hivyo kuhatarisha afya yao.
xv. Wasimamizi wa hospitali za umma wanazorotesha huduma za afya kwa kuiba dawa na kuziuzia kwenye maduka yao.
xvi. Wanafunzi wanamsaliti Ridhaa kwa kumsimanga shuleni na anaondoka kwenda kumwambia mama yake anayeongea na mwalimu wake.
xvii. Mwanzi anamsaliti Selume kwa kumkataa na kumwoa msichana wa kikwao hivyo Selume anaishia kwa upweke.
xviii. Sally anamsaliti Billy kwa kuuvunja uchumba wao kwa sababu zisizo na msingi.
xix. Fumba anamsaliti wajibu wake wa ulezi kwa kumtekeleza mwanawe Chandachema kwa mamake mzazi na kuenda kuolewa uingereza.
xx. Tenge anawasaliti wanawe pamoja na Chandachema kwa kufanya mapenzi na makahaba machoni pao na ilhali alikuwa na mkewe Kimai. Pia anamsaliti mkewe.
xxi. Baba Kipanga anausaliti wajibu wa uzazi na kumkana Kipanga kuwa mwanawe halisi hivi kumfanya Kipanga kuishia kuwa mlevi.
xxii. Bi Kangara anawasaliti watoto wadogo kwa kuwateka nyara na kuwauza madanguroni na kwa matajiri wanaowatumikisha kwenye majumba na mashamba yao.
xxiii. Halmashauri inayotoa mikopo bila ya masomo inausaliti wajibu wake bila mapendeleo. Inatoa mikopo kwa wanafunzi kutoka familia zinazojiweza kiuchumi na kuwaacha wana wa maskini kufanya vibarua ili kugharamia mahitaji mengine. ( Zozote 10 x1= alama 10)

**2. Eleza kwa tafsili sifa za Bw Ridhaa**

i. Amesawiriwa kama mhusika mwenye *machungu* katika nafsi,kutokana na kuuliwa kwa mkewe Terry, mkaza mwana, wanawe na mjukuu wake. Alipoteza majumba yake mawili yalibomolewa na serikali kwa sababu ya kujengwa kwa ardhi ya umma. Baada ya vita vya ndani kutibuka ilimlazimu kuhamia msitu wa Mamba. Aliporejea nyumbani. Alikata uamuzi wa kujengahospitali ya Mwanzo mpya katika kitovu cha gofu la jumba lake.

ii. Mshirikina – Aliingiwa na kiwewe aliposikia mlio wa bundi na kereng'ende. Pamoja na Kunguru wengi kutua kwa paa la maktaba yake. Tunaona mkewe Terry akimkejeli kuwa anashangaa jinsi daktari mzima akijishughulisha na mambo ya kishirikina ya mwanaye. Aila yake na Mwangeka ilipochomwa. Alikataa katakata kuyazika majivu ya mabaki yao.

iii. Mcha mungu – Anamueleza Mwangeka kuwa alimuomba Maulana kila uchao aweze kurejea nyumbani salama. Alipiga dua hilo ili Mwangeka aendeleze ukoo wake baada ya mjukuu wake na wanawe wengine kuaga dunia. Terry anasema kuwa mumewe alimhimiza kukabiliana na matokeo ya maisha. Pia wamlaani shetani aliyejaribu kuzuia mafanikio yao.

iv. Msomi – Alisoma hadi chuo kikuu. Alifuzu kwa shahada ya udaktari na uzamili katika taaluma ya upasuaji. Elimu yake na juhudi zake kazini zilimpa furasa ya kuwa mkurugenzi wa mashirika mbalimbali yaliyohusiana na huduma za afya.

v. Mwepesi wa hasita – Wanafunzi wenzake wa shule ya msingi walipojaribu kumsomea alichukua mkomba wake na kufululiza moja kwa moja hadi mastakimuni. Alipofika alijitupa chini mchangani na kumpasulia mamaye kuwa hangerudi tena katika shule hiyo mpya wala kuwaruhusu wamtanie na kumcheka tena. Aliingiwa na hasira alipowatazama wanawe wakiingiza mazishi ya Dede. Alihisi kama angewasagasaga. Mwandishi anasema alivua mshipi wake na kumcharaza Mwangeka vilivyo.

vi. Mkarimu – Alidhamini elimu ya wapwa wake wawili vilevile alijizatiti kwa udi na ambari kuhakikisha kuwa kijiji kizima kilipata maji ya mabobma kwa hisani na gharama yake. Alijenga kituo cha afya cha Mwanzo mpya katika ganjo lake. Kituo hiki kiliwafaa raia wengi ambao hawakumudu gharama za matibabu. Katika hospitali za kibinafsi na za umma.

vii. Mwenye majuto – Alijuta kwa yale mengi mema aliyowafanyia wakazi wa msitu wa Heri, lakini nao shukuran yao ikawa kuua jamaa wake.

*viii.* Mwenye utani – Alisema kuwa chepeo yake na mwanya wa meno ya ndio ulimvutia Terry kumkubali amchumbie. *"Chepeo hii ndiyo ilikupa usingizi wa mang'amung'amu siku hizo" uk 34.*

ix. mwenye taasubi ya kiume – Alimweleza Tila kuwa itamlazimu aridhike na kiongozi wao wanaume kwa kuwa wakati wa mwanamke kuchaguliwa haikuwa imetimia.

x. Msiri – Alipofika nyumba, ilisadfu Mwangeka, Tila na watoto wengine walikuwa wakiigiza mazishi ya Dede. Alijibanza kwenye kimbaza cha jiko kushuhudia mazishi hayo bila kuwakaripia waombolezaji wa utani.

xi. Mwenye tamaa – Alikuwa na uchu kuona mwanaye Mwangeka amefunga akidi tena. Suala hili lilimfanya kushusha pumzi Mwangeka alipofunga tena pingu za maisha na Bi Rachael Apondi.

xii. Mwenye bidii – Alijitahidi kwa udi na umbari kuona kijiji cha msitu wa Heri kilipata maji ya mabomba. Baada ya baadhi ya wakimbizi kurejeshwa kwa makao yao asilia. Ridhaa alititahidi kajenga kituo cha afya cha mwanzo mpya kwa manufaa ya makabaila kupata matibu bora bila gharama. ( Zozote 10 x1= alama10)

**KIAMBATISHO G: MTIHANI WA KCSE MASWALI YA FASIHI 2015 – 2019**

***SEHEMU YA B: RIWAYA -2015***

*K.Walibora:Kidagaa Kimemwozea*

*Jibu swali la 2 au 3*

*2. "Moyo ulimpapa na kijasho chembamba kumtekenya juu ya mwanzi wa pua. Akahisi uchungu wa mwiba wa kujidunga."*

*(a) Eleza muktadha wa dondoo hili.* *(alama 4)*

*(b) Huku ukirejelea riwaya hii, fafanua kwa kutoa hoja nane, namna anayelengwa na kauli hii alivyojidunga.* *(alama 16)*

*3. (a) "Imani ni kielelezo cha vijana waliowajibika." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea mifano kumi kutoka Kidagaa Kimemwozea.* *(alama 10)*

*(b) "Nadhani Mzungu pale alipo hana budi* kutambua *<u>ukomavu Wa Mwafirika katika kila sekta ya maisha</u>"*

*Onyesha kinyume katika kauli iliyopigiwa mstari kwa kurejelea uongozi wa Tomoko (alama 10)*

***SEHEMU YA B: RIWAYA -2016***

*K.Walibora:Kidagaa Kimemwozea*

*Jibu swali la 2 au 3*

*2. Fafanua majukumu ya elimu na dini katika jamii kwa mujibu wa riwaya: Kidagaa Kimemwozea.* *(*alama *20)*

*3. "Wasemao husema, atafutaye hachoki."*

*(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili.* *(*alama *4)*

*(b) Kauli hii ina maana gani kwa mujibu wa muktadha huu.* *(*alama *2)*

*(c) Jadili umuhimu wa kinachotafutwa katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea.* *(*alama *14)*

***SEHEMU YA B: RIWAYA -2017***

*K.Walibora:Kidagaa Kimemwozea*

*Jibu swali la 2 au 3*

*2. "Lakini waliogopa … Waliogopa hata kuwa na uoga."*

*(a) Eleza muktadha wa dondoo hili.* *(alama 4)*

*(b) Bainisha tamathali moja ya usemi ambayo imetumiwa katika dondoo hili. (alama 2)*

*(c) Kwa kurejelea hoja kumi na nne kutoka kwenye riwaya hii, thibitisha kwamba raia wa Tomoko walistahili kuogopa hata kuwa na uoga'* *(alama 14)*

*3. (a) "Usinivue nguo kwa macho yako wee!"*

*Kwa kurejelea hoja kumi na mbili kutoka kwenyc riwaya hii, thibitisha kwamba mzungumzaji anastahili kuvuliwa nguo.* *(alama 12)*

*(b) Tathmini umuhimu wa barua ya Ben Bella kwa Mashaka katika kuijenga riwaya hii.* *(alama 8)*

***SEHEMU YA B: RIWAYA -2018***

*K.Walibora:Kidagaa Kimemwozea*

*Jibu swali la 2 au 3*

*2. Riwaya hii ya aina yake inathibitisha kwa usanii wa kupigiwa mfano jinsi ndoto ya uhuru barani Afrika imegeuka kuwa jinamizi;*

a) *Eleza wa dondoo hili* (alama 4)

b) *Onyesha jinsi ndoto ya uhuru barani Afrika imegeuka kuwa jinamizi kwa kurejelea wahusika wafuatao:*

i) *Majisifu* (alama 8)

ii) *Fao* (alama 4)

iii) *Wahudumu wa zahanati ya Nasaba Bora* (alama 4)

*3. "Leo usukani uko mikoni mwetu wenyewe.Mbeberu ameshang'olewa pamoja na mizizi yake"*

a) *Onyesha kinaya katika kauli hii kwa kutoa mifano kumikutoka kwa Kidagaa Kimemwozea* (alama 10)

b) *Tathimini mchango wa wanyonge katika kuzorota kwa hali ya maisha yao* (alama 10)

## *SEHEMU YA A: RIWAYA -2019*

*A.MATEI:Chozi la Heri*

*1.***Swali la lazima**

***a)*** *"Sasa haya ameyapa kisogo…kufunguliwa kwa kituo hiki ni kama mana iliyomdondokea kinywani kutoka mbinguni"*

*i)* *Eleza muktadha wa dondoo hili* *(*alama *4)*

*ii)Bainisha tamathali mbili za semi ambazo zimebainishwa katika dondoo hili (*alama *2)*

*ii)* *Fafanua umuhimu wa mhusika anayerejelewa katika dondoo hili katika kuijenga riwaya hii* *(*alama *6)*

***b)*** *Jadili mikakati mwafaka ambayo vijana wanatumia kukabiliana na hali yao ya maisha kwa kuwarejelea wahusika wafuatao*

*i)* *Chandachema* *(*alama *4)*

ii) *Dick* *(*alama *4)*

# KIAMBATISHO H: IDHINISHO

**KENYATTA UNIVERSITY**
**GRADUATE SCHOOL**

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

**P.O. Box 43844, 00100**
**NAIROBI, KENYA**
**Tel. 020-8704150**

**Internal Memo**

**FROM:** Dean, Graduate School **DATE:** 1st December, 2020

**TO:** **Mr. Kikechi Kombo Batholomew**
**C/o Department of Educational**
**Communication & Technology**

**REF:** E55/CE/22908/2010

**SUBJECT: APPROVAL OF RESEARCH PROPOSAL**

=====================================================

This is to inform you that Graduate School Board, at its meeting on **18th November, 2020,** approved your Research Proposal for the M.Ed. Degree entitled, **"Matumizi ya Mbinu ya Maigizo Katika Ufundishanji wa Wahusika Katika Riwaya ya Kiswahili Katika Shule za Upili, Kwenye Kaunti ya Nairobi, Kenya."**

You may now proceed with your Data collection, subject to clearance with the Director General, National Commission for Science, Technology & Innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed Supervision Tracking and Progress Report Forms per semester. The forms are available at the University's Website under Graduate School webpage downloads.

Thank you.

**HARRIET ISABOKE**
**FOR: DEAN, GRADUATE SCHOOL**

CC. Chairman, Department of Educational Communication & Technology

**Supervisors:**

1. Dr. Omar Babusa
   C/o Department of Educ. Communication & Technology
   **Kenyatta University**

2. Dr. Florence Miima
   C/o Department of Educ. Communication & Technology
   **Kenyatta University**

## KIAMBATISHO I: IDHINISHO

**KENYATTA UNIVERSITY**
**GRADUATE SCHOOL**

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke

Website: www.ku.ac.ke

**P.O. Box 43844, 00100**
**NAIROBI, KENYA**
**Tel. 020-8704150**

**Our Ref: E55/CE/22908/2010**

**DATE: 1st December, 2020**

Director General,
National Commission for Science, Technology
and Innovation
P.O. Box 30623-00100
**NAIROBI**

Dear Sir/Madam,

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR MR. KIKECHI KOMBO BATHOLOMEW – REG. NO. E55/CE/22908/10**

I write to introduce Mr. Kikechi Kombo Batholomew who is a Postgraduate Student of this University. He is registered for M.Ed. degree programme in the **Department of Educational Communication & Technology.**

Mr. Kikechi intends to conduct research for a M.Ed. thesis Proposal entitled, **"Matumizi ya Mbinu ya Maigizo Katika Ufundishanji wa Wahusika Katika Riwaya ya Kiswahili Katika Shule za Upili, Kwenye Kaunti ya Nairobi, Kenya."**

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

**PROF. ELISHIBA KIMANI**
**DEAN, GRADUATE SCHOOL**

## KIAMBATISHO J: KIBALI CHA UTAFITI

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **781548**

Date of Issue: **06/January/2021**

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Mr.. Batholomew Kombo Kikechi of Kenyatta University, has been licensed to conduct research in Nairobi on the topic: MATUMIZI YA MBINU YA MAIGIZO KATIKA UFUNDISHAJI WA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI, KWENYE KAUNTI YA NAIROBI, KENYA MATUMIZI YA MBINU YA MAIGIZO KATIKA UFUNDISHAJI WA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI, KWENYE KAUNTI YA NAIROBI, KENYA for the period ending : 06/January/2022.**

License No: **NACOSTI/P/21/8327**

**781548**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

National Commision for Science, Technology and Innovation -

**KIAMBATISHO K: RAMANI YA NAIROBI (ENEO LA UTAFITI)**

